Jumatatu Julai 1, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579958

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


NIPASHE JUMATATU JULAI 1 2019

Nipashe **Spotika**

SABABU STARS KUWA YA KWANZA KUAGA AFCON UK.18

ISIKUPITE

Aaron Wan-Bissaka ambaye ametua Old Trafford kwa pauni milioni 50 akitokea Crystal Palace, ambapo sasa atakuwa akilipwa pauni 80,000 kwa wiki, anakuwa mchezaji wa tano kununuliwa kwa dau kubwa Manchester United baada ya Paul Pogba, Romelu Lukaku, Angel di Maria na Fred.

SAMBARATISHA...

Beki wa Peru, Carlos Zambrano, akiwahi kuucheza mpira kwa kichwa dhidi ya mshambuliaji wa Uruguay, Luis Suarez kwenye mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano ya Copa America iliyopigwa Salvador, Brazil na Peru kushinda kwa mikwaju ya penalti 5-4. HABARI UK. 15

UKURASA 13



## RIPOTI MAALUM

## Siri ugumu kunguni kufa, wanavyotesa familia nyingi

UK. 4

# Chadema yamwendea Tundu Lissu mahakamani

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**WADAU SEKTA KILIMO WAJA NA MAMBO 10**

WAKATI serikali ikifanya maboresho ya sera ya kilimo ya mwaka 2013, wadau wa kilimo nchini wametoa mapendekezo katika maeneo 10 yanayopaswa kufanyiwa maboresho, mojawapo ni upatikanaji wa mbegu ...

UKURASA WA 23

**DIASPORA KUJENGA DARAJA DAR- Z'BAR**

UONGOZI wa Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) uko tayari kusimamia ujenzi wa daraja refu la kisasa lenye uwezo wa kuunganisha miji miwili ya Dar es Salaam na Zanzibar katika harakati za kuimarisha uchumi na mawasiliano.

## UMASKINI BADO TISHIO VIJIJINI

UK. 3

**HONGERA**




Mgeni rasmi katika sherehe za utoaji Tuzo za Umahiri katika Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2018, Professa wa Sheria wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chris Peter Maina (kushoto) akimkabidhi mfano wa hundi mshindi wa jumla wa mashindano hayo, Mwandishi wa Habari Mwandamizi wa gazeti la Nipashe, Salome Kitomari katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Jackton Manyerere, mmoja wa washindi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nipashe yazoa tuzo za umahiri

**Yatoa** mshindi wa jumla aliyefichua uonevu kikokotoo kipya mafao ya wastaafu...*Endelea uk. 2*

**MICHEZO** **MORIS KUPASULIWA GOTI CAIRO** UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Wadau sekta kilimo waja mambo 10

**Na Gwamaka Alipipi**

WAKATI serikali ikifanya maboresho ya sera ya kilimo ya mwaka 2013, wadau wa kilimo nchini wametoa mapendekezo katika maeneo 10 yanayopaswa kufanyiwa maboresho, mojawapo ni upatikanaji wa mbegu bora na pembejeo. Wakizungumza na waandishi wa habari Mjini Morogoro mwishoni mwa wiki, wadau hao wakiongozwa na Jukwaa huru la Wadau wa Kilimo (Ansaf), walieleza kuwa sera ya kilimo ya mwaka 2013 imekuwa na changamoto nyingi kwa wakulima nchini.

Baadhi ya wadau hao ni Chama cha Wakulima Tandahimba (Tafa), Action Aid Tanzania, Chama cha wafanyabiashara, wasindikaji na wasafirishaji wa mboga, viungo, matunda na maua nchini (TAHA), Mtandao wa asasi zisizo za kiserikali mkoani Arusha (Anglonet), Chama cha Maendeleo Mwanasatu (Mwado), Taasisi ya wajasiriamali vijijini, chama cha wafugaji jamii ya Kimaasai (MPDO-Lareto), pamoja na Katani Ltd.

Mkurugenzi Mtendaji wa Ansaf, Audax Lukonge, alisema kwenye sera mpya inapaswa kueleza namna ya kudhibiti upotevu wa mazao wakati wa kuvuna.

"Tunashauri sera ihimize serikali na wadau waweke mkazo katika kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kupunguza upotevu wa mazao kwenye mnyororo wa thamani, vipaumbele viwekwe katika kuhimiza upatikanaji wa elimu kwa wadau, teknolojia za uhifadhi, miundombinu ya uhifadhi katika maghala na vihenge," alisema Lukonge.

Alisema sera mpya pia itambue umuhimu wa upatikanaji wa takwimu sahihi za kilimo na uwapo wa wadau mbalimbali, alisema kunapaswa kuboreshwa dawati la sekta binafsi pamoja na kundwa kwa dawati maalumu la vyama vya wakulima na ushirika kwa maendeleo ya kilimo.

Pendekezo lingine ni kuwapo kwa msukumo zaidi kwenye upatikanaji na matumizi bora ya mbegu na pembejeo muhimu za kilimo, huduma za ugani, tafiti, na matumizi bora na endelevu ya udongo kwa mazao mbalimbali ili kuongeza tija katika uzalishaji.

Lingine ni serikali kutunga sheria ya kulinda ardhi ya kilimo, kutambua na kuheshimu maeneo yaliyotengwa mahsusi kwa shughuli za kilimo nchini, ambapo sheria hiyo iendane na mipango ya matumizi bora ya ardhi, hati miliki, mazao ya kipaumbele na mabadiliko ya tabia nchi. Pia sera iweke mazingira rafiki yatakayohakikisha uwapo na ukuaji wa viwanda vya ndani kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo ya Kilimo (ASDPII) na mwongozo wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Kadhalika, sera iongeza nguvu kwenye mpango wa utekelezaji wa mkakati wa kushirikisha vijana kwenye kilimo biashara. "Sera ya kilimo inatambua umuhimu wa miundombinu katika maendelo ya kilimo. Ili kukuza kilimo kunahitajika kuwekeza kwenye miundombinu ya nishati, umwagiliaji, usafirishaji wa mazao vijijini, masoko na hifadhi ya mazao na mashirika," alisema Lukonge. Alisema sera ya kilimo inatambua umuhimu wa kuongeza bajeti ya kilimo na bima ya mazao, hivyo serikali inapaswa kutoa asilimia 10 ya bajeti itakayokwenda kwenye kilimo pamoja na uharakishwaji wa kuanzisha bima ya mazao.


# Nipashe yazoa tuzo za umahiri



Ashton Balaigwa



Elizabeth Zaya



Aisia Rweyemamu



Marco Maduhu



Sanura Athanas



Rahma Suleiman



Felister Peter

**Na Mwandishi Wetu**

NIPASHE imeng'ara katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari kwa mwaka 2018 baada ya waandishi wake sita kushinda tuzo na kutoa mshindi wa jumla wa mashindano hayo.

Tuzo hizo zinazoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) kwa kushirikiana na washirika wake, zilitolewa jijini Dar es Salaam juzi usiku.

Katika hafla ya utoaji wa tuzo hizo iliyohudhuriwa na Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, mwandishi wa gazeti hili, Salome Kitomari, alitangazwa mshindi wa jumla na kupewa zawadi ya Sh. milioni tatu. Kabla ya kutwaa tuzo hiyo kubwa, Salome aliibuka mshindi wa kwanza katika vipengele vya Habari za Uchunguzi na Kundi la Wazi.

Salome pia alishika nafasi ya pili katika kipengele cha Habari za Gesi, Mafuta na Madini ambacho Manyerere Jakton wa gazeti la Jamhuri aliibuka mshindi.

Moja ya habari zilizompa ushindi Salome ni kuhusu sakata la mabadiliko ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu nchini.

Waandishi wengine wa Nipashe waliong'ara katika tuzo hizo ni Sanula Athanas, aliyeibuka mshindi kwenye kipengele cha Habari za Uchumi, Biashara na Fedha.

Mwandishi wa gazeti hili mkoani Shinyanga, Marco Maduhu alishika nafasi ya tatu katika kipengele cha Habari za Wazee. Mwakilishi wa Nipashe mkoani Morogoro, Ashton Balaigwa, alitangazwa mshindi wa tatu katika vipengele vya Habari za Utalii na Uhifadhi pamoja na Habari za Kilimo.

Mwandishi mwingine wa Nipashe, Elizabeth Zaya, alishika nafasi ya tatu katika Uandishi wa Habari za Watoto.

Mwakilishi wa Nipashe visiwani Zanzibar, Rahma Suleiman, alishika nafasi ya pili katika Uandishi wa Habari za Elimu.

Waandishi wawili wa The Guardian, gazeti dada wa Nipashe; Felister Peter na Aisia Rweimamu pia waling'ara katika tuzo hizo.

Felister alishika nafasi ya pili katika Uandishi wa Habari za Uchumi, Biashara na Fedha wakati Aisia alishika nafasi ya tatu kwenye Uandishi wa Habari za Usalama Barabarani.

**TUZO ALIZOWAHI KUSHINDA SALOME**

Ameshinda tuzo mbalimbali ikiwamo ya habari za kilimo cha kahawa iliyotolewa na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Kilimanjaro (TaCRI), mwaka 2011, 2012 na 2013 alishinda tuzo ya uandishi wa habari za utalii iliyokuwa inaandaliwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa).

Alianza kushiriki tuzo za EJAT mwaka 2010 na mwaka 2012 aliibuka mshindi katika kipengele cha uandishi wa habari za watu wenye ulemavu, na mwaka 2015 alikuwa mshindi wa pili katika habari za uchunguzi.

Mwaka 2016 aliibuka mshindi katika kipengele cha habari za uchunguzi, 2017 aliibuka mshindi katika kipengele cha habari za Utalii na Uhifadhi.

Mwaka 2018 alishinda katika vipengele vya habari za uchunguzi, kundi la wazi na tuzo ya jumla ya umahiri katika uandishi wa habari.

# Chadema yamwendea kortini Lissu

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesema kitaenda mahakamani ili kupata tafsiri ya kisheria kuhusu sababu zilizotolewa na Spika wa Bunge, Job Ndugai kumvua ubunge Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu.

Akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya chama hicho, jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji, alisema kuwa chama hicho kimeshaandika barua ya kuomba nakala ya uamuzi uliotolewa na Spika Ndugai kuitaarifu Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa jimbo hilo lipo wazi.

"Chama kimeamua kwenda mahakamani ili mahakama itafsiri kwa usahihi sheria na haki ionekane ikitendeka katika suala hili," alisema Dk. Mashinji na kuongeza:

"Tayari tumeagiza Kurugenzi ya Sheria kwa kushirikiana na wanasheria wengine kuanza maandalizi mara moja ya kutekeleza uamuzi huu kwa mahakama za ndani na kimataifa."

Akizungumza bungeni Ijumaa Ndugai alisema mambo mawili yaliyosababisha Lissu kupoteza sifa za kuendelea kuwa mbunge ni kutotoa taarifa kwake (Spika) ya mahali aliko na kutojaza fomu za maadili ambazo hujazwa na wabunge kila mwaka.

"Nimetumia kifungu cha 37(iii) sura ya 343 ya Sheria ya Uchaguzi inayonitaka kumpa taarifa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikiwa kuna jimbo ambalo liko wazi kwa mujibu wa Sheria," alisema Ndugai.

Akifafanua kuhusu sababu ya utoro bungeni iliyotolewa na Spika Ndugai katika kufikia uamuzi wa kumvua Lissu ubunge, Dk. Mashinji alidai chama hicho kina taarifa za mawasiliano rasmi ya kiserikali kupitia nyaraka kati ya Ofisi ya Katibu wa Bunge na familia ya Lissu kuhusu matibabu yake nchini Ubelgiji.

"Hapa Spika anataka kuwaambia Watanzania kuwa Ofisi ya Katibu wa Bunge na Ofisi ya Spika na Spika mwenyewe hawana mawasiliano ya kikazi kiasi Katibu wa Bunge anajua Lissu alipo na Spika hajui?" Alihoji Dk. Mashinji.

Kuhusu kutokujaza fomu za Maadili ya Umma ambazo hujazwa na wabunge kila mwaka, Dk. Mashinji alisema kuwa kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi, mamlaka yenye wajibu wa kusimamia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

"Swali hapa ni je, lini Sekretarieti ya Maadili ya Umma imempelekea wito wa kumtaka Lissu afike kuhojiwa au kusikilizwa kabla ya kuchukuliwa hatua?" Dk. Mashinji alihoji.

Lissu ambaye bado yupo Ubelgiji kwa matibabu, amepanga kurejea nchini Septemba 7, mwaka huu, tarehe ambayo mwaka 2017, alishambuliwa kwa kupigwa risasi zaidi ya 30 na watu wasiojulikana jijini Dodoma akiwa ndani ya gari nyumbani kwake Area D hao wakati akitoka bungeni.

Baada ya shambulio hilo, Lissu ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kwa matibabu ya awali na siku hiyo hiyo usiku alihamishiwa katika hospitali moja mjini Nairobi, Kenya.

Lissu ambaye pia ni Mwanasheria Mkuu wa Chadema, alikaa siku 121 hospitali ya Kenya hadi Januari 6, mwaka jana, alipohamishiwa hospitali nyingineUbelgiji ambako Desemba 31, alimaliza matibabu yake ya awali na kuanza ziara nchi mbalimbali.

## HABARI KITAIFA

# Umaskini bado tishio vijijini, Rukwa kinara

**Augusta Njoji na Paul Mabeja,** DODOMA

UTAFITI wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi kwa mwaka 2017/18, umebaini kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi kwa maeneo ya vijijini bado ni mkubwa ikilinganishwa na mijini.

Kwa mujibu wa matokeo ya viashiria muhimu vya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi Tanzania Bara 2017/18 yaliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) juzi, yalionyesha kuwa pamoja na umaskini wa mahitaji ya msingi kupungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18, lakini maeneo ya vijijini bado ni mkubwa.

Umaskini huo ni mkubwa kwa maeneo ya vijijini kwa asilimia 31.3 ikilinganishwa na maeneo ya mijini kwa asilimia15.8.

Aidha, matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa mkoa wa Rukwa una kiwango kikubwa cha umaskini wa mahitaji ya msingi kwa asilimia 45, wakati mkoa wa Dar es Salaam una kiwango kidogo cha umaskini kwa asilimia 8.

Kwa upande wa mikoa mingine, Dodoma asilimia 23.2, Arusha (24.7), Kilimanjaro (10.5), Tanga (21), Morogoro (19.3), Pwani (27.9), Lindi (38), Mtwara(29.1), Ruvuma (30.6), Iringa (24), Mbeya (21.4), Singida (34), Tabora (34.5), Kigoma (34.5), Shinyanga (31.9), Kagera (31.9), Mwanza (34.6), Mara (23.2), Manyara (30.5), Njombe (13.2), Katavi (29), Simiyu (39.2), Geita (37.5) na Songwe (20.7).

Chakula vijijini

Kwa upande wa chakula, kiwango cha umaskini wa chakula kimepungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/12 na kufikia asilimia 8.0 mwaka 2017/18, huku umaskini wa chakula ni mkubwa maeneo ya vijijini kwa asilimia 9.7 ikilinganishwa na maeneo ya mijini kwa asilimia 4.4.

Umaskini wa chakula kwenye mikoa Dodoma asilimia 3.7, Arusha (7.6), Kilimanjaro (2.1), Tanga (8), Morogoro (4.3), Pwani (12.1), Dar es Salaam (2.3), Lindi (15.3), Mtwara (9), Ruvuma (6.6), Iringa (8), Mbeya

INAENDELEA UK. 26



Mkurugenzi wa Masoko na Utafiti wa Benki ya CRDB, Tully Mwambapa, akimkabidhi tuzo mshindi wa kundi la Habari za Usalama Barabarani Bety Tesha kutoka TBC katika sherehe ya kukabidhi Tuzo za Umahiri katika Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2018 zilizofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TPA kutoa mrabaha wa bil. 200/- serikalini

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), imeongeza makusanyo yake kutoka Sh. bilioni 818 mwaka 2017/19 na kufikia zaidi ya Sh. bilioni 900 mwaka 2018/19.

Mkurugenzi wa TPA, Deusdedit Kakoko, aliyaeleza hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuwa ongezeko hilo ni zaidi ya Sh. bilioni 90 kwa kipindi cha mwaka mmoja.

"Mapato yatokanayo na Bandari yameongezeka kwa zaidi ya Sh. bilioni 90 ingawa bado hatujafunga hesabu hadi leo (jana), kutoka Sh. bilioni 818 mwaka 2017/18 hadi Sh. bilioni 900 ambazo tumeshakusanya hadi sasa na tunaamini tukifunga hesabu yatakuwa yameongezeka," alisema Kakoko.

Aidha, alisema katika mwaka huu wa fedha uliomalizika jana, wanatarajia kutoa mrabaha serikalini wa zaidi ya Sh. bilioni 200.

"Tunatarajia kutoa mrabaha kwa serikali si chini ya bilioni 200 ambazo ni nje ya kodi ya taasisi nyingine za umma na halmashauri zetu na mwaka jana tuliongoza naamini na mwaka huu tutaongoza," alisema Kakoko.

Alisema sababu za kuongezeka kwa mapato hayo ni maboresho yanayoendelea kufanywa katika bandari zote

INAENDELEA UK. 8

# Kipunguni wacharuka, wamtaka Prof. Mbarawa

**Na Beatrice Moses**

WAKAZI wa Kipunguni jijini Dar es Salaam wanaosubiri kulipwa fidia ili kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege, wamecharuka na kumtaka Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Prof. Makame Mbarawa, kwenda kuwapa majibu ya lini serikali itawalipa fedha zao.

Wamechukua hatua hiyo baada ya kusubiri kwa zaidi ya miaka 20.

Hali hiyo ilitokea juzi wakati wakazi hao walipoalikwa kwenye mkutano ulioandaliwa na Mbunge wa Segerea, Bonna Kamoli, ambapo Prof. Mbawara alipaswa kufika kuwapa majibu ya maswali yao kuhusu fidia ya nyumba zao ambazo nyingi zilifanyiwa tathmini tangu mwaka 1997.

Wakazi hao walijitokeza kwa wingi kuitikia wito wa mbunge wao, lakini walipofika katika mkutano huo walibaini Waziri Mbarawa hayupo kama walivyotarajia, wengi walikerwa na hatua hiyo.

Licha ya Mbunge kuwa tayari kufanya nao mazungumzo kama mwakilishi wao, hawakuwa tayari baadhi waliopata nafasi ya kutoa maoni yao walieleza wazi kuwa Waziri Mbarawa ndiye wanayemtaka ili awape majibu kutoka serikalini.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kipunguzi, Praxeda Mkandara, aliwatangazia wananchi hao kuahirishwa kwa mkutano huo hadi watakapoarifiwa tena, akieleza kuwa taarifa walizonazo ni kwamba waziri amepata dharura amekwenda Bandari ya Dar es Salaam kuna tishio la mgomo wa madereva.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili mwenyekiti huyo alieleza kuwa tatizo hilo limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi, imedumaza maendeleo yao huku baadhi ya wananchi wa Kipunguni Mashariki wakiamua kuendelea na ujenzi wa nyumba zao wakitarajia kufanywa

INAENDELEA UK. 8


IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MOSHI DISTRICT REGISTRY
AT MOSHI

LABOUR EXECUTION NO.6 OF 2019
GRACE PETER ............DEGREE HOLDER
VERSUS
IMARA DRILLING AND
FARMING CO.LTD.........JUDGEMENT DEBTOR

TO:
IMARA DRILLING AND FAMING CO.LTD.
WHEREVER YOU ARE.

NOTICE FOR MENTION.

TAKE NOTICE: That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 2nd July 2019 at 09:30 am before Honourable F.H. Mahimbali -Deputy Registrar.
WHEREAS: Service on you has been ordered to be published in the Nipashe newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
TAKE FURTHER NOTE THAT in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
GIVEN UNDER my hand and seal of the Court this 13th day of June, 2019

F.H. Mahimbali
Deputy Registrar



**KUPOTELEWA NA LESENI YA UCHIMBAJI MADINI**

**MARIAM EMANUEL SHAURI,**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA LESENI YA UCHIMBAJI WA MADINI YENYE JINA LA KHALID JUMA MANDIA YENYE NO,PML 000926NZ.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI .

**POLISI TAARIFA : BNG/RB/3142/2019**



**alkhalij enterprises Limited**

**JOB OPENING**

**SALES EXECUTIVE**

**Roles and Responsibilities:**

- Present and sell the Company's products and solutions to new and existing accounts
- Accountable for ensuring timely communication and customer satisfaction at assigned accounts
- Understand each customer's business and technical applications, anticipating their needs for products and solutions
- Establish and strengthen individual relationships within purchase, maintenance, and operations departments at assigned accounts
- Identify and analyze key opportunities and threats as it relates to products, markets, and competitors
- Prepare weekly and monthly reports on customer visits, significant quotations, and overall sales activity
- Achieve the allocated sales target for assigned accounts and new business

**Requirements:**

- A degree from a reputable academic institution
- Minimum 2-3 years' sales experience related to products
- Effective communication skills and an ability to build and sustain strong customer relationships
- English proficiency is a must
- Willing to work in Dar es Salaam, Tanzania and travel to other cities

**To apply, please send your CV to careers@alkhalij.com**

115289902

## RIPOTI MAALUM

# Siri ugumu kunguni kufa, wanavyotesa familia nyingi

**Na Romana Mallya**



Rebeca Kwandu

KUNGUNI (Bedbugs) ni mdudu mwenye uwezo mkubwa wa kustahimili hatari dhidi ya maisha yake na utafiti mbalimbali unaonyesha sumu inayoweza kuua viumbe wengine, humuimarisha zaidi badala ya kumuua.

Mdudu huyo ambaye hupenda kuishi maeneo ya joto na kujificha mahali popote, kwenye godoro, fanicha, ukutani na katika pindo za nguo, kwa sasa ni miongoni wa wadudu ambao wanawatesa familia nyingi kutokana na tabia yake ya kutokufa kwa sumu kwa urahisi, hivyo kusababisha kuzaliana kwa wingi.

Uchunguzi uliofanywa maeneo tofauti jijini Dar es Salaam na kuongea na wananchi wa jiji hilo, umebaini idadi kubwa ya familia zimeathiriwa na mdudu huyo na wapo waliotumia Sh. milioni 40 kukabiliana nao bila mafanikio.

Kwa kawaida kunguni hupenda kujificha karibu na binadamu kutoka mita tatu hadi sita kwenye vitanda na maeneo ya kukaa ili iwe rahisi nyakati za usiku kunyonya damu.

**WAATHIRIKA WASIMULIA**

Mzazi wa mwanafunzi mmoja anayesoma katika Shule ya Msingi ya Atlas, Madale, ambaye hakutaka jina lake liandikwe, alisema, mtoto wake ambaye yupo bweni shuleni hapo, alianza kulalamika tangu mwaka jana kuwapo kwa kunguni bwenini.

"Mtoto wangu wakati wa likizo mwaka jana aliniambia kuwa shuleni kuna kunguni ambao wamekuwa wakiwakosesha usingizi, baada ya taarifa hiyo niliwasiliana na uongozi wa shule nao ulithibitisha na mwishoni mwa mwaka jana kabla ya shule kufungwa, kilifanyika kikao cha wazazi na uongozi wa shule," alisema.

Mzazi huyo alisema katika kikao hicho uongozi wa shule uliwahakikishia kuwa shule itakapofunguliwa mwanzoni mwa mwaka huu tatizo hilo litakuwa limekwisha, ingawa hadi sasa bado.

"Mtoto wangu alikuwa akilalamika kuwa wakilala vitandani zikizimwa taa wanang'atwa zaidi kuliko zinapowashwa, lakini matroni wao licha ya kuwapo kwa tatizo hilo, alikataa uwashaji wa taa nyakati za usiku, hivyo mwanangu anasema wamekuwa waking'atwa sana wanapoingia vitandani kuanzia saa sita usiku," alisema.

Alisema likizo ya mwezi huu uongozi wa shule hiyo ulimpigia simu na kumtaka ama walichukue godoro kwa ajili ya kwenda kulihudumia nyumbani ili kuangamiza wadudu hao au libaki shule kwa sharti kwamba liwe na kava.

"Tulilichukua godoro na tulipofika nyumbani tuliliweka nje nyakati zote na tulikuwa tukilipulizia dawa na kulianika kwenye jua hadi aliporudi shule. Hii ilikwenda sambamba na vitu vyote alivyotoka navyo shule viliishia nje tulihofia wasisambaze ndani," alisema.

Mzazi mwingine katika shule hiyo ambaye naye hakupenda jina lake liandikwe, alisema licha ya mtoto wake kuwa mwanafunzi wa kutwa, amekuwa akilalamika kuwa mara kwa mara wawapo darasani wamekuwa wakiwaona kunguni kwenye sare za shule na begi.

"Yaani sasa imekuwa kama ni mtihani akirudi nyumbani kabla ya kuingia ndani anavua kila kitu nje na anaacha na begi, tunapukuta tukiwakuta tunawaua, hofu kama mzazi ni kwamba wasijeingia ndani wakazaliana," alisema.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wakizungumza na gazeti hili walisema kuwa kuwapo kwa wadudu shuleni hapo kumewaathiri kisaikolojia kwa sababu muda ambao wanatakiwa kulala baada ya kutoka kujisomea, wanashindwa kwa sababu mara tu waingiapo vitandani, huanza kung'atwa.

Mwanafunzi wa darasa la nne ambaye (jina linahifadhiwa), alisema amekuwa akikosa raha kwa sababu hata akiwa darasani yale maumivu ya kung'atwa yamemfanya wakati wote kuhisi hivyo.

"Ninakosa raha na amani mara giza linapoingia ninawaza kunguni, maana ukiingia kitandani kulala tu taa ikizimwa unaanza kung'atwa na kujikuna, hali hii imenifanya hata nikiwa darasani mwalimu akifundisha nahisi nang'atwa tu," alisema.

Mwanafunzi mwingine wa darasa la saba shuleni hapo (jina linahifadhiwa), alisema kuwa wakati mwingine akiwa darasani anawaona wadudu hao kwenye sare ya shule. "Wakati mwingine unawakuta kwenye begi, wakati mwingine mwalimu akiwa anafundisha unashangaa mwenzako anakukung'uta nguo, ukimgeukia anakwambia ni kunguni. Binafsi usiku silali kwa raha tukitoka kujisomea usiku ukimaliza ukiwa umechoka ukiingia kitandani wanaanza, kuna wakati ilifikia tukawa hatuzimi taa angalau hatung'atwi kama ikizimwa lakini sasa matroni hataki taa iachwe bila kuzimwa," alisema.

Alisema hali hiyo ya kung'atwa kila wakati imemuathiri hata kwenye masomo kwa sababu ya kutolala vizuri usiku na kutumia muda mwingi kuhisi anang'atwa.

"Tunaomba wazazi na walimu washirikiane kuhakikisha wadudu hawa wanaisha kabisa maana bila kufanya hivyo tutafeli mitihani kwa sababu ukifika darasani badala ya kumsikiliza mwalimu unajikuta unasinzia kutokana na usiku kucha hukulala vizuri, tunaolalamika siyo sisi peke yetu tunaolala bweni hata wanaoondoka nyumbani kwa sababu tunasoma madarasa hayo hayo muda mwingi tupo pamoja wa hiyo tunawabeba mabwenini tunawaleta darasani nao wanawapeleka majumbani, hata sisi tukifunga shule tunawahamishia majumbani kwetu, ndio maana tunaomba ushirikiano wa wazazi na walimu kumaliza tatizo hili shuleni kwetu," alisema.

**MILIONI 40 ZATUMIKA KILA MWAKA**

Mmiliki wa Shule ya Msingi na Sekondari Atlas iliyopo Madale, Sylivanus Rugambwa, alikiri shule yake kuwa na tishio la kunguni kwa miaka mitatu sasa na kila mwaka wanatumia Sh. milioni 40 kukabiliana nao.

Rugambwa alisema wametumia njia mbalimbali za kukabiliana na wadudu hao bila mafanikio na likizo ya mwezi huu wameamua kila mzazi aende shuleni hapo kuchukua godoro la mtoto wake ili wakaweke foronya ya godoro (cover) ambayo ndiyo njia ya kupambana nao.

"Tumeona huu ndio mkakati wa mwisho wa kukabiliana na kunguni, maana shule nyingine za wenzetu ndiyo wametumia kukabiliana nao," alisema.

Aliongeza: "Kila mwaka tunatumia Sh. milioni 40 kukabiliana na kunguni kwa upande wa shule ya msingi na sekondari, kila nusu muhula tunatumia milioni 10, muhula tumeigawanya mara nne, hivyo kwa mwaka tunatumia Sh. milioni 40 kwa upande wa shule ya msingi na kwa upande wa shule ya sekondari."

Alisema walichoamua ni kwenye likizo ya Juni, kila mzazi anatakiwa kwenda shuleni kuchukua godoro la mtoto wake ili akaliwekee foronya ambayo inatakiwa kuwa na zipu mbili kama za hospitali.

"Tatizo la kuongezeka kwa wadudu hawa pia linasababishwa na baadhi ya wanafunzi ambao bado wanajikojolea kuwafanya kunguni kuongezeka," alisema.

Alisema ndani ya miaka mitatu, wamepuliza dawa za kuua wadudu, lakini hazijasaidia, na ndiyo maana uongozi wa shule umeamua kuja na mkakati wa magodoro yote yawekwe foronya. "Wito wangu kwa wazazi wenye watoto shule ya Atlas watekeleze kilichoelekezwa, sasa hivi wakati wa likizo wakati uongozi ukiendelea kupambana kwa kuweka mazingira mazuri kwa kufungua vitanda na maeneo yote yenye mazalia kuyatokomeza na kupaka kuta rangi," alisema.

Mkuu wa Kitendo cha Mawasiliano ya Serikali, Ofisi ya Rais Tamisemi, Rebecca Kwandu, alipoulizwa kuhusu changamoto ya wadudu hao shuleni na kama kuna mikakati ya kupulizia dawa mara kwa mara, alisema hawajapokea malalamiko kuwapo kwa kunguni shule za bweni na za kutwa.

"Ila kama kuna changamoto hiyo kwa sababu shule zina uongozi na zina wataalamu wa afya mara nyingi matatizo yanapotokea wanayamaliza huko huko au kuyafikisha kwenye mikoa yao husika, kuhusu serikali kuu hawajatufikishia," alisema.

**WAGONGA HODI MAJUMBANI**

Fatuma Abdallah, mkazi wa Tandale, aliliambia gazeti hili kuwa hafahamu wapi alipomtoa mdudu huyo, ambaye amemsababishia hasara kubwa ya vitu vyake vya ndani.

Alisema alianza kuhisi kung'atwa kila akilala ndipo alipoanza kufuatilia na kubaini kwenye chaga za kitanda kumejaa mayai mengi na kunguni waliozaliana wakubwa kwa wadogo.

"Nimeshapulizia sumu za kila aina, nikajaribu kubadilisha godoro na kununua jipya, lakini sijapata ahueni, wengine waliniambia nitoe nje vitu vyote ambavyo ni makochi, godoro, kitanda na nguo ambavyo ndivyo kupenda kujificha ili vipuliziwe dawa na kumwagia maji ya moto, lakini sijaona matokeo," alisema.

Alisema wapo waliomweleza kuwa wadudu hao wanapoona mwanga wa jua hulichukia, hivyo kila siku alilazimika kutoa vitu nje kuvianika na jioni kuvirudisha ndani bila mafanikio.

"Usiombee ukaingiwa na huyu mdudu kwanza kumwondoa ndani ni gharama na ni kazi kubwa, hawafi mapema na wanazaliana sana na sidhani kama wanakufa kwa sumu, naona wanaongezeka badala ya kupungua licha ya kuwapulizia dawa," alisema.

Agnes Moses (siyo jina lake halisi) anasimulia kuwa mmoja ya watoto wa ndugu yake walipata matatizo akawekwa moja ya mahabusu (anaitaja) jijini Dar es Salaam baada ya kutoka alifikia nyumbani kwake, Mikocheni.

Alisema baada ya kijana huyo kukaa siku chache na baadaye kuondoka, wakati wakifanya usafi kwenye chumba alichokuwa akilala, walikuta idadi kubwa ya kunguni.

"Tumeshatumia dawa za kila aina, kuna dawa ambayo tuliambiwa ndiyo kiboko kutoka Afrika Kusini, tulinunua tukatumia kuwaangamiza, lakini baada ya muda hali imerejea. Tunachofanya sasa ni kupiga dawa na kutoa magodoro na viti nje kila siku, lakini bado wapo," alisema.

**INAENDELEA KESHO**

HABARI KITAIFA

# Pinda aishauri serikali uwekezaji sekta kilimo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameiomba serikali kuipa kipaumbele cha uwekezaji sekta ya kilimo ili Watanzania waweze kujikwamua kiuchumi.

Pinda alitoa ushauri huo juzi wakati akifunga Kongamano la Fursa za Uwekezaji mkoani Dodoma.

Pinda alisema serikali inapaswa kujikumbusha ya kuwa Tanzania bado ni nchi maskini na watu wengi wapo vijijini, hivyo wakitumia fursa ya kilimo kuwekeza itasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza uchumi wa kati kupitia sekta hiyo.

Alisema idadi kubwa ya watu wanatumia kilimo kama nyenzo ya kujitoa katika umaskini, hivyo uwekezaji ukifanyika ipasavyo katika sekta hiyo, itachangia kiasi kikubwa kuwainua Watanzania kiuchumi.

"Tunaomba serikali iwekeze katika sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi, kwa sababu ina watumiaji wengi," alisema Pinda.

Pinda pia alisema wanapaswa kuwekeza katika miradi ya uvunaji maji katika mabwawa ambayo yatasaidia ongezeko la kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mbalimbali jijini Dodoma.

Alisema wataalamu wanapaswa kuwaelekeza watu mbinu za uvunaji maji ili yawasaidie baadaye.

Alibainisha kuwa wakifanya hivyo hakutakuwa na malalamiko ya uhaba wa maji wakati wawekezaji watakapoanza shughuli za uwekezaji katika maeneo mbalimbali.

"Nashauri wataalamu wawafundishe watu mbinu za uvunaji maji kwa sababu kuna mabwawa mengi ambayo maji yanatuama mwisho wa siku yanapotea bure." Alisema wakifanya hivyo kutakuwa na uhakika wa maji ya kutosheleza viwanda na shughuli za binadamu kwa sababu kuna vyanzo vingi vya maji.

"Tuna kila sababu ya kufanya uwekezaji kwa sababu ardhi ipo na wazawa wapo, ambapo kupitia kilimo wawekezaji wakiwekeza watainufaisha jamii inayozunguka eneo hilo," aliongeza.

Aliwataka wakazi wa Dodoma kuchangamkia fursa za uwekezaji zilizotangazwa katika kongamano hilo ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Pinda alisema asingependa kusikia wakazi wa Dodoma wanalalamika wakati wamesogezewa fursa kinachotakiwa wao ni kuangalia nini wanaweza kufanya na kuanza harakati za kujiwekeza.

Alipongeza serikali ya awamu ya tano kutokana na jitihada inazofanya kuhakikisha Tanzania inafika mbali kiuchumi.




Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akiwa na viongozi waandamizi wa Shirikisho la Wafanyakazi Zanzibar wakiimba wimbo wa Mshikamano Daima wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Nne wa Shirikisho hilo, uliofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil Kikwajuni jana. **PICHA: IKULU**

# DC ataka kuimarishwa ulinzi mipaka ya bahari

**Na Dege Masoli,** TANGA

MKUU wa Wilaya ya Muheza, Hijat Mwanaisha Tumbo, ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuimarisha ulinzi wa mipaka ya bahari na kudhibiti vitendo vya kihalifu kabla ya kuleta madhara.

Angalizo hilo ametoa mwishoni mwa wiki wakati akifunga Maadhimisho ya Mabaharia Duniani yaliyofanyika kitaifa jijini hapa kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Hijat Tumbo alihimiza umuhimu kwa vyombo vya usalama kuimarisha ulinzi wa mipaka majini na kudhibiti vitendo vya kihalifu kabla ya madhara na kwamba majeshi yote yanawajibu wa kuhakikisha ulinzi huo unaimarika.

Hata hivyo, alitaka ushirikiano huo kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuzingatia pia sheria za kiutendaji zinazowaongoza na lengo likiwa kuhakikisha ulinzi wa nchi unakuwapo pamoja na wananchi.

Aliagiza pia kufanyika kwa utafiti wa wavuvi wadogo nchini, kuwabaini walipo na changamoto walizonazo na namna ya kuzitatua ikiwamo kuwapatia elimu ya matumizi sahihi ya vyombo vya majini ili kuleta tija kwao na taifa.

Aidha, aliwataka wanawake kujengewa mazingira mazuri ya kujiunga na sekta ya bahari ikiwamo kusoma katika chuo cha ubaharia na kujiunga na umoja wa mabaharia wanawake nchini na hilo litawavuta kundi hilo kunufaika na fursa zilizomo. Awali, Meneja wa Usajili, Ukaguzi na Udhibiti wa Vyombo vya Majini (TASAC), Alfred Wariana, alisema kuwa shirika hilo limepiga marufuku wavuvi wanaotumia vyombo visivyodhibitishwa kuingia baharini na kwamba katazo hilo linatokana na sheria ya usalama majini yenye lengo la kukinga maafa na majanga yasiyo ya lazima.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Wakala wa Meli nchini (TASAC), ambayo pia ndiyo wafadhili wakuu wa maadhimisho hayo, Wariana alieleza nafasi ya shirika hilo inapotokea majanga baharini kuwa pamoja na mambo mengine inajukumu la kutoa elimu na kudhibiti usalama wa vyombo vya majini ikiwamo kuvifanyia ukaguzi wa ubora wake kabla ya kufanyakazi kwa mujibu wa matakwa ya sheria ya nchi.

## Wateja wa katapila wazawadiwa mafunzo

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya Mantrac, ambayo ina idhini ya kuingiza nchini mashine za uchimbaji maarufu kama caterpillar, imewazawadia wateja wake kwa mafunzo ili waweze kuelewa namna ya kuendesha mashine zao mpya.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Meneja Mauzo wa Mantrac Tanzania, Butwa Sanga, alisema mafunzo hayo ya siku tatu yaliyojulikana kama 'The Operator Challenge', yaliandaliwa mahususi kwa waendeshaji hao ili kuwaongezea ujuzi hasa wanapotumia mashine mpya zinazojulikana kama New Generation Hydraulic Excavator (NGH).

Alisema mashine hiyo mpya ya NGH inalenga kuongeza ufanisi wa hali ya juu, kupunguza gharama na kupunguza muda wa kufanya kazi, hivyo kuongeza uzalishaji.

"Makatapila haya mapya ya NHG yanapunguza muda wa kazi kwa nusu na wakati huo huo kupunguza matumizi ya mafuta kwa kati ya asilimia 25 na kuongeza ufanisi kwa hadi asilimia 45," alisema.

Mafunzo hayo ya siku tatu yalidhaminiwa na Mantrac Tanzania na kuendeshwa na mtaalamu wa mafunzo Ehab Abdelfatah Mohamed kutoka Misri.

"Tunataka waendeshaji hawa wapate ujuzi zaidi kuhusu makatapila haya mapya kwa kuwa yana teknolojia ya juu zaidi ukilinganisha na mengine ya nyuma," alisema na kuongeza kuwa uzinduzi rasmi wa katapila hiyo mpya ya NHG utafanyika Julai 17, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Mafunzo hayo pia yalienda sambamba na zoezi maalumu lijulikanalo kama 'The Operator Challenge' ambapo waliofanya vizuri zaidi walipokea zawadi na vyeti.

Mmoja wa wahudhuriaji wa mafunzo hayo, Samuel Leonard, ambaye alipokea moja ya tuzo za juu, alisema mafunzo hayo yalikuwa muhimu katika kuhakikisha wanaweza kuendesha mashine hizo mpya bila matatizo. "Tunajifunza kila siku na hasa ukizingatia makatapila haya mapya yana teknolojia ya juu sana, mafunzo haya ni muhimu sana kwetu," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars fungukeni mkiivaa Algeria leo vipaji viuzike

**LEO** timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars itashuka uwanjani kukamilisha mechi zake za hatua ya makundi ya michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 dhidi ya Algeria.

Katika fainali hizo zinazoendelea nchini Misri, tayari Stars imeshacheza mechi mbili dhidi ya Senegal na Kenya (Harambee Stars) na kupoteza zote.

Taifa Stars ambayo ipo Kundi C, ilianza kwa kupoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya Senegal kabla ya kuchapwa 3-2 na Harambee Stars.

Kwa matokeo hayo Stars leo itashuka katika Uwanja wa Al Salaam jijini Cairo, Misri kukamilisha ratiba tu na baada ya hapo kutazama njia ya kugeukia nyumbani kwa kuwa haina nafasi tena ya kusonga mbele katika michuano hiyo ambayo mwaka huu imejumuisha timu 24 kwa mara ya kwanza.

Kwa upande wake Algeria katika mechi ya leo itakuwa ikilinda heshima tu kwani tayari imeshafuzu hatua ya robo fainali kutokana na kuwa na pointi ambazo zinaweza kufikiwa tu na ama Kenya au Senegal ambazo kila moja ina alama tatu.

Hata hivyo, Senegal na Kenya zinakutana leo katika mchezo wao wa mwisho, hivyo timu itakayoibuka na ushindi ndiyo itakayoungana na Algeria kutoka Kundi C kutinga robo fainali.

Hivyo, zote Tanzania na Algeria hazina cha kupoteza katika mechi hiyo zaidi ya kutaka kulinda heshima lakini pia kujiwekea rekodi kwani moja imeshaaga na nyingine imeshafuzu.

Kwa maana hiyo, Kocha wa Taifa Stars, Mnigeria Emmanuel Amunike hana budi kuandaa mfumo utakaokuwa rafiki kwa kuwawezesha wachezaji watakaopangwa kucheza kwa uhuru zaidi ili kuweza kuonyesha vipaji vyao.

Tunatambua katika michuano hiyo kuna mawakala wengi wapo nchini Misri na wengine wakifuatilia kwa njia ya luninga ili kubaini vipaji kwa ajili ya klabu zao ndani ya Afrika na nje hususan barani Ulaya.

Kutokana na hilo, kama kikosi cha Stars kitashuka dimbani kikiwa kinatumia mfumo wa kujilinda zaidi kama kilivyocheza dhidi ya Senegal, ni wazi itakuwa ni vigumu kwa mawakala kubaini uwezo wa mchezaji mmoja mmoja.

Tunatarajia kuona Stars ikifunguka kwa kucheza soka la kushambulia zaidi kwani kwa kutumia mfumo huo uwezo na kipaji cha mchezaji mmoja mmoja utaonekana kirahisi na hivyo kutangaza soko lao.

Tunatambua kushindwa kuibuka na pointi hata moja katika michuano hiyo hadi sasa, kumechangiwa na wachezaji wa Stars kukosa uzoefu wa kucheza mechi kubwa, huku wakikutana na wapinzani wao walioiva kufuatia kuzitumikia klabu kubwa ndani na nje ya Bara la Afrika.

Hivyo kupitia fainali hizi za Afcon, Nipashe tunatamani kuona hatutoki patupu, kwa kukosa pointi na kisha kushindwa hata kufanikiwa kuuza wachezaji angalau wawili ?

Kwa kuwa tumeshapoteza matumaini ya kusonga mbele, mechi ya leo tunataka wachezaji waitumie kwa kuuza vipaji vyao zaidi na hilo litawezekana tu kama Amunike atatumia mfumo rafiki kwao kama 4-3-3 ambao utawapa nafasi ya kufunguka na kushambulia zaidi.

Pamoja na kutamani wachezaji kuutumia mchezo huo kutangaza vipaji vyao, lakini pia Stars inapaswa kulinda heshima angalau kuondoka na pointi zote tatu au hata moja kuliko kukubali kumaliza michuano hiyo kwa aibu bila hata alama moja.

Kwa ujumla, pamoja na kutofanya vizuri katika michuano hiyo, Nipashe tunawapongeza wachezaji wa Stars kwa hatua na uwezo walioonyesha na tunawataka kuendelea kujituma zaidi ili michuano ijayo waweze kufika mbali zaidi. Kila la heri Stars dhidi ya Algeria leo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Viongozi wa klabu jipangeni sasa kubadili kanuni Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

**NILIKUWA** nashangazwa na baadhi ya viongozi wa klabu mbalimbali kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika kulalamika baadhi ya kanuni za ligi. Mfano kuna kanuni ya mapato ya mlangoni ambapo timu mwenyeji inachukua mapato yote.

Nilikuwa nikishangaa baadhi ya viongozi wakipinga hilo wakati ni kanuni iliyopitishwa na wao wenyewe.

Kanuni za ligi hupitishwa na viongozi wa klabu zenyewe zinazoshiriki ligi na awali Shirikisho la Soka nchini (TFF), linachofanya ni kuwapata viongozi hao kuleta mapendekezo mapya ya kanuni, lakini pia marekebisho kama kuna kanuni ambazo wanaona hazifai na zimepitwa na wakati.

Kanuni za ligi hutolewa, kurekebishwa na kupitishwa kila msimu, hivyo kabla ya msimu kuanza TFF itatangaza na kuwataka viongozi kupeleka mapendekezo ya kanuni ambazo zinapitiwa na mwisho wa siku zinapitishwa na wao wenyewe.

Nilichogundua ni kwamba viongozi wengi wa ligi wao wako bize kwenye kusajili wachezaji na mambo mengine ya klabu na kusahau kabisa kupeleka mapendelezo, au marekebisho ili TFF wayaingize kwenye kanuni mpya na mwisho wa siku kupigiwa kura ya kupitishwa au la.

Wengi hawajishughulishi na hilo na wanakuja kuzishtukia zikiwa zinatumika, wanaanza kushangaa.

Siku si nyingi TFF itatangaza juu ya marekebisho ya kanuni mpya kuelekea msimu ujao, hii sasa iwe fursa ya viongozi kupeleka mapendekezo yao. Kama hawataki ule mfumo uliopita wa timu kuchukua mapato yote na badala yake wagawane, ndiyo muda wa kupeleka mapendekezo ya marekebisho ya kanuni.

Si hilo tu kuna vitu vingi kama vile timu zikifungana pointi nini kiangaliwe, uwiano wa mabao ya kufunga na kufungwa au timu hizo zilipokutana zenyewe kwa zenyewe na vingine vingi.

> **Si hilo tu kuna vitu vingi kama vile timu zikifungana pointi nini kiangaliwe, uwiano wa mabao ya kufunga na kufungwa au timu hizo zilipokutana zenyewe kwa zenyewe na vingine vingi. Niliona viongozi wengi wakilalamika kuwa wanasafiri mikoani, lakini hakuna chochote wanachoambulia kwani mapato yote yanakwenda kwa mwenyeji.**

Niliona viongozi wengi wakilalamika kuwa wanasafiri mikoani, lakini hakuna chochote wanachoambulia kwani mapato yote yanakwenda kwa mwenyeji.

Nadhani kanuni hii ilitungwa msimu uliopita na inavyoonekana baadhi ya viongozi wa klabu za mikoani ndiyo waliipendekeza na kuipitisha kwa sababu wao viwanja vyao huingiza mashabiki wengi zinapocheza na klabu kubwa za Simba na Yanga.

Wakaona watafaidika sana na mapato ya mlangoni, wakati huo viongozi wa Simba na Yanga walikuwa kama vile wamelala na kujiamini, walipozinduka tayari kanuni imepitishwa.

Cha ajabu ni kweli klabu za mikoani zinapata mapato mengi ya mlangoni timu za Simba na Yanga zinapokwenda huko, lakini na wao wamekuja kukiona cha moto wanaposafiri mikoani kucheza na klabu nyingine ndogo.

Huko wanasafiri kwa umbali mrefu, lakini hawapati kitu, timu inazunguka viwanja vitatu bila kuambulia senti tano na kwa hali hiyo hata ile ya kuchukua mapato yote inapocheza nyumbani dhidi ya klabu kubwa ikaanza kuwatumbukia nyongo.

Wakaanza kuona ni afadhali mapato ya kugawana, hata kama wakigawana nusu kwa nusu na Simba na Yanga, lakini na wao wanapokwenda huko kwa wenzao wapate hata pesa ya maji ya kunywa ya wachezaji wao, hivyo wakaanza kulalamika.

Sasa waache kulalamika na badala yake wajipange kubadilisha kipengele cha kanuni hiyo ili kurudisha kama ilivyokuwa zamani, mapato ya nusu kwa nusu mwenyeji na mgeni.

# Barua ya wazi kwa Rais John Magufuli

*KWA heshima na taadhima, ninakuandikia barua hii ili uweze kunisaidia nipate haki yangu ambayo kwa zaidi ya miaka 15, nimeshindwa kuipata, hata baada ya kupitia katika ngazi mbalimbali za mamlaka.*

*Ninakuandikia ili unisaidie niweze kuipata haki yangu niliyopewa kupitia Hukumu au Amri ya Mahakama ya Wilaya ya Korogwe Criminal Appeal No: 9/03 PAULO P. BALIGILA DHIDI YA HUSSEIN ALLY.*

*Hadi sasa utekelezaji wa hukumu hiyo ya mwaka 2003 umeshindikana hata baada ya kupitia ngazi zifuatazo nikiomba msaada ili nisaidie.*

- *Mahakama ya Wilaya Korogwe.*
- *Mahakama Kuu Dar es Salaam.*
- *Mahakama ya Rufani Dar es Salaam.*
- *Mwanasheria Mkuu wa Serikali.*
- *Katibu wa Jaji Mkuu.*
- *Naibu katibu wa Jaji Mkuu.*
- *Kamishna wa Maadili.*
- *Katibu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.*
- *Katibu Tawala Mkoa wa Tanga.*
- *Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.*
- *Katibu Tawala Wilaya ya Korogwe.*
- *Taasisi ya kuzuia na Kupambana na Rushwa (P.C.C.B).*
- *Katibu Kiongozi Ikulu.*
- *Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.*

*Mheshimiwa Rais, ngazi zote hizo nimepitia kwa kufika mwenyewe, kuandika barua na zikatoa maelekezo mbalimbali kwa mamlaka zilizo chini yao ili waweze kusaidia utekelezaji wa hukumu hiyo ya Mahakama ya Wilaya ya Korogwe lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika.*

*Mbaya zaidi niliyekuwa ninamlalamikia yupo, anaendelea na shughuli zake kama kawaida huku mimi niliyeathirika nikiwa sina la kufanya.*

*Na hiyo ni pamoja na ukweli kwamba hata maagizo ya ngazi mbalimbali yaliyotolewa kuhakikisha ninapata haki yangu yameendelea kupuuzwa hadi sasa.*

*Ninaomba basi Mheshimiwa Rais Magufuli, mtetezi wa wanyonge unisaidie kwa hili ili nipate haki yangu.*

*Natanguliza shukrani.*

**Ndimi mwananchi wako,**
**Paulo P. Baligila,**
**S.L.P 154, Korogwe,**
**Simu Namba 0657-453523, 0655-324580**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Kwa ushauri huu wa Rostam, hakika Yanga itazidi kudidimia




**Na Adam Fungamwango**

NIMEMSIKIA mfanyabiashara maarufu nchini Rostam Aziz ambaye aliingia kwenye anga la mambo ya soka hivi karibuni, baada ya kutoa ahadi ya kuichangia Klabu ya Yanga kiasi cha Sh. milioni 200 kwenye hafla iliyoitwa 'Kubwa Kuliko'.

Nadhani baada ya wanachama wengi na mashabiki wa Yanga kuwa na uhakika kuwa Rostam kumbe ni mwenzao, waliangalia kama kuna uwezekano wa yeye kuwekeza kwenye klabu hiyo au kuifadhili ili kujikwamua na matatizo ya kifedha ambayo yamekuwa yakiikumba kwa sasa.

Siku chache baadaye alizungumza na waandishi nyumbani kwake na kusema kuwa Klabu ya Yanga haihitaji kumilikiwa au kufadhiliwa na mtu mmoja, hivyo haungi mkono Yanga kuwa kwenye mfumo huo.

Akasema iwapo klabu hiyo itamilikiwa au kutegemea ufadhili itapoteza maana na hadhi ya klabu hiyo.

"Kwa mtazamo wangu, Yanga haitakiwi kumilikiwa na mtu binafsi au kutegemea ufadhili kwa sababu ni klabu yenye wanachama wengi." alisema na kuongeza.

"Yanga inatakiwa kumilikiwa na wanachama wake wote. Kunapokuwa na ufadhili au umilikiwa na mtu binafsi, unawanyima au kubinywa wale walio wengi."

Hayo ni baadhi ya maneno kutoka kwa bilionea huyo ambaye wengi walidhani kuwa anaweza kuamua kuwekeza kwenye Klabu ya Yanga kama ilivyo kwa Mohamed "MO" Dewji alivyofanya kwenye Klabu ya Simba. Huo ni mtazamano wake. Lakini kwa maneno hayo ni kwamba ndoto za Yanga kumpata bilionea huyo kuwekeza au kufadhili kwenye klabu hiyo zimeyeyuka.

Atakachokuwa akifanya ni kuchangia kama alivyochangia pesa hizo na kama wanavyochangia wanachama na mashabiki wengine.

Pamoja na hayo yote hapa kuna hoja au maswali kadhaa ya kujiuliza. Hivi Yanga inaweza kuendelea na kupiga hatua kwa kuchangishana pesa kwenye hafla milele?

Mimi nadhani kungekuwa na mfumo ambao ungekuwa unasababisha wanachama na mashabiki kuchangia bila kuitisha hafla za mara kwa mara za uchangishaji, au kupitisha bakuli viwanjani wakati timu inacheza.

Nataka nimkumbushe Rostam kuwa timu hizi za Simba na Yanga zimekuwa zikitegemea mfumo wa wanachama kujiendesha wenyewe kwa miaka zaidi ya 80 sasa, na hazina hata viwanja vya mazoezi.

Hivi sasa wadau wa soka na wachambuzi wanazishangaa klabu hizi kongwe kutokuwa na viwanja vyao wakati timu kama Azam na Gwambina FC ya Mwanza, zina viwanja.

Azam inamilikiwa na mtu binafsi, huku Gwambina ikiwa na mwekezaji na ndiyo maana zina viwanja vyao. Kama zingekuwa zinategemea michango ya wanachama kama Simba na Yanga zisingekuwa hivyo.

Zamani soka lilikuwa la ridhaa hasa nchi za Ujamaa, wachezaji walikuwa wakicheza kwa kugawana posho tu. Hapa Tanzania wachezaji walisajiliwa kwa fenicha za ndani, pia ahadi ya kutafutiwa kazi kwenye kampuni yoyote ile.

Kwa sasa mambo yamebadilika, mfumo wa kibepari umetawala, soka kwa sasa ni ajira ya moja kwa moja na wachezaji hununuliwa kwa pesa nyingi si hapa Tanzania tu ni duniani kote.

Kwa sasa Afrika mchezaji mmoja mwenye kiwango cha hali ya juu cha kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika ananunuliwa mpaka bilioni mbili, kama klabu itakuwa inaendeshwa na pesa za michango inaweza kweli kupambana na timu kama Al Ahly, Esperance, AS Vita na TP Mazembe kwenye soka la usajili?

Ndiyo maana kwa sasa klabu nyingi zimetafuta wawekezaji, na zingine zinatafuta kwa ajili ya kufanya mabadiliko ya uendeshaji kwenye klabu zao mbalimbali duniani. Huko Ulaya tunaona Wazungu wakiwakaribisha wawekezaji kutoka Bara la Asia ili kununua hisa kwenye klabu zao kwa ajili ya kuendana na dunia ya soka ya sasa inavyotaka.

Na hata zile klabu za wanachama ambazo ndizo zinatolewa mifano, zenyewe zimeweka mifumo thabiti ambayo wanachama na mashabiki wao wanapitia kama kununua jezi, tiketi za msimu, kutembelea makumbusho ya klabu, redio, televisheni na vitu mbalimbali ambavyo vinafanya kujipatia pesa za kuendesha klabu ambavyo huku havipo.

Nina wasiwasi kama Yanga ikiendelea kutegemea mashabiki wachange pesa kujiendesha, inaweza kucheza Ligi Kuu na kuzifunga Ndanda, Biashara na KMC, lakini siyo kufanya vema kwenye Ligi ya Mabingwa na kupata maendeleo mengine kama klabu.

Kama wanachama wa klabu za Simba na Yanga wameshindwa kwa zaidi ya miaka 80 sasa, sidhani kama wanaweza kwa miaka hii michache ijayo, kama hazijapata wawekezaji.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**TAARIFA KWA MAFUNDI SIMU ZA MKONONI NA VIFAA VYA KIELEKTRONIKI**

Kumekuwa na mwitikio mzuri sana kwa Mafundi wa simu za Kiganjani na vifaa vya kielekroniki katika kupata mafunzo maalum ya kitaalamu tangu mafunzo hayo yaanze kutolewa kuanzia tarehe 23/07/2018 hadi sasa. Ni dhahiri kuna uhitaji mkubwa wa kuwa na Mafundi wa simu za mkononi waliofundishwa vema na wenye kuzingatia taratibu na sheria katika kazi zao, ili kuwa na uhakika wa mawasiliano salama kwa watumiaji wa vifaa hivyo.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania **(TCRA)** kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam **(DIT)** na Vyuo vya Ufundi Stadi **(VETA)** wamekuwa wakitoa mafunzo kwa Mafundi simu hao ambapo wanafunzi 144 wamehitimu mafunzo hayo na kati yao wanafunzi 110 wamefanikiwa kupata vyeti vya usajili kutoka **TCRA.**

Mafunzo haya yataendelea kutolewa tena kikanda kama ifuatavyo; **Kanda ya Ziwa** (Mwanza, Simiyu, Mara, Shinyanga, Geita na Kagera), **Kanda ya Kaskazini** (Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga), **Kanda ya Kati** (Dodoma, Tabora, Kigoma na Singida), **Kanda ya Mashariki** (Dar es Salaam, Mtwara, Pwani na Morogoro), **Kanda ya Nyanda za Juu Kusini** (Mbeya, Songwe, Njombe, Ruvuma, Iringa, Rukwa na Katavi) na **Ofisi ya Zanzibar** (Unguja Mjini Magharibi, Unguja Kaskazini, Unguja Kusini, Pemba Kaskazini, Pemba Kusini).

Aidha, tumeshuhudia pia mwitikio mzuri wa Mafundi simu na vifaa vya kielektroniki katika kujisajili na kupata cheti cha **TCRA** ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na Mafundi simu wenye ujuzi, **TCRA** inapenda kuwatangazia kuwa kuanzia tarehe **1 Julai 2020** Mafundi wote wa simu za Kiganjani na vifaa vya kielekroniki **ambao hawajasajiliwa na TCRA** hawataruhusiwa kutoa huduma ya kutengeneza simu za Kiganjani na vifaa vya kielekroniki. Sharti kubwa la kupata usajili wa **TCRA** ni kuwa wamepitia mafunzo ya awali ya ufundi wa simu za kiganjani na vifaa vya kielekroniki yanayotolewa na **DIT** au **VETA.**

Imetolewa na:

MKURUGENZI MKUU
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)**

# Kipunguni wacharuka, wamtaka Prof. Mbarawa

**INATOKA UK. 3**

tathmini.

"Ni kero kwa wananchi bora waambiwe ukweli maana jambo hili limeshughulikiwa na mawaziri karibu wanne lakini hadi sasa hakuna suluhisho, mbunge wa upande wake amekuwa akijitahidi kukumbusha jambo hili lishughulikiwe," alisema.

"Wakati tathmini inafanywa watu walikuwa vijana wamepata watoto, wanawajukuu wanatamani kuongeza majengo ya nyumba zao lakini wanazuiwa, wanakosa maendeleo," alisema.

Mmoja wa wakazi hao, Hilda Kaijage, alisema ucheleweshwaji wa malipo ya fidia hiyo umewakwamisha kimaendeleo kwa kuwa imechukua miaka mingi bila kutolewa, pia wamekuwa wakiishi kama wapo kizuizini.

Hilda aliiambia Nipashe kuwa leseni za makazi ni muhimu kwa kuwa inaweza kutumika kama dhamana ya mikopo kutoka kwenye benki mbalimbali.

Alisema fedha za mikopo hiyo wangeweza kutumia kukuza mitaji ya biashara au kufanya mambo mengine ya maendeleo.

Mustafa Ahmed alisema anakumbuka wakati anajenga nyumba yake yenye vyumba sita saruji ilikuwa inauzwa shilingi 3,800 ikichangazwa na gharama za nauli ilikuwa 200 kwa mfuko mmoja.

"Tangu tulipozuiwa kuendeleza ujenzi ni muda mrefu ukiangalia nyumba nyingi zimepoteza mvuto, tunaishi kwa hisia tutahamishwa kesho kiwanja nimepewa muda mrefu, lakini nitajenga na nini kule Majohe Kivule," alisema Ahmed.

Mbunge Kamoli alieleza kuwa jambo hilo la fidia limekuwa likimkosesha amani kwa kuwa anatambua ni haki ya wananchi hao kulipwa ili wajiendeleze kimaisha katika maeneo waliyopewa.

Gazeti hili awali liliwasiliana na Katibu wa Waziri, Martin Ngeleja ili kujua kuhusu nia ya kwenda kuzungumza na wakazi hao alisema hakujipanga kwenda kwenye mkutano huo.

Awali mwaka 2017 aliyekuwa Naibu Waziri, Edwin Ngonyani, akijibu swali la Mbunge wa Segerea Bonna alisema serikali imefanya tathmini na katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilitenga Sh. bilioni 30 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wakazi hao.




Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari wakati kampuni ya Tigo ilipotangaza udhamini kwenye Maonyesha ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano wa Tan-Trade, Theresia Chilambo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TPA kutoa mrabaha wa bil. 200/- serikalini

**INATOKA UK. 3**

nchini ambazo zinahudumia meli za shehena ya mizigo na abiria.

Alisema wamekuwa wakitekeleza miradi mikakati ya taifa na miradi ya TPA ambayo kwa pamoja inasaidia kuboresha utendaji kazi wa bandari na kuongeza mapato.

Alieleza kuwa, upande wa Bandari ya Dar es Salaam pekee wanatekeleza miradi mikakati ambayo mmoja unagharimu Sh. bilioni 377.

Alisema gharama za miradi yote inafika Dola za Marekani bilioni 431 na kwamba bajeti ya TPA inatumia trilioni moja ya kuendeleza mradi mmoja katika bandari hiyo.

Alitoa mfano miradi mikakati ya kitaifa ni ile ya ununuzi wa scana au midaki uliofanywa kwa agizo la Rais John Magufuli mwaka 2016 na ujenzi wa flowmeter ambayo inajengwa na ujenzi wake umefika zaidi ya asilimia 45.

Alisema pia ujenzi wa kuongeza kina katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara unaendelea katika kuhakikisha bandari hizo zinakuwa na kina kirefu cha kupokea meli kubwa na kuongeza mapato.

Pia, alieleza miradi ya TPA ni ile ya ujenzi wa gati za kisasa, upanuzi wa bandari zote nchini, ujenzi wa ofisi na maghala ya kuhifadhia mizigo ili kufungua milango ya kibiashara na nchi za jirani.

Alisema miradi hiyo inatumia zaidi ya Sh. bilioni 500 ya fedha za ndani na hufika Sh. bilioni 600 kama wakipata na fedha za nje na asilimia 30 ya fedha hizo wanalipa mrabaha serikalini.

HABARI KITAIFA

# Benki zatakiwa kukopesha wawekezaji miradi mikubwa

**NA Beatrice Philemon**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, ameiomba Benki ya Standard Chartered na taasisi nyingine za kibenki kuangalia jinsi gani wanaweza kukopesha fedha katika miradi mikubwa kusaidia Watanzania kushiriki katika ujenzi wa viwanda.

Kairuki alisema hayo katika halfa ya chakula cha usiku iliyoandaliwa na benki hiyo kumkaribisha Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo ukanda wa Afrika na Mashariki ya Kati, Sunil Kaushal.

Kaushal alikuwa nchini kwa ziara ya siku mbili kukutana na wateja wao wakiwamo wawekezaji wazawa na wa nje ili kuona changamoto zinazowakabili katika miradi yao ya uwekezaji, nini wanahitaji ili iweze kutatua changamoto hizo.

"Standard Chartered ni benki ya kimataifa inayotoa mitaji na kukopesha wazawa ili waweze kupanua biashara zao, kama hakuna fedha, mitaji, hakuna uwekezaji," alisema na kuongeza:

"Sisi kama serikali tutaendelea kuhimiza benki hii na zingine waone ni jinsi gani wanaweza kukopesha miradi ya umeme, barabara na tutaendelea kuwahimiza waone pia maeneo mengine ya miradi ili waone watatusaidiaje."

Alisema lengo kuu la kupata mitaji na mikopo ni kusaidia Watanzania kushiriki katika ujenzi wa viwanda, kukuza sekta binafsi na uwekezaji bora wenye viwango endelevu.

Kwa upande wake Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Standard Chartered Tanzania, Sanjay Rughani, alisema kuwa Kaushal alikuja nchini kuangalia changamoto zinazowakabili wateja wake na kuangalia miradi ipi benki hiyo inaweza kusaidia serikali ya Tanzania ili iweze kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Naibu Gavana, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibese, aliishukuru benki ya Standard Chartered kwa kuandaa chakula cha pamoja na wateja wao ili kubaini changamoto zinazowakabili pamoja na wawekezaji.

Alisema hali ya uchumi wa Tanzania imeimarika kwa asilimia 7 na mfumuko wa bei umepungua kwa asilimia tano na bei ya kubadilisha fedha pia imeimarika na kusaidia wafanyabiashara wanaoingiza na kupeleka bidhaa nje. Alisema pia BoT itafanya ukaguzi maalumu katika benki kwa wafanyakazi mmoja mmoja ili kubaini ambao siyo waaminifu katika utoaji wa mikopo na itawaondoa.




Wafanyakazi wa Airtel Tanzania wakishiriki zoezi la kuchangia damu kwa hiari kwa lengo la kuokoa maisha kwa wahitaji wa damu kupitia banki ya damu salama. Anayetoa damu ni ofisa kutoka Mpango wa Taifa wa Damu Salama Rosemary Bulemo. Zoezi la uchangiaji damu kwa hiari lilifanyika makao makuu ya Airtel Morocco jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mgawanyo majukumu watakiwa malezi mtoto

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZWA kuwa suala la ustawi wa mtoto ni jukumu la jamii, hivyo kunatakiwa kuwapo na mgawanyo wa majukumu.

Hayo yalisemwa na Fadhili Nandonde, Ofisa kutoka Bright Jamii, katika semina ya jinsia na maendeleo (GDSS) iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP Mtandao).

Fadhili alisema kuwa shirika lao ambalo sio la kiserikali pia linafanyia kazi masuala ya wanawake katika kuwawezesha kiuchumi.

Fadhili alitoa mada kwa wadau wanaoshiriki GDSS ambayo ilizungumzia kuwa nafasi ya baba na mama katika malezi ya mtoto.

Mmoja wa washiriki, Juma Hasani, alisema yeye anachojua baba kazi yake ni kulipa ada, kuhakikisha chakula kipo na kuhakikisha kwamba nyumba inaamani.

Alisema kazi ya mama ni kupika, kuhakikisha chakula kipo na kuwa karibu na watoto.

Hawa Jamali kwa upande wake alisema kuwa mama majukumu yake ni kubeba mimba, kupika, kuhakikisha watoto wanakula na kuishi nao katika malezi yaliyo sawa.

Fadhili alisema mfumo dume bado upo baada ya kusikiliza maoni ya washiriki na kusema kuwa malezi ya watoto ni jukumu la jamii.

Alisema mgawanyo wa majukumu utasaidia kuwapo na malezi ya mtoto, lakini sio majukumu yote kupewa mtu mmoja.

Alisema kinachotakiwa ni kuondoa mfumo dume na ukatili ili kuwezesha kuwapo na nafasi ya baba na mama katika malezi ya mtoto.

# TADB yahimiza wakulima kuchangamkia mikopo

**Na Mwandishi Wetu,** KATAVI

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imewataka wakulima na wadau mbalimbali katika sekta hiyo na mifugo hapa nchini kuchangamkia fursa ya mikopo inayodhaminiwa na benki hiyo kupitia benki za biashara kuongeza uzalishaji.

Akizungumza katika kikao cha wadau wa kilimo mkoani Katavi hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema wakulima wanapaswa kuchangamkia fursa za mikopo katika benki hizo ambazo ni mkombozi na pia zitasaidia kuchagiza ukuaji wa sekta ya viwanda.

"Benki ipo tayari kutoa mikopo kwa haraka katika miradi mbalimbali itakayosaidia wakulima wadogo kukua, hivyo nawaomba wadau waandae maandiko na kuyawasilisha TADB kwa ajili ya utekelezaji wa haraka," alisema Justine na kuzitaja benki ambazo TADB inadhamini mikopo kwa wakulima ni pamoja na NMB,CRDB na TPB.

Aidha, katika kikao hicho na wadau wa kilimo, Justine mbali ya kutembelea maeneo yenye viwanda alipata kusikia changamoto ambazo wakulima wanakabiliana nazo ili ziweze kupatiwa ufumbuzi na kuongeza tija katika kilimo.

Kuhusu kufufua kiwanda cha alizeti kilichopo Wilaya ya Tanganyika mkoani humo, alisema benki itakaa na wadau mbalimbali kutengeneza muundo wa ukopeshaji na kuainisha mkopaji ambaye atakuwa tayari kuwekeza katika kiwanda hicho.

"Mkoa wa Katavi una fursa nyingi za uwekezaji katika viwanda vya nyama, maziwa kutokana na uwepo wa ng'ombe pia kuendeleza kiwanda cha kusindika asali ambayo hupatikana kwa wingi mkoani humu," alisema.

Alisema Katavi ina mazao ya kipaumbele kama vile tumbaku, pamba, korosho, kahawa na chikichi, hivyo uwekezaji katika kukuza uzalishaji katika mazao hayo na uanzishwaji wa viwanda kutainua uchumi katika mkoa na kufanikisha azma ya serkali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025 kufikiwa kwa vitendo.

"TADB ipo kwa ajili ya Watanzania wote hivyo ni wajibu wa kila mtu katika eneo lake kuandaa andiko la mradi na kuwasirishwa kwetu kwa ajili ya hatua mbalimbali ili kutoa mikopo kwa jamii itakayosaidia kuendeleza sekta ya kilimo na mifuko nchini," alisema.

Alifafanua kuwa benki hiyo inawataalamu wakutosha ambao wapo tayari kutoa elimu ya namna ya kuandaa maandiko ya mradi kitaalumu ili yatakapo wasilishwa kusiwe na kipingamizi katika andiko na kupelekea mkopo kutoka kwa haraka.

Mkuu wa Mkoa Katavi, Juma Homera, mbali ya kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa TADB kwa kuitikia mwaliko wa kutembelea mkoa huo na kujionea fursa zilizopo, aliainisha changamoto zilizopo mkoani hapo ikiwamo upungufu wa viwanda vya kusindika mazao mbalimbali ili kuongeza thamani.

"Kazi kubwa iliyopo ni kuunganisha wadau kutoka serikali na sekta binafsi na wote ndani ya mkoa ili kuweka mikakati ya pamoja kutatua changamoto mbalimbali zilizopo ili kuleta tija katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi," alisema Homera.

# Ukaguzi wa mizani sasa watua Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKALA wa Vipimo nchini (WMA) Mkoa wa Shinyanga unaendelea na utoaji wa elimu ya vipimo sahihi kwa wakulima wa pamba katika Wilaya ya Kahama kwa lengo la kuwawezesha wakulima kutambua mizani sahihi iliyo hakikiwa na WMA.

Mizani iliyohakikiwa na WMA huwekewa stika pamoja na lakiri kwenye njia za kuingilia kwenye mizani ili kuzuia isichezewe na wafanyabiashara wenye lengo la kujiongezea faida zaidi.

Kabla ya kuanza kwa msimu wa ununuzi wa pamba, WMA Mkoa wa Shinyanga ilifanya uhakiki wa mizani yote itakayotumika katika vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) 195 katika Halmashauri za Ushetu, Kahama Mji, Msalala, Kishapu, Shinyanga DC pamoja na Manispaa ili kuhakikisha wakulima wanauza pamba kwa kutumia vipimo vilivyo sahihi.

Meneja wa WMA Mkoa wa Shinyanga, Elias Nyanda, alisema kata 20 za Wilaya ya Kahama zimepatiwa elimu hiyo sambamba na ukaguzi wa mizani katika vituo vinavyotumiwa kuuzia pamba.

"Lengo la WMA ni kujiridhisha kama mizani hizo zinafanya kazi kwa usahihi ili kumsaidia mkulima aweze kupata fedha kulingana na thamani ya pamba anayouza.

"Katika zoezi hilo, wakulima wameelimishwa wawe makini wanapokwenda kuuza pamba kwa kuhakikisha mizani inasoma sifuri kabla ya kuanza upimaji kwa kutumia mizani ya digitali.

"Aidha, baada ya kupima furushi la pamba mizani hiyo inatakiwa kurudi kusoma sifuri, na wahakikishe mizani hiyo haisomi hasi (-) baada ya kutoa mzigo, ikitokea hivyo karani anayesimamia mizani aizime na kuiwasha tena mizani kisha upimaji uendelee.

Mmoja wa wakulima wa pamba, Joseph Nyamwanga aliipongeza WMA kwa elimu wanayowapatia kwani imewasaidia kupunguza changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa upimaji.

"Kupitia elimu hii tuta endelea kuwa makini ili tuendelee kupata haki tunayostahili kila tunapokwenda kuuza pamba katika AMCOS zetu," alisema mkulima huyo.

Aidha Meneja huyo wa WMA aliwakumbusha wadau wote wa pamba mkoani humo kuwa Sheria ya Vipimo Sura Na. 340 na mapitio yake ya mwaka 2002 imeboreshwa na imekuwa kali tofauti na miaka ya nyuma. Alisema endapo mnunuzi wa pamba atabainika kuchezea vipimo akikamatwa na kukiri kosa atatozwa faini kati ya Sh. 100,000 mpaka milioni 20 kutegemea idadi ya makosa aliyotenda.

"Na endapo mtuhumiwa atakataa na kufikishwa mahakamani kwa kosa la kwanza atatozwa faini isiyopungua Sh. 300,000 na isiyozidi Sh. milioni 50 au kifungo kisichozidi miaka miwili (2) au vyote kwa pamoja.

"Vilevile, endapo mtuhumiwa atakamatwa na kosa kwa mara ya pili na kuendelea na akipelekwa mahakamani akikutwa na hatia adhabu yake ni faini isiyopungua Sh. 500,000 na isiyozidi milioni 100 au kifungo kisichozidi miaka mitano (5) au vyote kwa pamoja," alisisitiza Nyanda.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Idd Badru, akizungumza wakati wa mkutano na waandishi wa habari katika banda la benki hiyo lililopo kwenye Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayoendelea katika Viwanja vya JK Nyerere Barabara ya Kilwa. Kulia ni Meneja wa Benki ya NMB tawi la Temeke, Kidawa Masoud na kushoto ni Meneja Uhusiano wa Benki hiyo, Vicent Mnyanyika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu majengo mengi kujengwa holela zatajwa

**Na Yasmine,** PROTACE

ASILIMIA 90 ya nyumba zilizojengwa nchini, hazikujengwa kwa mpangilio unaofaa kutokana na ukosefu wa wataalamu wa wabunifu majenzi na wakadiliaji majenzi.

Hayo yalisemwa na Mbaraka Igangura, kutoka Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiliaji Majenzi, katika mkutano wa mafunzo kwa waandishi wa habari juu ya shughuli zinazofanywa na bodi hiyo.

Alisema inatakiwa jamii iwashirikishe ili waweze kujenga maeneo yanayofaa na kuwaelewesha wasijenge katika maeneo yasiyofaa.

"Tunaona hata mvua zinaponyesha, madhara makubwa yanatokea kama maji kujaa, mawasiliano kukosekana kwenda maeneo mengine kutokana na maji kujaa, hiyo inatokana na ujenzi holela ambao haukufuata taratibu za wataalamu wa wabunifu majengo na wakadiliaji majenzi," alisema.

Pia alisema jamii ifuate wataalamu ambao wanatoa ramani kwa ajili ya ujenzi.

Alisema kuna watu wanauza ramani za nyumba kiholela ambapo changamoto inakuja pale wauza ramani kutofika katika ujenzi na kusababisha nyumba kujengwa chini ya kiwango.

Alisema mtu anayejenga nyumba kwa kufuata taratibu kutoka kwa wabunifu majengo na wakadiliaji majenzi, nyumba itajengwa kwa gharama nafuu, lakini wasiofuata utaratibu wanajikuta wanajenga nyumba kwa gharama kubwa.

"Mtu akifuata utararibu na akatumia wataalamu kujenga nyumba atajenga kwa gharama ndogo kutokana na kuwatumia wataalamu wanaokubalika.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Dk. Ludigija Bulamile, alisema kuwa bodi hiyo ni taasisi ya serikali iliyoanzishwa kusimamia sheria ya usajili wa wabunifu majengo na wakadiliaji majenzi namba 4 ya mwaka 2010 na iko chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Aliongeza kuwa mpaka sasa bodi imesajili jumla ya wataalamu 1596 na kampuni za kitaalamu 372. "Wakati bodi ilipoanza shughuli zake mwaka 1998 kulikuwa na wataalamu 188 na kampuni 53," alisema. Aliongeza kuwa ongezeko hilo ni kubwa, lakini kiuhalisia bado mahitaji ya wataalamu nchini ni wachache ikilinganishwa na idadi ya Watanzania wanaohitaji huduma zao.

Alisema katika kuhamasisha usajili wa wataalamu na kampuni, bodi imepunguza muda wa usajili toka miezi mitatu hadi muda usiozidi wiki mbili kwa wale ambao maombi yamekamilika.

# Mradi waokoa watoto kiafya

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

AFYA za watoto waliobainika kuwa na hali mbaya zaidi kiafya zinaendelea kuimarika katika maeneo mbalimbali mkoani Kagera, baada ya wananchi kufundishwa namna ya kuandaa chakula dawa kwa ajili ya watoto hao.

Hali iyo imewezekana kupitia mradi wa serikali wa mtoto mwerevu, unaoratibiwa na Shirika la IMA World Health unaofadhiliwa na Serikali ya Uingereza.

Wakitoa ushuhuda katika Tamasha la Mtoto Mwerevu lililoandaliwa na wananchi wa kata za Buyango, Ruzinga na Kitobo wilayani Missenyi, baadhi ya wananchi walisema chakula dawa kimekomboa afya za watoto wao, zilizokuwa katika hali mbaya, kutokana na baadhi yao kutokuwa na uelewa wa namna ya kuandaa chakula cha watoto.

Mmoja wa wananchi hao, Johanita Samwel, mkazi wa kijiji cha Kikono Kata Buyango, alisema analea mtoto wa shemeji yake ambaye alifariki dunia na kuwa alianza kumlea akiwa na uzito wa kilo tano wakati huo akiwa na umri wa miaka mitatu, lakini sasa ana miaka mitatu na nusu na ameongezeka uzito na kufikia kilo tisa.

"Mama yake alikimbia akamwacha mtoto na baba yake ambaye ni shemeji yangu, naye akafariki, ikabidi nimchukue mtoto akiwa na hali mbaya, nikapata elimu namna ya kumwandalia chakula, sasa anaendelea vizuri, alikuwa hawezi kutembea wala kutambaa, lakini sasa anatambaa na akipata pa kushikilia anajaribu kutembea, uti wa mgongo ulikuwa unaonekana sasa umerudi ndani kidogo," alisema Johanita.

Naye Renatus Mulokozi mkazi wa kijiji Rushasha katika kata ya Buyango, alisema wakati akifundishwa namna ya kuandaa chakula dawa, mtoto wake alikuwa na umri wa miaka mawili na miezi minne wakati huo akiwa na uzito wa kilo 8.5, na kuwa baada ya kufundishwa na kuanza kumlisha mtoto chakula dawa, kwa sasa ana uzito wa kg 11.4 na ana umri wa miaka miwili na miezi saba.

Anold Mutafungwa ofisa tathmini na ufuatiliaji kutoka Shirika la IMA mkoa wa Kagera, alisema mradi wa mtoto mwerevu unalenga kupunguza tatizo la udumavu mkoani humo na kuwa kwa takwimu za mwaka 2015/2016 zinaonyesha kati ya watoto kumi, watoto wanne wamedumaa.

## HABARI ARUSHA

# Wananchi waonywa mauaji ya simba

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

MENEJA wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Enduiment (EWMA), Peter Millanga, amekemea kitendo cha vijana wa jeshi la kimaasai (Moran) kufanya mauaji ya simba kutokana na mila na desturi zao hususani maeneo ya Kata ya Sinya. “Nimeumia sana na kusikitika kwa kitendo kilichotokea siku chache Kata ya Sinya, mauaji ya simba sijapendezwa kabisa, acheni hiyo tabia nawaomba,” alisema Millanga.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha mafunzo yaliyoandaliwa na Shirika la Oikos East Afrika kwa siku nne katika Tarafa ya Enduiment, yaliyolenga umuhimu wa uhifadhi na kupata watalii ndani ya jumuiya hiyo, alidai kuwa kama jamii itaendelea kuwa na tabia ya kuua wanyama wakali akiwamo simba watapoteza watalii na kukosa mapato. “Tukiwatunza na kuwapenda wanyama wakali kama vile simba, tembo, chui na mbogo, wageni wengi watavutiwa kuja Enduiment na kuacha kutumia safari ndefu kwenda Serengeti au Ngorongoro, tutunze wanyama wetu na mazingira yao,” alisisitiza Millanga.

Akizungumzia hali ya utalii katika jumuiya hiyo kwa miaka ya nyuma, alisema kwa sasa hali ni nzuri na wageni wameongezeka zaidi ya wageni 1,349, huku mapato yakiongezeka kwa asilimia 10. “Mwaka 2017 wageni waliotembelea hifadhi hiyo ni 2,501 na mwaka 2018 ni 3,850, huku mwaka 2019 wageni 1,021 hadi Aprili 2019, kwa mwaka jana tulikuwa na ongezeko la wageni 1,349 ikilinganishwa na wale wa mwaka 2017,” alieleza Millanga.

Aidha, aliwataka walioshiriki katika mafunzo hayo kuwa mabalozi wazuri katika kutoka elimu ya uhifadhi na faida zake popote watakapokuwa kwa kuwa jumuiya hiyo inahitaji ulinzi kutoka kwa wanajumuiya wa vijiji 11 wanachama.

“Hata hivyo, jumuiya hiyo kwa watalii wa ndani tunaowapata sana ni wale expatriates wanaofanya kazi kwenye mashirika mbalimbali, mwamko wa wazawa bado mdogo, wageni wa nje zaidi tunapata Wajerumani na Wamarekani, mataifa mengine yanayotufikia ni Uingereza, Italia na Spain,” alisema Millanga.

Kayongo Saigurani, mkazi wa kijiji cha Irikaswa alieleza kuwa hapo awali walikuwa hawafahamu kama wanyamapori ni chanzo cha mapato makubwa hapa nchini, lakini kwa sasa wametambua na kuiomba serikali kukemea mila na desturi kwa baadhi ya makabila ikiwamo desturi za mauaji ya wanyama.

“Naomba viongozi wa mila (Malaigwanani) wakutane na kuangalia juu ya desturi ya Moran kuua simba na kutafuta njia nyingine ya kutumika katika tamaduni badala ya kuua simba ambaye ni chanzo cha mapato makubwa hapa nchini,” alishauri Saigurani.

Hata hivyo, alieleza ili utalii uweze kukua kwa kasi katika hifadhi ya Enduiment jamii inapaswa kutunza vifaa vya asili na jadi ikiwamo mikuki, vibuyu, nyumba za asili (tembe), mavazi ya Kimaasai, shanga, nyimbo za asili (ngoma) na hata Morani kuendelea kusuka misuko ya asili.

Ofisa Wanyamapori Wilaya ya Longido (DGO), Lomayan Lukumay, alifafanua kuwa eneo la Longido ni la uhifadhi na wanyama wengi wanaotembea kuelekea Kenya na wengine kuingiza Tanzania.

“Kwa upande wa eneo la upande wa kulia kuelekea mkoani Arusha ni eneo la pori tengefu la Natroni ambalo lina vitalu vinne ambavyo ni Natron Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi huku eneo la kushoto likiwa ni kitalu cha Longido yenye hifadhi ya EWMA,” alisema. Akizungumzia kuhusu mauaji ya simba alisema sheria ipo wazi juu ya ujangili na kwa sasa wilayani hapa ujangili umedhibitiwa na wanyama wamekuwa wengi wanaonekana asubuhi, mchana na jioni na kama ikitokea mtu amebainika kufanya shughuli za ujangili atachukuliwa hatua kali za kisheria.

“Simba mmoja ana thamani ya Dola za Kimarekani 4,900, huku tembo mmoja akiwa na thamani ya Dola 15,000 hadi 20 kutokana na aina ya tembo aliyeuawa, niseme tu watu wawe makini sheria ni msumeno, “ alisema Lukumay.



Mkazi wa Dar es Salaam akipita karibu na malori yaliyobeba miwa yaliyoegeshwa katika Soko la Tandale yakisubiri kupakuliwa tayari kwa kuuzwa jumla. Baadhi ya wakulima wa miwa wamekuwa wakileta sokoni moja kwa moja na kuwauzia watengeneza juisi. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Tanzania yang’ara Afrika tuzo ya Kaizen

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KIWANDA cha A to Z Textile Mills kilichopo Kisongo jijini Arusha, kimeibuka mshindi wa kwanza katika Bara la Afrika na kuipa sifa Tanzania, kwa kupata tuzo ya kimataifa ya Kaizen katika viwanda bora vinavyofanyakazi kwa ufanisi.

Tuzo hiyo hushirikisha sekta mbalimbali ikiwamo viwanda vya kati na vikubwa na hutolewa na Shirika la Kimataifa la Misaada la Japan (JICA), kwa taasisi hizo kutekeleza majukumu yao kwa kufuata dhana ya Kaizen ambayo ni kuzalisha kwa tija, ubora na kupunguza gharama.

Kabla ya kuibuka na ushindi huo, A to Z iliibuka kidedea dhidi ya viwanda vyote vya Tanzania katika mashindano ya Tanzania Kaizen Award,

yaliyoandaliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia kitengo cha Kaizen Tanzania (TKU), yaliyofanyika Machi, 2019 jijini Dar es Salaam na kuchaguliwa kwenda kuiwakilisha Tanzania katika ngazi ya Afrika.

Akizungumzia tuzo hizo, kwa niaba ya kiwanda cha A to Z, Ruben Lyanga, ambaye ndiye mmoja wa wasimamizi wa kitengo cha Kaizen kiwandani hapo, alisema Tanzania ilipambanishwa na kampuni 16 barani Afrika katika kuandaa uwasilishaji wa shughuli mbalimbali za Kaizen zilizofanyika pamoja na mafanikio yake. Alisema katika uwasilishaji huo ambao hutokana na taarifa ya waangalizi wa tuzo hizo ambazo huzichukua awali baada ya kutembelea viwanda hivyo, waangalizi hao walikubaliana na maelezo yaliyotolewa na kukitangaza kiwanda hicho kuwa mshindi wa kwanza katika ngazi ya Afrika kwa viwanda vinavyoibukia na kutekeleza vyema dhana hiyo.

Lyanga alisema baada ya tuzo hiyo, Agosti mwaka huu A to Z itashiriki kwenye mkutano wa kimataifa unaojulikana kama TICAD7, utakaoshirikisha wakuu mbalimbali wa nchi kwa lengo la kuzungumzia maendeleo ya Afrika katika sekta tofauti ikiwamo sekta ya viwanda na pia katika mkutano huo, washindi wa tuzo ya Kaizen watapata fursa ya kueleza utekelezaji wake na mafanikio waliyopata.

Akizungumza kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa A TO Z, Kalpesh Shah, Meneja wa Biashara za Nje, Sylvester Kazi, alisema tuzo hiyo ya kwanza kutolewa Afrika ni zawadi ya Watanzania hasa kupitia serikali.

Alisema ni kweli kiwanda cha A to Z kimeibuka mshindi, lakini anayestahili kupewa hongera na pongezi nyingi ni Rais Dk. Magufuli kuwa mstari wa mbele kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda mbalimbali tangu alipoingia madarakani.

Kazi alimwomba Rais Magufuli kuipokea tuzo hiyo yeye mwenyewe au kupitia kwa kiongozi wa chini yake ambaye ataagiza apatiwe ili kuonyesha ishara ya uwajibikaji na utekelezaji wa malengo ya serikali yake ya kuanzishwa kwa viwanda na kutoa ajira nyingi kwa Watanzania.

## H’shauri Babati yashindwa kuomba miradi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, ameianika Halmashauri ya Babati kuwa ndiyo ya mwisho kati ya halmashauri za mkoa huo, kwa kushindwa kuandika andiko la kuomba miradi ya kimkakati na kuwataka kuomba msaada kama wataalamu wao wameshindwa.

Mnyeti aliwaanika mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa mkutano wa Baraza Maalum la Madiwani lililoitishwa kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG).

“Kwenye kuandika kuomba miradi ya kimkakati nyie ndio wa mwisho hii inatokana na wataalamu wenu wengine shule yao iko chini sana sijui mnashindwa nini wakati Hanan’g wameishawafikia na Kiteto muda siyo mrefu wanapata,” alisema Mnyeti.

“Kwanini mwenyekiti hauji kuniambia ofisa mipango wako hatoshi aondolewe apelekwe sehemu ambayo wameishawafikia na kama mnashindwa kuandika hiyo paper nendeni chuo cha Hombolo walipe Sh. milioni 28 wawaandikie,” alisisitiza.

Aidha, aliomba baraza hilo kumuonya mwekahazina wa halmashauri hiyo kuwa yeye ndiyo amesababisha hoja nyingi za ukaguzi za CAG licha ya halmashauri kuwa na hati ya kuridhishwa hivyo amemtaka kujitathmini yeye pamoja na wasaidizi wake ili mwakani hali hiyo isijirudie.

“Mwekahazina kakae na watu wako vizuri ili mfute hoja zenu mimi ningependa mwakani tujadili kurasa mbili siyo kujadili kitabu mwakani siko tayari kwenda kukutetea kwa Waziri Mkuu,” aliongeza.

Mnyeti alimwambia mtaalamu huyo wa fedha kuwa yeye hayuko tayari kutumbuliwa badala yake atamwajibisha kabla yake kuchukuliwa hatua.

Wakati huo huo, Mnyeti amewaonya wanasiasa wanaompaka matope kuwa ana nia ya kuwadondosha kutoka kwenye nafasi zao, huku akidai hana nia hiyo kwa mtu yeyote ila anashughulika na matatizo ya wananchi wa Manyara.

“Mimi ninapohangaika na shida za wananchi wa Manyara sitaki mtu anivuruge nitamfyatua mtu wa namna hiyo mimi sijaja hapa kushughulika na mtu kutoka kwenye nafasi yake,” alisema.

Alisema akiwa anahangaika na shida za watu wa Manyara asitokee mtu wa kuweka kifua wala mgongo maana yeye hatambeba mtoto mgongoni wala tumboni, watu wote ni sawa kwake.

Naye Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Nicodemus Tarimo, alisema kwenye miradi ya kimkakati hawatakubali kuwa wa mwisho, anadai wataalamu wamemwambia wanajitahidi, lakini sasa anaambiwa hawatoshi.

# Mghwira aagiza viongozi kuwasaidia wajane

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amewataka viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa kuhakikisha wanasaidia wanawake wajane baada ya kufiwa na waume zao ili waweze kupata haki zao.

Akizungunza na Nipashe ofisini kwake, alisema katika Mkoa wa Kilimanjaro, wajane wengi wamekuwa wakinyanyaswa kwa kudhulumiwa mali baada ya waume zao kufariki hali inayosababisha migogoro katika familia.

Alisema wajane wengi wanapoteza haki zao baada ya waume zao kufariki dunia na kusababisha kubaki na visasi, huzuni na ongezeko la watoto wa mitaani na magonjwa kutokana na msongo wa mawazo.

"Nawaagiza viongozi wote kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa kuhakikisha wanasimamia na kutetea haki za wajane baada ya wenzi wao kufariki ili kupunguza migogoro, dhuluma kwa wajane na watoto," alisema.

Alisema umefika wakati kinamama kuwa na sauti moja ya kukemea ukatili, ukeketaji na kurithiwa hali ambayo inaleta ongezeko la mitafaruku katika familia na kukwamisha maendeleo. Alisema viongozi wote hasa wa wilaya na mkoa wahakikishe wanafanya kazi ya kuwa wasuluhishi wa migogoro katika kutoa elimu kwa wananchi ili kuondokana na mila na desturi za ukandamizaji wa wanawake katika jamii.

"Nawaomba viongozi wa dini kuombea amani, kuwapa wananchi wa mkoa matumaini mapya kwa kuwapa ushauri nasaha za kuachana na vinyongo vilivyosababishwa na kudhulumiwa mali kwa muda mrefu... kwa kuwa vinyongo hasira na mambo yanayofanana na hayo husababisha magonjwa mbalimbali ikiwamo kansa," alisema.

Nao baadhi ya wajane katika Wilaya ya Moshi, Faustina Msaki, alikiri kuwapo kwa ukatili kwa wajane baada ya wezi wao wanapofariki na kuiomba serikali kukemea jambo hilo kwa vitendo bila kupokea rushwa kwa wenye nacho.

"Tunaiomba serikali mbali na kushiriki kwenye vikao vya familia na kutoa elimu, lakini pia mahakama zetu zisimamie sheria haki na usawa bila kumtizama mwenye nacho," alisema Elisaria Masawe (61), mkazi wa Moshi.

Mkurugenzi wa Shilirika la Kutete Haki na Msaada wa kisheria (KWIECO), Elizabeti Minde, alisema ikiwa mkuu wa mkoa na watendaji wake watasimamia kwa vitendo changamoto zanazowakabili wajane, wataweza kusaidika kwa haraka na tatizo la watoto wa mitaani litageuka historia mkoani Kilimanjaro.



Meneja Uzalishaji, Nurdin Bofu, akimwonyesha jambo Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angella Kairuki, wakati wa ziara yake katika kiwanda cha kutengeneza gypsum board cha KNAUF kilichopo Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WTU**

# Madereva bodaboda, Bajaj, Noah waonywa

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

SERIKALI wilayani Siha mkoani Kilimanjaro, imewaonya baadhi ya madereva bodaboda, Bajaj na Noah kuacha tabia ya kushiriki katika vitendo vya ubakaji wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Hatua hiyo imekuja baada ya takwimu kuonyesha katika Mahakama ya Wilaya ya Siha kwa mwaka 2018, mashauri ya jinai 27 kati ya 114 yaliyofunguliwa yanahusiana na makosa ya ubakaji. Zaidi takwimu zinaonyesha mwaka 2019 kufikia mwezi Mei, jumla ya mashauri yaliyofunguliwa ni 50 na kati ya hayo 17 ni ya ukatili kwa watoto na wanawake.

Mwaka 2018 takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mashauri 27 ya ukatili yaliyosikilizwa, 20 yalihusisha vifungo kwa watuhumiwa wa ukatili huo kwenda jela/gerezani kwa miaka kati ya 30 na 60 pamoja na vifungo vya maisha. Kwa mwaka huu tayari mashauri saba yameshaamuliwa na yote yamehusisha vifungo.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, akizungumza na madereva wa bodaboda na bajaji wakati akitoa elimu kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto uliofanyika katika kiwanja cha Sanya Juu yenye kaulimbiu 'Siha bila ukatili wa wanawake na watoto inawezekana', aliwataka wanaume kuacha kuwarubuni wanafunzi.

Alisema kuna wanawake wamejaa mtaani wa kuoa na kuwaonya kwa kuwaacha wanafunzi wasome kwanza ili taifa liwe na wasomi.

"Ebu jifikirie unakwenda kutumikia jela miaka 30 kwa kubaka mwanafunzi, huku wewe mwenyewe una miaka 35 ukirudi hapo umezeeka na maisha yako wewe na familia yako unakuwa umeshayaharibu," alisema.

Semina hiyo ya siku moja ilitolewa kwa viongozi mbalimbali wakiwamo wa Mahakama ya Wilaya Siha, Dawati la Jinsia na Watoto, Ustawi wa Jamii, wasaidizi wa kisheria.

Mwenyekiti wa umoja wa madereva bodaboda wilayani humo, Arodi Peter, aliwataka wanafunzi kutulia kwa kuwa baadhi yao ndiyo wanawafuata wanaume. Akitoa mfano, alisema mwanafunzi mmoja ambaye wilayani humo baada ya wazazi wake kumtafuta kwa muda mrefu walimkuta akiishi na mwanamume na alipoulizwa alisema yeye hafahamu kama yule ni mwanafunzi.

Pia mwingine alitoroka nyumbani kwao na kwenda kuishi katika Kijijij cha Majengo na wananchi walipogundua walitoa taarifa kwa uongozi wa kijiji kuwa nyumba ya jirani kuna mwanafunzi anaishi.

Alisema baada ya polisi kufika eneo hilo wakiongozana na viongozi wa kijiji walipekua nyumba hiyo, lakini hawakumkuta mwanafunzi huyo wakati wanaondoka ndipo askari alipohisi jambo na kwenda kufunua karai kubwa na kumkuta binti huyo amejificha kwenye karai hilo. "Mwanafunzi kama huyo kwanini isitengenezwe sheria kwa kitendo alichofanya badala yake sheria inambana mwanaume peke yake tunaomba serikali iangalie jambo hili ili haki itendeke kwa wote," alisema Peter.

Vile vile, alitaka somo la ukatili wa wanawake na watoto litolewe kwa jamii nzima wilayani kuanzia ngazi ya kitongoji hadi wilaya badala ya kuishia kwa madereva peke yao.

# H'shauri Moshi yapewa jukumu hoja za CAG

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro imetakiwa kufanyia kazi hoja 53 zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), katika taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2017/18 ili kuepuka kupata hati chafu mwaka wa fedha 2018/19.

Hayo yalibainishwa na Mkaguzi Mkuu wa Nje wa Hesabu za Serikali mkoa, Anorld Kishimbo, wakati wa Baraza Maalum la Madiwani la kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18 na halmashauri hiyo ilipata hati safi ya mashaka.

Kishimbo alisema, halmashuri hiyo imekuwa ikipambana kuhakikisha inapata hati safi na katika ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2016/17 ilipata hoja 121, lakini katika mwaka wa fedha wa 2017/18 imejitahidi kupunguza hoja hizo kwa kuzifanyia kazi na kufikia 53 na kuwataka kupambana kuzimaliza.

"Niwapongeze Halmashauri ya Moshi kwa kupata hati safi yenye mashaka hivyo mnapaswa kuongeza juhudi kubwa kuhakikisha maoni yaliyotolewa na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali mnayafanyia kazi ili kuondoa kabisa hoja na itawasaidia mwaka wa fedha 2018/19 msipate hati chafu," alisema Kishimbo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, aliwataka watumishi wa halmashauri hiyo kwa kushirikiana na madiwani kuhakikisha mapendekezo yote yaliyotolewa na CAG yanafanyiwa kazi pamoja na maoni ya kamati ya fedha na mipango ya halmashauri hiyo ili kumaliza hoja hizo zilizopo katika ripoti ya mkaguzi.

Warioba alisema, kuendelea kupungua kwa hoja hizo kutasaidia halmashauri hiyo kupata hati safi isiyo na mashaka na kuwataka kila mtendaji kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu na weledi mkubwa.

"Natambua wapo baadhi ya watumishi ambao wamekuwa sio wazalendo katika utendaji kazi wa majukumu yao na ndiyo wanaosababisha kuzalishwa kwa hoja hizi hivyo mnapaswa kuwachukulia hatua watumishi hao ili wasiweze kuwakwamisha na kupata hati chafu," alisema Warioba.

Naye Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa, Grace Makiluli, alisema kuwa, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imeichukua hoja ya kufanyika mafunzo mara kwa mara kwa watumishi wa serikali na itaanza kutoa mafunzo kwa wataalamu wanaosimamia mifumo na fedha ili kuondoa makosa yanayosababishwa ya kiutendaji.

Aliwataka madiwani kuendelea kufuatilia kwa ukaribu ili kuhakikisha hoja zilizotolewa katika taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hazijirudii.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Moshi, Michael Kilawilam, alisema katika kamati ya fedha wameazimia watumishi wanaoshindwa kubadilika na kuendelea kufanya kazi kwa mazoea watawachukulia hatua ikiwamo kuwaondoa ili kuwapisha watu wengine.

Kilawila alisema aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo kuunga mkono mambo mazuri ya maendeleo yanayofanywa na serikali na kuweka pembeni itikadi za vyama katika shughuli za maendeleo.

Nipashe

# Spotika



SABABU STARS KUWA YA KWANZA KUAGA AFCON UK.18



# SAMBARATISHA...

Beki wa Peru, Carlos Zambrano, akiwahi kuucheza mpira kwa kichwa dhidi ya mshambuliaji wa Uruguay, Luis Suarez kwenye mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano ya Copa America iliyopigwa Salvador, Brazil na Peru kushinda kwa mikwaju ya penalti 5-4. **HABARI UK. 15**

## ISIKUPITE

Aaron Wan-Bissaka ambaye ametua Old Trafford kwa pauni milioni 50 akitokea Crystal Palace, ambapo sasa atakuwa akilipwa pauni 80,000 kwa wiki, anakuwa mchezaji wa tano kununuliwa kwa dau kubwa Manchester United baada ya Paul Pogba, Romelu Lukaku, Angel di Maria na Fred.

SOKA

# USAJILI MPYA MADRID NA WATAKA-OPOTEZWA



Praet

**MADRID, Hispania**

MSIMU uliomalizika hivi karibuni wa Ligi Kuu za Ulaya, ulikuwa mbaya zaidi katika historia ya Klabu ya Real Madrid, kwani 'Los Blancos' hao walijikuta wakimaliza bila kuwa na taji lolote mkononi, huku wakiwa na kiwango kisichovutia kabisa dimbani.

Klabu hiyo ikaamua kujibu kiaina kutokana na hali hiyo kwa kutumia kiasi cha euro milioni 270 kwa ajili ya kuleta wachezaji wapya, huku pia wengi wakitajwa kutua kwa miamba hao wa soka la Hispania ili kuimarisha kikosi chao kwenye Ligi Kuu na mashindano ya Ulaya msimu unaokuja.

Ili kupata kiasi kikubwa zaidi cha fedha na kuingia kwa nguvu kwenye soko la usajili, Real Madrid watalazimika kuwauza baadhi ya wachezaji wake ili kupata fedha zaidi za kuingia sokoni na kusajili nyota wakali.

Makala haya yanawaangalia wachezaji watano ambao kwa kiasi kikubwa wanaonekana wataathirika na usajili mpya wa Real Madrid.

**5. MARCELO**

Wakati Marcelo pengine alikuwa beki bora zaidi wa kushoto kwa zaidi ya miaka saba iliyopita, lakini msimu uliopita unaweza kuwa ni wakati ambao nyota huyo mwenye umri wa miaka 31, hataki kabisa kuukumbuka. Kwani alikuwa mmoja wa wachezaji waliokuwa kwenye kiwango kibovu zaidi katika kikosi cha Real Madrid, na matokeo yake akapoteza namba ya kuanza kikosi cha kwanza kwa kinda, Sergio Reguilon.

Kiwango chake kimataifa pia kilionekana kushuka, kwani licha ya kuichezea timu ya Taifa ya Brazil mechi 58, aliachwa na kocha Tite katika kikosi cha wachezaji 23 kinachoshiriki michuano ya Copa America 2019 inayoendelea kwenye ardhi ya nyumbani kwao.

Usajili wa Real Madrid wa beki wa Ufaransa, Ferland Mendy ni ishara kwamba kocha, Zinedine Zidane haoni kama Marcelo anaweza kuwa kwenye mipango ya muda mrefu ya kikosi cha Real Madrid.

Mapema mwaka huu, uvumi ulizagaa kwamba, Marcelo angeweza kujiunga na Juventus na uhusiano wake mzuri na Cristiano Ronaldo, ulitajwa kwamba ndio ungekuwa chanzo cha yeye kuondoka hapo kwenye dimba la Bernabeu.

**4. MARIANO DIAZ**

Baada ya kuuzwa kwa Cristiano Ronaldo, huku Rais wa Real Madrid, Florentino Perez kutonunua mbadala wake kwenye safu ya upachikaji mabao, waliamua kumchukua mchezaji wao wa zamani, Mariano Diaz kutoka Lyon.

Na mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alipewa jezi namba saba ambayo ilikuwa ikivaliwa na wachezaji bora kabisa hapo Real Madrid.

Ni rahisi kusema kwamba, Mariano Diaz ndie pengine mchezaji aliyeonyesha kiwango duni zaidi kati ya wachezaji waliowahi kuvaa jezi namba saba pale Real Madrid, alishindwa kufanya maajabu yoyote, alifunga mabao manne tu katika mechi 19 alizoichezea kwenye mashindano yote, huku pia akiwa na wakati mgumu wa kuwa na namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

Kuwasili kwa Eden Hazard klabuni hapo kwa ada iliyoweka rekodi ni wazi kwamba siku zake za kucheza hapo Real Madrid zinafikia mwisho, huku Valencia ikitajwa kuwania saini yake.

**3. JAMES RODRIGUEZ**

Baada ya kung'ara kwenye Kombe la Dunia mwaka 2014 na kutwaa Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora, James Rodriguez alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi kutua Real Madrid.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia awali alipata namba kwenye kikosi cha kwanza chini ya Kocha Carlo Ancelotti, lakini chini ya Zinedine Zidane kiwango chake kikashuka.

Kipindi cha kucheza kwa mkopo wa miaka miwili kule Bayern Munich, kilimalizika mwaka 2017 na licha ya awali kuwa na taarifa kwamba miamba hao wa Ujerumani wangeweza kumsajili moja kwa moja, kiungo huyo na klabu yake wakakubaliana arudi tena pale kwenye mji mkuu wa Hispania.

Na hilo likamfanya kuwa kwenye hali ngumu zaidi, kwani majaliwa yake yalionekana kutokuwapo pale kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu, huku mkataba wake ukiwa umebaki mwaka mmoja, Real Madrid wanaweza kufikiria kumuuza. Hana ushawishi wa kutakiwa na klabu nyingi Ulaya, lakini anaweza akanunuliwa na timu yoyote.

**2. ISCO**

Isco amekuwa mchezaji wa Real Madrid tangu mwaka 2013 na ameichezea mechi 277 katika mashindano yote, akifunga mabao 47 akishinda taji moja la Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Isco alitajwa kuwa ni mchezaji wa kizazi cha dhahabu mwaka 2012 na kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani kwa wakati huo. Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, maendeleo yake yameonekana kudidimia na kiwango chake kutokuwa cha kuvutia.

Huku Zinedine Zidane akiwa kwenye harakati za kukijenga kikosi chake upya, kuna uwezekano akamwachia mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania kuondoka ili apate fedha za kuendelea kununua wachezaji wengine wapya.

Klabu kama Manchester City na Juventus zimekuwa zikitajwa kuwania saini yake kwa muda mrefu na inaonyesha wazi kwamba nafasi yake pale Santiago Barnabeu haipo tena.

**1. GARETH BALE**

Mmoja wa wachezaji ghali duniani na ambaye alikuwa na uwezo wa kushinda tuzo ya Ballon d'Or, Gareth Bale amejikuta kwenye wakati mgumu kwa kushuka kwa kiwango chake.

Raia huyo wa Wales alitua pale Real Madrid mwaka 2013 kwa ada iliyoweka rekodi akitokea Tottenham na iliaminika kwamba angeweza kuonyesha kiwango cha juu zaidi kushinda kile alichokuwa nacho kwa miamba hao wa London Kaskazini.

Hata hivyo, hili halikutokea, na baada ya miaka sita ya kusherehekea ubora wake, sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 hajafanya makubwa ya kutosha akiwa na jezi ya Real Madrid licha ya kuwa anachukua mshahara mkubwa.

Katika siku zake, Bale alikuwa akitajwa kama mchezaji mwenye kipaji cha hali ya juu, akiwa katika jezi ya Real Madrid mwanzo wake ulionekana kuwa mzuri. Hata hivyo, majeraha ya mara kwa mara yalifanya kipaji chake kuporomoka kwa haraka.

Zinedine Zidane ameshaonyesha wazi kuwa Gareth Bale hana majaliwa ya kuendelea kucheza pale Real Madrid ingawa inaonekana ni ngumu kumuuza kutokana na umri wake pamoja na mshahara wake kuwa mkubwa zaidi, lakini klabu hiyo itafanya kila iwezalo kuhakikisha wanamtafutia timu mpya kwa ajili ya msimu ujao.

**JE, WAJUA?**



Divock Origi ni mchezaji wa pili Ubelgiji kuweza kufunga kwenye mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya Yannick Carrasco aliyeifungia Atletico Madrid dhidi ya Real Madrid mwaka 2016.

MICHEZO




Zacharia Hans Poppe akipeana mkono na Mbrazil Gerson Fraga Vieira (kulia) baada ya kutia saini mkataba wa kujiunga na Simba.

# SABABU 5 SIMBA KULETA WABRAZIL

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Simba imekuwa ikisainisha wachezaji kwa ajili ya kuichezea timu hiyo kwa msimu ujao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Dirisha la usajili kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa limemalizika jana Juni 30 na zimebaki wiki mbili za nyongeza ambazo zitakuwa ni za faini, ikiongezeka kila baada ya wiki moja.

Na kwa upande wa dirisha la usajili kwa ajili ya Ligi Kuu lenyewe litafungwa Julai 15, mwaka huu. Na katika hali iliyowashangaza mashabiki wengi nchini hata wa Simba wenyewe ni kunasa saini za wachezaji kutoka nchini Brazil.

Ilianza kuwashtua watu ilipomsainisha straika Wilker da Silva, wakati mashabiki wengi nchini wakiwa kwenye mshangao, wanamsajili mchezaji mwingine kutoka huko anayecheza nafasi ya beki wa kati Gerson Fraga Viera.

Wakati kukiwa na mijadala mbalimbali mitaani na kwenye mitandao ya kijamii, ikamshusha Mbrazil mwingine ambaye ni beki anayeweza kucheza nafasi karibuni zote za nyuma, Tairone Santos da Silva.

Kumekuwa na mitazamo tofauti kwa wapenzi wa soka nchini juu ya Simba kuchanganya wachezaji kwani pamoja na kunasa saini ya baadhi ya wachezaji wa Kiafrika, lakini sasa imeamua pia kuwa na Wabrazil.

Mwandishi wa makala haya ameorodhesha sababu tano ambazo zinaweza kuwa ndiyo zimewafanya viongozi na benchi la ufundi la Simba kufanya hivyo.

**1. KUTOKA ILIPOISHIA KWENDA INAPOPAHITAJI**

Simba iliishia hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliomalizika na kwa mujibu wa viongozi wao, akiwamo mwekezaji wao mkuu, Mohamed "MO" Dewji ni kuifanya timu hiyo kufanya vema msimu unaofuata.

Kama lengo ni hilo, haiwezekani ikawa na wachezaji wale wale waliokuwa nao msimu uliopita, hivyo ni lazima waingize wachezaji wapya ambao uwezo wao ni zaidi ya wanaotoka.

Ofisa Mtendaji wa klabu hiyo, Cresentius Magori anasema kuwa asilimia kubwa ya wachezaji wenye uwezo wa kuisaidia timu hiyo kufanya vema kwenye michuano ya kimataifa ni wa nje, hivyo ni lazima wawaondoe baadhi ya wachezaji wageni, ili kupisha wengine wenye uwezo mkubwa zaidi.

Lengo la msimu ulioisha lilikuwa ni kuishia makundi, lakini ikafika robo fainali, hivyo usajili unaofanyika sasa ni kuifanya timu hiyo kufika angalau robo fainali kwa lengo la chini.

**2. DAU KUBWA LA WACHEZAJI WA KIAFRIKA**

Kuna tatizo kama vile la kukomoana kwa klabu na klabu kwenye soka la Kiafrika hasa linapokuja suala ya usajili wa wachezaji wanapokuwa bado na mikataba. Kuna baadhi ya klabu hutaja dau kubwa kwa wachezaji ambao kiuhalisia hawana thamani hiyo au uwezo unaolingana na dau linalotajwa.

Na hii imesababisha baadhi ya klabu nyingi Afrika kusubiri wachezaji ambao mikataba yao inamalizika.

Taarifa zinaeleza kuwa Simba iliwakosa baadhi ya wachezaji inaowahitaji kwa kutajiwa dau kubwa zaidi kuliko uwezo halisi wa wachezaji, hivyo ikaona ni bora kutafuta wachezaji ambao dau na thamani yao vitakuwa vinaendana. Kwa sasa soko lipo kwa wachezaji wa Amerika ya Kusini ambao kwa thamani ya pesa inayomnunua mchezaji wa Kiafrika unapata mwenye kiwango cha juu zaidi yake.

**3. KUENDANA NA FALSAFA YA SOKA LAO**

Kiasili Simba ina falsafa yao ya soka ambayo inaifuata tangu kuanzishwa kwake mwaka 1936. Ni soka la chini, la pasi fupi, na kufanya mashambulizi mengi zaidi kuliko kuzuia.

Ndiyo maana hata ikishinda, kama haikucheza kwenye mfumo uliozoeleka, wanachama na mashabiki wake bado huwa hawaridhiki. Ni kama vile haijapotea katika kusainisha wachezaji kutoka Brazil, kwani nchi hiyo inasifika kwa kuwa na wachezaji wenye vipaji vya hali ya juu kutandaza soka hasa la chini, pasi fupi na ubunifu mwingi.

**4. KUTIBU UPUNGUFU MECHI ZA KIMATAIFA**

Pamoja na Simba kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini ilikuwa na upungufu mwingi hasa kwenye safu ya ulinzi.

Ilikuwa ikiruhusu mabao mengi kwenye mechi za ugenini. Ilifungwa mabao 5-0 dhidi ya AS Vita na idadi kama hiyo kwenye mechi dhidi ya Al Ahly, ikikubali pia kipigo cha mabao 4-1 dhidi ya TP Mazembe. Moja kati ya upungufu ni mabeki wake kushindwa kuruka kuokoa mipira ya vichwa.

Ukiangalia mabeki wawili waliosajiliwa Gerson na Tairone ni warefu na wakakamavu, lakini Kocha Mkuu Patrick Ausems, anasema kuwa anahitaji mabeki wenye uwezo wa kumiliki mpira ili kuwa na uwezo wa kuanzisha mashambulizi si kubutua, na hilo si la kuuliza kwa wachezaji wa Kibrazil.

**5. KUFUATA NYAYO ZA MAMELODI SUNDOWNS**

Inaonekana ni kama viongozi wa Simba wamechungulia au kumegewa siri ya mafanikio ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini ambayo ina idadi kubwa ya wachezaji kutoka Amerika ya Kusini.

Mamelodi, Mabingwa wa Afrika mwaka 2016, msimu uliomalizika ilitolewa hatua ya nusu fainali na Wydad Casablanca ya Morocco.

Jambo lisilosahaulika ni timu hiyo kuichapa Al Ahly mabao 5-0 nyumbani na kufunga bao 1-0 ugenini.

Siri ya mafanikio ni kuwapo kwa baadhi ya wachezaji kutoka Amerika ya Kusini ambao ni Leandro Gaston Sirino raia ya Uruguay, Ricardo dos Santos Nascimento ambaye ni Mbrazil, Emilliano Tade raia wa Argentina, Jose Meza Draegertt kutoka Venezuela, lakini pia yupo Jeremy Russell Brockie, yeye akitoka New Zealand. Wachezaji hawa wenye wa umri wa kati ya miaka 28 hadi 33, ndiyo wamekuwa mhimili wa klabu hiyo na kuiletea mafanikio, licha ya kwamba hawana majina makubwa na wametoka kwenye klabu za chini huko kwao, lakini wakiuwasha moto vilivyo kwenye Ligi Kuu Afrika Kusini na Ligi ya Mabingwa kwa ujumla.

## NJE YA UWANJA

### Neymar amfariji Suarez tuta Peru

Neymar ameahidi kumfariji Luis Suarez baada ya nyota huyo wa Uruguay kukosa penalti na kusababisha timu yake ya taifa kutupwa nje na Peru kwenye mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano ya Copa America.

Suarez alikuwa mchezaji pekee aliyekosa penalti katika hatua ya matuta kufuatia sare tasa kwenye mechi hiyo na hivyo kuipa nafasi Peru kutinga nusu fainali kwa mikwaju ya penalti 5-4 katika mchezo huo uliopigwa Salvador, Jumamosi.

Mshambuliaji huyo wa Barcelona alimwaga machozi baada ya kipigo hicho ambacho ni cha kwanza kwa Uruguay – kufuatia kutopoteza mechi yoyote katika hatua ya makundi.

Suarez ambaye walicheza pamoja na Neymar Barca, na ambaye anahusishwa na kurejea kikosini hapo akitokea Paris Saint-Germain, ameahidi kumfariji nyota huyo wa Uruguay.

"Simama," majeruhi huyo wa Brazil aliandika katika ukurasa wake wa Instagram, pembeni akiweka picha ya Suarez akilia.

"Wewe ni mzuri sana, kaka. Nakupenda rafiki."

Neymar anahusishwa sana na kurejea Barcelona kuelekea msimu ujao, ikiwa ni miaka miwili baada ya kuachana na mabingwa hao wa La Liga.



## Extra Time

# NYOTA WA5 WANAOWEZA KUONDOKA EPL



Zaha

**LONDON, England**

LIGI Kuu ya England inachukuliwa na wengi kuwa moja ya ligi yenye ushindani mkubwa na ya kuburudisha zaidi duniani, hasa kutokana na ukweli kwamba, mamilioni ya mashabiki wamekuwa wanaifuatilia kila wiki pamoja na wachezaji wao.

Kuongezeka kwa fedha za udhamini kwenye ligi hiyo pamoja na matangazo mengi na kuwa na mapato makubwa kwa klabu, maana yake timu zimekuwa na uwezo wa kutumia fedha za kutosha kusainisha wachezaji nyota duniani.

Katika miaka ya hivi karibuni, imeshuhudiwa kwamba si tu wachezaji bora watatua kwenye Ligi Kuu ya England, bali pia makocha bora duniani wanakimbilia EPL na hilo kwa kiasi kikubwa limechangia ligi hiyo kuwa na mvuto mkubwa.

Msimu uliomalizika ulishuhudiwa timu nne zote kutoka Ligi Kuu England zikiingia kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na ile ya Europa na mabingwa kutokea huko.

Hata hivyo, pamoja na kuingiza fedha za kutosha, klabu za Ligi Kuu ya England hazina kinga ya wachezaji wake kunyakuliwa na Klabu za Hispania, Italia na hata China, huku ikiwa imeshashuhudiwa nyota kama Cristiano Ronaldo, Gareth Bale, Luka Modric, Luis Suarez na Philippe Coutinho wakiondoka na kwenda kutafuta maisha bora zaidi kwingineko.

Msimu huu wa kipindi cha majira ya joto tayari imeshuhudiwa wachezaji kadhaa wakiondoka kwenye Ligi Kuu ya England, huku Eden Hazard akiweka rekodi ya usajili na kutua pale Real Madrid, wakati Aaron Ramsey na Ander Herrera pia wamejiunga na Klabu za Juventus na PSG.

Huku ikiwa imebakia miezi miwili kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto, bado kunaweza kuwa na wachezaji kadhaa wakubwa watakaoondoka kwenye Ligi Kuu ya England. Makala hii inakuchambulia wachezaji watano ambao wanaonekana kwamba wanaweza kuondoka England.

### 5. IDRISA GUEYE

Idrisa Gueye aliwasili kwenye Ligi Kuu ya England kipindi cha majira ya joto mwaka 2015 wakati aliposajiliwa pale Aston Villa akitokea Lille ya Ufaransa kwa ada ya pauni milioni tisa na aliweka heshima kwa uwezo wake wa kukaba dimbani.

Alimaliza msimu wake wa kwanza akiwa ameweza kukaba na kushinda mpira mara 144 na kuwa wa pili kwenye Ligi Kuu ya England nyuma ya kiungo wa Leicester wakati huo, N'golo Kante na msimu uliofuata akakaba na kushinda mpira mara 135 na alimaliza katika nafasi ya pili katika kipindi cha misimu minne aliyokaa England.

Uwezo wake dimbani ndio umemfanya mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal sasa kujikuta akiwania na timu kubwa Ulaya, huku mabingwa wa Ufaransa, PSG wakiwa na nafasi kubwa zaidi.

Hata hivyo, Everton walikataa ofa ya kwanza iliyotolewa kwa ajili ya kiungo huyo, lakini ni wazi kwamba haitaweza kuzikataa ofa zote.

Na inaonyesha wazi kwamba klabu hiyo itarudi kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, na kutoa ofa nyingine kwa Gueye baada ya michuano ya mataifa ya Afrika, Afcon, ambako anaiwakilisha nchi yake.

### 4. ALEXIS SANCHEZ

Kulikuwa na matarajio makubwa mno kwa mashabiki wa Manchester United wakati Alexis Sanchez alipomwaga wino katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa usajili wa dirisha la Januari 2018.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile alikuwa katikati ya vita kati ya klabu za jiji moja la Manchester na mwisho wa siku City wakajikuta wakishindwa kwenye mbio za kuwania saini yake na akatua pale Old Trafford.

Moja ya mambo waliyoyafanya Man United ni kumfanya kuwa mchezaji anayelipwa kiasi kikubwa zaidi cha mshahara katika historia ya Ligi Kuu ya England. Kwani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 analipwa kiasi cha pauni 400,000 kwa wiki, lakini ameshindwa kuifanyia lolote klabu hiyo.

Alifunga mabao matano katika mechi 45 alizocheza kwenye mashindano yote na hivyo kujikuta akiwa garasa kubwa kwa klabu hiyo.

Mshahara wake mkubwa ndio umekuwa kikwazo kwa Manchester United kufanya naye mazungumzo kwa ajili ya mkataba mpya na ni wazi kwamba watamwachia kipindi hiki.

Huku Inter Milan ya Italia ikitajwa kwamba inamtaka nyota huyo, Man United kwa vyovyote itafanya lolote kuhakikisha kwamba anaondoka klabuni hapo. Mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona mchango wake umeonekana kuwa si chochote kwa klabu hiyo.

Hata hivyo, mchezaji huyo anayevaa jezi namba saba pale Manchester United, kiwango chake kwenye michuano ya Copa America kimekuwa cha kuvutia zaidi tofauti na anapokuwa kwenye dimba la Old Trafford.

### 3. WILFRED ZAHA

Wilfred Zaha alikuwa katika akademi ya watoto wa Crystal Palace kutoka mwaka 2004 hadi 2010, akapandishwa katika kikosi cha kwanza mwaka 2010 na alitumia misimu mitatu kuichezea klabu hiyo.

Ukafuatia uhamisho wa kwenda Manchester United Januari mwaka 2013, lakini katika misimu yake miwili kama mchezaji wa United, Zaha alishindwa kuonyesha thamani yake, akicheza mechi mbili tu za Ligi Kuu na akapelekwa kwa mkopo mara mbili.

Alirudi tena Crystal Palace mwaka 2015 na ameonyesha kiwango cha juu kabisa, na klabu nyingine kuanza kummezea mate.

Zaha ni mchezaji mwenye kipaji cha hali ya juu, lakini amekuwa akishutumiwa kwa kuwa na kiwango cha kupanda na kushuka pamoja na nidhamu mbovu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amebainisha kwamba anatamani kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast ameonyesha ishara ya kutaka kuondoka na kwenda kwenye klabu kubwa.

Ndoto zake zinaweza kutimia kwani kocha wa miamba wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Borussia Dortmund, Lucien Favre alisema Januari kwamba anaweza kumsainisha Zaha kipindi hiki cha majira ya joto.

Kwa sasa yupo na timu yake ya Taifa ya Ivory Coast kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon), na pengine akirudi anaweza kuondoka kwenye Ligi Kuu ya England.

### 2. CHRISTIAN ERIKSEN

Christian Eriksen anatajwa kwamba ni mmoja wa viungo wachezeshaji bora kabisa si tu kwenye Ligi Kuu ya England, lakini duniani kote, hiyo ikitokana na mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark akionyesha uwezo wa juu zaidi katika klabu yake hiyo kwa kuwalisha mipira 'mitamu' washambuliaji wake.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, licha ya kiwango chake hicho, lakini hakijamlipa, huku Tottenham haijatwaa taji lolote katika miaka ya hivi karibuni na pia hawawezi kumlipa mshahara mkubwa zaidi anaoutaka.

Huku akiichezea kwa mapenzi yote klabu hiyo ya London Kaskazini kwa kipindi cha miaka sita, ishara inaonyesha kuwa mchezaji huyo wa zamani wa Ajax majaliwa yake pale White Hart Lane yanaweza kufikia mwisho kipindi hiki cha majira ya joto.

Amekuwa anatajwa zaidi kwenda Real Madrid ambao wamekuwa wakimfuatilia kwa muda mrefu, huku taarifa za hivi karibuni zikieleza kwamba, Spurs imewaomba Real Madrid wapewe Marco Asensio kwa ajili ya kubadilishana na Eriksen.

### 1. PAUL POGBA

Paul Pogba aliwasili Manchester United kipindi cha majira ya joto mwaka 2016 kwa ada iliyoweka rekodi wakati akitoka kule Juventus, huku akitajwa kuwa mmoja wa viungo wenye kasi zaidi duniani.

Awali akiwa kinda alicheza katika akademi ya hapo Manchester United mwaka 2012 na aliporudi alionekana kuwa mkombozi wa kweli wa 'Mashetani Wekundu' hao.

Hata hivyo, amekuwa na kiwango cha kupanda na kushuka, huku pia alikuwa katikati ya mgogoro na kocha Jose Mourinho ambaye alifukuzwa Desemba mwaka jana.

Ndani ya miaka mitatu ya uwapo wa Pogba hapo Man United, ameshindwa kuonyesha thamani yake na mashabiki wamegawanyika kwa mtazamo wao kwa nyota huyo.

Mapema wiki iliyopita, mshindi huyo wa Kombe la Dunia alitamka wazi kwamba anataka kupata changamoto mpya na kuwa anataka kuondoka Man United, huku Real Madrid ikitajwa kuwa ndio sehemu anayokwenda.

Miamba hao wa Hispania kwa muda mrefu wamekuwa wakimwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, huku klabu yake ya zamani ya Juventus pia ikitaka kumsajili tena.

## Nukuu

"Sawa, nilikuwa nafikiria kwenda kufanya kazi nchi nyingine, huo ndio ulikuwa mpango wangu baada ya kukaa kwa muda mrefu England, lakini kwa sasa huko ndiko kunakostahili niwapo," **Arsene Wenger akikiri kuwa na mpango wa kurudi kufanya kazi Ligi Kuu England, lakini akijiweka mbali na mpango wa kwenda kuinoa Newcastle United.**



"Kuna fursa kwangu ya kwenda katika uongozi moja kwa moja, na wakati nitakapotundika daluga, uamuzi huo utafanywa na matarajio ya klabu yangu yatakuwa ya kwanza kwa yote. Scott Parker, John Terry pale Aston Villa - ni nzuri kwangu binafsi, ambaye ninataka kwenda katika uongozi, kuona vijana hawa wanapata fursa na inakupa matumaini kwamba itatokea kwako," **Wayne Rooney akielezea malengo yake ya kuwa kocha.**



"Kile ninachoamini ni kwamba Neymar anataka kurudi, lakini kusema kwamba tumeanza mikakati ya kutaka kumsainisha hicho ni kitu ambacho si cha kweli. Hatusajili mtu yeyote kwa sasa hasa mchezaji huyu ambaye hatujawasiliana naye," **Makamu Rais wa Barcelona, Jordi Cardoner akisisitiza kuwa hakuna mawasiliano yoyote yaliofanyika ya kumrejesha Neymar kutoka PSG**



# SABABU STARS KUWA YA KWANZA KUAGA AFCON



Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta (kulia), akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikichapwa 3-2 dhidi ya Harambee Stars katika mechi ya Afcon Kundi C wiki iliyopita.

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), imekaa kwa muda wa miaka 39 bila ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon), mashindano ambayo ni makubwa barani hapa.

Na mwaka huu, hizi ni fainali za 13 zikiwa zinafanyika katika majiji manne tofauti ambayo ni Cairo, Alexandria, Suez na Ismailia, katika taifa hili lenye watu milioni 99.21 kwa mujibu wa takwimu huku Cairo pekee likielezwa kuwa na wakazi milioni 19.5.

Mwaka huu kwa mara ya kwanza, fainali hizo zimeshirikisha nchi 24, baada ya uongozi mpya chini ya Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (Caf), Ahmad Ahmad, kufanya mabadiliko katika idadi ya timu.

Kuelekea fainali hizo, Taifa Stars ilikuwa inatumia kauli mbiu isemayo "Afcon 2019 Ni Zamu Yetu", na kwa juhudi zilizoonyeshwa na wachezaji, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), serikali, wadau mbalimbali na mapenzi ya Mungu, ndoto za Watanzania kufuzu kushiriki fainali hizo zilitimia.

Ilikuwa ni vita ambayo iliwaunganisha Watanzania wote bila kujali tofauti walizonazo katika klabu wanazozishangilia au vyama vyao vya siasa wanavyoviishabikia.

Katika safari hiyo, tulishuhudia wanasiasa wa upinzani na chama tawala (CCM), wakikaa kupanga mipango ya ushindi na kuonekana jukwaani wakishangilia pale timu inapopata matokeo mazuri au wakihuzunika endapo Stars inakuwa imefungwa.

Licha ya Stars kuwa imepata nafasi ya kushiriki fainali hizi, bado mwamko kwa mashabiki haukuwa mkubwa kama timu hiyo ilivyokuwa chini ya Kocha Mkuu Mbrazil Marcio Maximo, ambaye baadaye alirejea nchini kuifundisha Yanga.

**STARS NDANI YA MISRI**

Kikosi hicho kinachonolewa na Mnigeria Emmanuel Amunike, ndicho kilikuwa cha kwanza kutua nchini hapa, kati ya timu 24 zinazowania ubingwa huo unaoshikiliwa na Cameroon.

Taifa Stars ilifika mapema, kwa sababu iliamua kuweka kambi mjini Alexandria, na kambi hiyo iliendana na kucheza mechi za kirafiki za kimataifa ili kujiandaa na fainali hizi, ambazo awali zilitarajiwa kufanyika Cameroon.

Stars ilicheza mechi yake ya kwanza dhidi ya Misri, ambayo ilifungwa bao 1-0, halafu baadaye ikakutana na Zimbabwe, mchezo uliomalizika kwa sare ya 1-1, lakini ikimwacha beki, Erasto Nyoni akiumia na kuungana na Aggrey Moris ambaye aliumia katika mchezo dhidi ya wenyeji.

Taarifa kutoka katika idara ya matatibu wa timu hiyo, zimesema kuwa Moris hataweza kucheza mchezo wowote katika fainali hizi, lakini shirikisho likimwacha jijini hapa akiwa na wenzake ambao wanapeperusha bendera ya nchi.

Iliamua kucheza mechi dhidi ya Misri ili kujiandaa kuikabili Algeria, wakati mchezo wake wa pili wa kirafiki dhidi ya Zimbabwe ulilenga kujiimarisha zaidi na kutumia kurekebisha zaidi mapungufu yaliyopo.

**MAMBO MAGUMU AFCON**

Stars ambayo inavaa jezi ya rangi ya bluu ikiwa nyumbani na njano ikiwa ugenini, iko katika Kundi C pamoja na vigogo wawili, Senegal, Algeria pamoja na majirani zao kutoka Afrika Mashariki, Harambee Stars ya Kenya.

Katika kampeni ya kuwania taji hilo la Afcon, Stars ilianza kwa kupoteza mechi dhidi ya Senegal ambapo ilifungwa mabao 2-0 na mchezo wake wa pili ikakubali kichapo kingine cha 3-2 kutoka kwa Harambee Stars na kupoteza matumaini ya kusonga mbele katika mashindano haya.

Kutokana na matokeo hayo, Stars ambayo mara ya mwisho kucheza fainali hizi ilikuwa ni mwaka 1980, nahodha wa kikosi hicho akiwa Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leodegar Tenga, sasa kitashuka kwenye Uwanja wa Al Salaam leo usiku kucheza mechi ya kukamilisha ratiba dhidi ya Waarabu wa Senegal.

Katika mechi ya kwanza dhidi ya Senegal, Stars ilionekana kuanza kupoteza mechi hiyo kabla haijaingia uwanjani, na hiyo ilitokana na wachezaji wa kikosi cha kwanza ambao walipangwa na Kocha Amunike katika mchezo huo.

Licha ya kufahamu kwamba Senegal ina kiwango bora na ina wachezaji wenye uwezo wa juu kuliko Stars, lakini kikosi hicho kilishindwa kufurukuta na kucheza soka la kiwango cha chini kuliko ilivyotarajiwa.

Moja ya safu ambazo zilionekana kuwa dhaifu katika mchezo huo wa kwanza, ilikuwa ni idara ya kiungo, hali iliyosababisha washambuliaji wa timu hiyo wanaoongozwa na Mbwana Samatta kushindwa kufanya mashambulizi katika lango la wapinzani wao.

Hali hiyo ilifanya golikipa wa Senegal kukaa muda mrefu 'akisoma gazeti' kutokana na kukosa misukosuko kwenye lango lake, lakini pia safu ya ulinzi ikiwahi kuokoa mipira, pale ilipokuwa inaelekea upande wao.

Mambo yaliendelea kuwa mabaya zaidi pale Stars ilipowakabili majirani zao, Harambee Stars kwa kushindwa kulinda ushindi waliokuwa wanaupata.

Iliwachukua dakika tano, kupata bao la kuongoza kupitia mshambuliaji wake, Simon Msuva, lakini mabeki walishindwa kuzuia vema na matokeo yake Harambee Stars walisawazisha bao hilo na kuendelea kuongeza presha kwa wawakilishi wetu.

Stars ikaibuka tena na kupata bao la pili, ambalo liliwafanya waende mapumziko wakiwa mbele kwa mabao 2-1, lakini pia nao walishindwa kuulinda ushindi huo, na kuwapa Kenya nafasi nyingi ya kusawazisha bao hilo.

Tofauti na mechi ya kwanza ilivyokuwa, kwa tofauti ya ubora wa wachezaji wa Stars na Senegal, mchezo wa pili Stars ilionyesha wazi kwamba bado nyota wake wamekosa uzoefu na kufanya uamuzi wenye faida pale wanapokuwa na mpira kama ambavyo Kenya walikuwa wakifanya.

Stars walionekana kushindwa kutunza mipira kila walipokuwa nao, na kuruhusu wapinzani wao kuwapokonya, na hii ikawapa nafasi majirani zao hao kufanya mashambulizi ya mara kwa mara na hatimaye kufanikiwa kusawazisha mabao yote na kupata la tatu lililowapa ushindi.

Vijana hao wa Amunike pia walianza kupoteza muda kwa kujiangusha, huku pia golikipa Aishi Manula akitumia ujanja wa kuonyesha ameumia ili atibiwe, lakini lengo likiwa ni kutaka kupunguza mashambulizi.

**AMUNIKE KAULI TATA**

Kabla ya kuanza kwa mashindano haya ya 13, Amunike alisema kuwa amekiandaa kikosi chake kufanya vizuri katika fainali hizi, baada ya kufanikiwa kukata tiketi ya kushiriki.

Amunike alisema kuwa mpira wa sasa umebadilika, na hakuna timu inayoogopwa, lakini heshima kwa wapinzani wako haswa kama Senegal na Algeria ambao kiuhalisia wako mbali sana, ukilinganisha na Tanzania ambayo iko katika nafasi ya 131 kwenye viwango vya ubora vya Fifa.

Baada ya kupata kichapo kutoka kwa Harambee Stars, Amunike alisema kuwa kiukweli kikosi chake hakikuwa na uwezo wa kushindana katika fainali hizo.

Mnigeria huyo alisema kuwa timu yake inaundwa na wachezaji wengi wanaoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ambao ina klabu mbili za Simba na Yanga zinazoonyesha ushindani kwenye mechi zake, nyota wachache wanaocheza soka la kulipwa nje.

Alisema pia ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara imekuwa ni kikwazo kingine kwa Stars kufanya vibaya kwa sababu haitoi nafasi kwa kikosi hicho kupata muda wa kucheza mechi za kirafiki za kimataifa, ambazo kiufundi husaidia kuwaimarisha wachezaji waliopo na chipukizi walioitwa kwa mara ya kwanza kikosini humo.

**MATOKEO KUNDI C.**

| | | |
|---|---|---|
| Tanzania | 0 -2 | Senegal |
| Algeria | 2 -0 | Kenya |
| Senegal | 0 -1 | Algeria |
| Kenya | 3-2 | Tanzania |

**MECHI ZA LEO**

| | | |
|---|---|---|
| Tanzania | vs | Algeria |
| Kenya | vs | Senegal |

**NAJUA WAJUA**



TAIFA Stars ilikuwa timu ya kwanza kuwasili Misri kwenye michuano ya Afcon 2019 kati ya timu 24 zinazoshiriki mashindano hayo na imekuwa miongoni mwa timu za kwanza kuaga katika fainali hizo.

SOKA

# KWA NINI UTD IMELAMBA DUME KWA WAN-BISSAKA?



**MANCHESTER, England**

MUDA unakimbia na ukatili wa soka hauna kinga. Tukirudi nyuma hadi Januari 2018, beki wa pembeni, Aaron Wan-Bissaka alijikuta akifadhaika wakati kocha, Roy Hodgson alipokataa uhamisho wa mkopo kwa kinda huyo kwenda Ligi Daraja la Pili ili kujiimarisha zaidi kwenye soka la ushindani.

Na miezi 18 baadaye, sasa amekamilisha usajili wa pauni milioni 50 kwenda Manchester United, ambako hadi sasa, ameweka rekodi ya kuwa beki ghali zaidi katika historia ya klabu hiyo kipindi hiki cha majira ya joto.

Maisha yake yalibadilika haraka tangu majeraha ya Joel Ward na Martin Kelly na kumfanya akaaminiwa kikosini, alionyesha kiwango cha juu na kuwafanya washambuliaji wengi kwenye Ligi Kuu England kumzungumzia.

Alipewa zawadi ya kuongeza mkataba wake Aprili mwaka huu, na mzaliwa huyo wa Croydon jijini London, alionyesha kuaminiwa zaidi na timu yake na aling'ara msimu wa 2018/19.

Wan-Bissaka alicheza mechi 39, huku akianza katika mechi 35 kwenye ligi na kumfanya beki huyo wa kulia kuaminiwa mno na Hodgson. Palace walimaliza Ligi wakiwa nafasi ya 12, lakini walipitwa pointi nane na Wolves iliyopanda daraja na kumaliza nafasi ya saba na imefuzu kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

Uwezo wake wa kutumia vizuri mguu wake wa kulia dhidi ya timu kubwa za Ligi Kuu, ukamfanya kuwa mmoja wa mabeki bora wa kulia na hakukuwa na mshangao wakati Ole Gunnar Solskjaer na makocha wengine walipoanza kumfuatilia kwa karibu na kuisaka saini yake.

Mabingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich na wapinzani wao, Borussia Dortmund pia walikuwa kwenye mbio za kuwania saini yake, hasa wakichukulia mfano wa mafanikio aliyoyapata Muingereza, Jadon Sancho katika siku za hivi karibuni nchini Ujerumani. Wan-Bissaka amekuwa mvumilivu kuendelea kucheza soka kule Kusini mwa Jiji la London, lakini sasa anakwenda kuonyesha kipaji chake sehemu nyingine.

Lakini Wan-Bissaka, wakati wa utoto wake alikuwa shabiki mkubwa wa Man United na sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, yupo kwenye nafasi ya kwenda kuitumikia timu aliyoipenda kwa miaka mingi.

Ada ya pauni milioni 50 ni kubwa, hata kama soko la usajili hivi sasa kutokuwa la kueleweka. Lakini inawakilisha United, ambao wanalipa kwa ajili ya mchezaji wa daraja la juu na pia kwa mchezaji mwenye asili ya Uingereza, kitu ambacho kinaweza kutochukuliwa kwa umuhimu wake.

Kiwango chake kisichoshuka kitakuwa ni moja ya sababu ya kumfanya kuwa na uhakika wa kucheza kikosi cha kwanza, huku wapinzani wao wa mji mmoja, Manchester City wakiwa katika mbio moja za kuwania saini ya beki wa Leicester, Harry Maguire. Akiwa amecheza dakika 3,700 kwenye Ligi Kuu, hilo litamfanya kuwa na majaliwa ya kukaa muda mrefu zaidi pale Old Trafford.

Hata hivyo, usajili wake unaweza kuwa habari mbaya zaidi kwa kinda wa Ureno, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 21, ambaye alisajiliwa kwa pauni milioni 20 kipindi cha majira ya joto kilichopita chini ya zama za kocha Jose Mourinho. Lakini kucheza mechi 50 katika mashindano yote, sio jambo dogo kwake, kwani ana uhakika wa kuendelea kucheza. Aaron kiurahisi tu ana uzoefu zaidi, hivyo ushindani wa kwanza utakuwa mkubwa hasa Antonio Valencia akiwa anamaliza kipindi chake cha uchezaji klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto.

Takwimu zake zinazungumza zenyewe: akiwa na wastani wa kukaba 3.7, kuokoa mipira 3.7, kumiliki 2.4 na kupiga chenga 1.7, kwa mchezo mmoja alipokuwa Palace msimu wa 18/19. Takwimu hizi zinaweza kuonekana si za muhimu kwa sababu alicheza katika kikosi dhaifu, lakini hilo linaweza kupuuzwa. Kwa nini?

Naam, kwa sababu alikuwa na wakati mzuri zaidi kucheza dhidi ya timu kubwa na ni Wilfried Ndidi wa Leicester (Akikaba na kushinda mpira mara 143) na kiungo wa Everton, Idrissa Gueye (Mara 142) ambao walishindana kwenye kuwa na uwezo mkubwa wa kukaba na kunyang'anya mpira kushinda nyota huyo kwenye umri wa miaka 21 kwa msimu wa 129 ni 18/19: akitajwa kuwa mmoja wa mabeki wenye kiwango kizuri na cha juu zaidi cha kukaba kwenye Ligi Kuu ya England.

**KULINGANISHA, MIJADALA NA TAFAKARI JUU YA MAKOSA**

Kwa kawaida bei inayotajwa kununuliwa kwake Wan-Bissaka, na ikilinganishwa na umri wake tayari mijadala imeaanza kuibuka. Mfano wa Luke Shaw baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kule Southampton ni mmoja wao. Mabeki wa kati, Chris Smalling na Phil Jones ambao walitajwa kuchukua mikoba ya Ferdinand-Vidic, ni mfano mwingine.

Wote wakajikuta wakiishia katika njia tofauti: Shaw alivunjika mguu mwaka 2015, na nusuru akatwe na licha ya kuwa majeruhi kwa kipindi kirefu, akaimarika na kushinda tuzo ya mchezaji bora wa msimu wa klabu mwezi uliopita.

Smalling alicheza mechi 13 tu za ligi kabla ya uhamisho wake wa pauni milioni saba mwaka 2010, huku Jones akipaishwa mno na Sir Alex Ferguson kufuatia uhamisho wake wa pauni milioni 17 kwa Blackburn katika msimu uliofuata. Wachezaji hao walijikuta wakitumia muda mwingine kuwa benchi kutokana na majeruhi na walishindwa kutimiza kile kilichotarajiwa kutoka kwao. Umeona somo lake?

Moja ni Nemanja Vidic mwenyewe aliamua kujiondoa mwaka jana, majeraha yalimfanya kushindwa kuwa kwenye kiwango chake na kuendelea kucheza na hivyo safu ya ulinzi ikaongozwa na vijana. Historia hii haitakiwi kujirudia yenyewe.

Halafu utachoka ukimlinganisha Wan-Bissaka na beki chipukizi wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold, ambaye katika umri wake mdogo tayari ana taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kwa hiyo, anatakiwa kujimarisha kwa umakini mkubwa ili kuonyesha kwamba fedha zilizotumika hakupoteza bure.

Bila shaka ni kwamba, anaingia katika klabu ambayo ina matarajio makubwa mno na yeye na kwa uhakika anaweza kufanya kile ambacho wengine hawakukitarajia, lakini kucheza kwa kujituma kunaweza kumfanya aaminiwe kwa uzuri zaidi na Man United


**UAMUZI WA MWISHO**

United inalipa zaidi kwa kuangalia sura, lakini kwa upande mwingine wanaweza kuwa na wakati mzuri zaidi kwani wanaweza kumjenga zaidi kwa miaka mingi ijayo. Mapato ya Ligi Kuu ya England yanamaanisha kwamba klabu inahitaji zaidi, hivyo mchezaji anayetua pale anatakiwa kuonyesha thamani yake.

Mshahara wa pauni 80,000 kwa wiki kwa mchezaji mwenye umri wa miaka 21, ulionekana hauwezekani kwa miaka michache iliyopita, lakini kwa wakati huu ni bora zaidi kwa mchezaji husika kwa ajili ya kumpa morali zaidi.

Yote kwa yote, Man United wanaweza kuwa wamefanya uamuzi wa busara zaidi kumsajili, Wan-Bissaka ambaye atakuwa na matarajio makubwa zaidi pale Old Trafford.

NDANI YA 18



Jordan Pickford ni kipa wa kwanza katika historia ya kikosi cha England kuweza kudaka na kufunga penalti kwenye hatua ya matuta.

Nipashe **Spotika**



Kuongezeka kwa fedha za udhamini kwenye ligi hiyo pamoja na matangazo mengi na kuwa na mapato makubwa kwa klabu, maana yake timu zimekuwa na uwezo wa kutumia fedha za kutosha kusainisha wachezaji nyota duniani.

Uk. 16-17



ALISSON

# NYOTA 11 WENYE THAMANI KUBWA ZAIDI DUNIANI

**LONDON, England**

LIVERPOOL ilifurahia msimu bora wa 2018-19, wakiwa kwenye mbio moja na Manchester City kuwania ubingwa wa Ligi Kuu England kabla ya kuibukia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na matokeo yake thamani ya wachezaji wa kikosi chake imepanda na 'Wekundu' hao wa Anfield wana wachezaji wanne kwenye kikosi bora cha wachezaji 11 wenye thamani zaidi duniani msimu huu.

Lionel Messi alikuwa kwenye kiwango cha juu pale Barcelona kwa msimu wote, huku nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe na Neymar wakiwa kwenye safu ya washambuliaji watatu, maana yake ni kwamba hakuna nafasi kwa mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo.

Lakini nani mwingine ambaye yupo kwenye kikosi hicho? Soma makala haya...

**GOLIKIPA**
**Alisson - Liverpool (Euro Mil. 96)**

Wengi walishangaa wakati Liverpool ilipowalipa AS Roma pauni milioni 56 kwa ajili ya kumchukua golikipa huyo, na Alisson tangu alipotua pale Merseyside ameonyesha thamani yake.

Alisson alicheza katika kila mchezo wa Ligi Kuu, huku akifungwa mabao 22, wakati Liverpool wakimaliza nafasi ya pili nyuma ya Manchester City, huku akiwa kiungo muhimu kwenye ushindi wao wa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**MABEKI**
**Trent Alexander-Arnold - Liverpool (Euro Mil. 81)**

Mchezaji wao wa pili Liverpool kwenye kikosi hicho ni beki wa kulia, Trent Alexander-Arnold, ambaye alikuwa na wakati mwingine wa kuufurahia pale Anfield.

Wakati safu ya ulinzi ikiimarika zaidi, Alexander-Arnold kwa uhakika alijitambulisha mwenyewe duniani, kwa kutoa pasi za mwisho 16 katika mechi 40 alizocheza kwenye mashindano yote, na thamani yake kuwa ni euro milioni 81.

**Virgil van Dijk - Liverpool (Euro Mil. 98)**

Bila shaka alikuwa na kiwango bora zaidi msimu uliopita, akishinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu England (PFA), Van Dijk kwa uhakika ndiye alikuwa katikati ya mafanikio ya Liverpool msimu uliopita, baada ya vijogoo hao kulipa pauni milioni 75 wakati walipomsajili Januari mwaka 2018.

Van Dijk ndiye alikuwa akiongoza safu ya ulinzi ya Liverpool na pia alifunga mabao sita, na sasa thamani yake imeongezeka. Beki huyo wa zamani wa Celtic na Southampton pia aliiongoza Uholanzi kwenye fainali ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, ambapo walifungwa na Ureno.

**Raphael Varane - Real Madrid (Euro Mil. 86)**

Akitoka kuisaidia Ufaransa kushinda Kombe la Dunia, Raphael Varane hakuweza kuonyesha kiwango chake alichokionyesha kwenye timu ya taifa pale Real Madrid, ambayo ilikuwa kwenye msimu mgumu zaidi kwao.

Varane bado aliendelea kuonyesha ubora wake kwenye safu ya beki ya Madrid, licha ya msimu uliomaliza kuwa mgumu zaidi kwa Madrid, lakini bado amekuwa beki namba mbili mwenye thamani kubwa zaidi duniani.

**Andy Robertson - Liverpool (Euro Mil. 66)**

Machezaji wa nne wa Liverpool katika kikosi hiki ni Andy Robertson, ambaye kama beki mwenzake wa pembeni, Alexander-Arnold alikuwa na wakati mzuri zaidi kwa kikosi cha Jurgen Klopp kwa msimu wote uliopita.

Kucheza kwa kupanda kusukumiza mashambulizi mbele, ndio ilikuwa staili ya uchezaji ya Robertson na haikushangaza kumuona akiwa kwenye kikosi hiki, huku beki huyo wa kushoto wa Scotland akitoa pasi za mwisho 13 katika mechi 48 alizocheza kwenye mashindano yote.

**VIUNGO**
**Paul Pogba - Manchester United (Euro Mil. 127)**

Paul Pogba pengine anaweza kuwa kwenye shutuma nyingi kuhusu kiwango chake kwa sasa pale Manchester United, lakini shaka imebakia kama ataweza kubakia pale Old Trafford, ila hilo halijamzuia kuwa kwenye kikosi cha wachezaji wenye thamani kubwa duniani akiwa na thamani ya euro milioni 100.

Nyota huyu wa Ufaransa amefunga mabao 16 na kutoa pasi 11 kwenye mashindano yote kwa klabu yake msimu uliopita, huku Juventus na Real Madrid zikiripotiwa kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26.

**N'Golo Kante - Chelsea (Euro Mil. 90)**

Maurizio Sarri aliamua kumtumia N'Golo Kante kama kiungo mshambuliaji msimu uliopita pale Chelsea, ni wazi kwamba mabadiliko hayo ya namba hayakuwa na mafanikio kwani yeye anatajwa kama mmoja wa viungo mkabaji bora zaidi duniani na kumchezesha kama mshambuliaji ilikuwa ni kupoteza muda.

Yote kwa yote, Kante ana thamani kubwa, kwani ameingia katika kikosi hiki akiwa ameisaidia Chelsea kutwaa taji la Ligi ya Europa na maana yake kwamba kila msimu katika maisha yake hapo England amekuwa akitwaa taji.

**Kevin De Bruyne - Manchester City (Euro Mil. 120)**

Kiungo bora wa Manchester City hakuwa na msimu mzuri zaidi wa 2018-19, bado aliweza kuwa kiungo muhimu kwa kikosi cha Pep Guardiola wakati kikitwaa taji la Ligi Kuu.

De Bruyne alifunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho 10 katika mechi 32 alizocheza kwenye mashindano yote na alionyesha umuhimu wake wakati akitwaa taji la FA, wakati City wakiifunga Watford kwenye fainali.

**WASHAMBULIAJI**

Lionel Messi - Barcelona (Euro Mil. 190)

Messi anaonekana anaendelea kuwa bora. Nahodha huyo wa Barca ambaye alitimiza umri wa miaka 32 Jumatatu iliyopita, alifunga mabao 51 kwa Barcelona msimu uliopita, na kufikisha mabao 600 aliyoifungia klabu yake hiyo.

Hata hivyo, Messi ambaye aliiwezesha Barca kutetea taji la Ligi Kuu, alishindwa kuisaidia wakati inatolewa kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Liverpool kabla ya kufungwa na Valencia kwenye fainali ya Kombe la Mfalme (Copa del Rey).

**Kylian Mbappe - Paris Saint-Germain (Euro Mil. 225)**

Huyu ndiye mchezaji wa gharama kubwa zaidi katika kikosi hiki. Mbappe baada ya kufanya makubwa kwenye Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa alifunga jumla ya mabao 39 kwa Paris Saint-Germain msimu wa 2018-19, na hivi karibuni aliifungia Ufaransa bao lake la 100 kwenye mchezo wa kufuzu Euro 2020 dhidi ya Andorra.

Katika umri wake wa miaka 20, thamani ya Mbappe imekuwa ni zaidi ya euro milioni 200 na ana uhakika wa kuendelea kutamba kwa thamani yake kuwa juu zaidi.

**Neymar - Paris Saint-Germain (Euro Mil. 195)**

Uvumi umeenea kwamba, majaliwa ya Neymar pale Paris Saint-Germain, yapo shakani kwani anataka kurudi katika timu yake ya zamani ya Barcelona. Alitua PSG kwa pauni milioni 200 mwaka 2017.

Neymar anashika nafasi ya pili kwa kuwa mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi duniani.

**USILOLIJUA**



MECHI 12 Chelsea ilizoshinda kwenye Europa League msimu wa 2018-19, zinaifanya kushika nafasi ya pili kwa kushinda michezo mingi katika michuano mikubwa ya Uefa kwa msimu mmoja, ni Atletico Madrid pekee inayoizidi kufuatia kushinda mechi 13 msimu wa 2011-12.



## Kampuni yakabidhi gari la wagonjwa la mil. 76/-

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

KAMPUNI inayojihusisha na ununuzi wa kokoa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, Biolands, imekabidhi msaada wa gari la wagonjwa lenye thamani ya Sh. milioni 76 ili kukabiliana na changamoto ya usafiri na wagonjwa kupata huduma kwa wakati.

Akizungumza katika hafla fupi ya makabidhiano ya gari hilo hivi karibuni, Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya, Hunter Mwakifuna, alisema gari hilo lilipatikana kwa ubia baada ya kuanzishwa kwa mfuko wa afya wa jamii CHF na wadau ambao ni Biolands waliamua kutoa gari hilo ambalo lililokuwa chini ya usimamizi wa Health Insurance Management Services Organization (HIMSO) ambao walisimamia rasilimali watu na magari.

Hanta alisema baada ya kipindi cha HIMSO kutoa huduma ndani ya Halmashauri ya Kyela, kumalizika muda wake na kuhamia wilaya nyingine na tangu mwaka 2014 halmashauri iliomba gari hilo libaki na hatimaye kampuni hiyo iliridhia kukabidhi gari hiyo.

"Tunashukuru kampuni ya biolands na wabia wao HMSO kwa kukubali kutoa gari hili ambalo litakuwa maalum kubebea wagonjwa maeneo mbalimbali naamini changamoto ya huduma ya usafiri wa kubeba wagonjwa itapungua tunaomba mwendelee kutusaidia kwa sababu bado uhitaji ni mkubwa," alisema Mwakifuna.

Mwakilishi wa HIMSO, Deodat Madembwe, alisema kuwa shirika lao lilianza kufanya kazi na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kwa kushirikiana na Biolands tangu mwaka 2010 na hadi kufikia 2014 kampuni hiyo ilinunua gari hilo. Meneja uendeshaji wa kampuni ya ununuzi wa kokoa ya Biolands, Felix Mtawa, alisema walisaini mkataba na Bima ya Afya CHF tangu mwaka 2010 kwa ajili ya kuwasaidia wakulima na wateja wao ambao wanawauzia kokoa na kila mkulima alikatiwa bima ya afya na kampuni hiyo.

Mtawa alisema mradi huo ulikuwa wa miaka mitano ulianza mwaka 2010 na kumalizika 2014 ulizinufaisha familia zote kwa kufunguliwa bima za afya na kila kichwa kililipiwa Sh. 3,000.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2011/2012, jumla ya wagonjwa 18,000 walinufaika na mradi huo wa kuboresha afya na mradi ulipomalizika fedha zilizobaki walikubaliana kununua gari la wagonjwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia kitta, aliahidi kulitunza gari hilo kama ishara ya kutambua mchango wa Kampuni ya Biolands katika Sekta ya Afya.



Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa mtaalamu wa mafunzo Grady Kikoti wa Shirika la One Acre Fund Tanzania, wakati wa tukio la uvunaji wa mahindi katika shamba la mmoja wa wakulima wa kijiji cha Kitumbuka Anatas Kiwonde, Kata ya Irole wilayani Kilolo leo (jana). Shirika la One Acre Fund husaidia wakulima wadogo katika kilimo cha mahindi kwa kuwakopeshe pembejeo za kilimo ili waweze kuzalisha kwa tija. **PICHA: FRIDAY SIMABAYA**

## Wagonjwa wa ukoma walalamika kukosa matibabu

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WAGONJWA wenye ukoma ambao wanaishi Kijiji cha Ndubi, Kata ya Kisondela katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wamelalamikia kukosa huduma za matibabu kwenye Kituo cha Afya cha Kisa, hali inayosababisha ugonjwa huo kuendelea kusambaa na kusababisha ulemavu. Waliyasema hayo jana wakati wakipokea misaada ya vitu mbalimbali vilivyotolewa na wasamaria wema wanaounda kundi la Whatsapp la 'They Need Our Help' lenye lengo la kuwasaidia watu wenye mahitaji.

Juliana Kabajila, alisema mwaka 1985 alifika katika Kijiji cha Ndubi akitokea wilayani Kyela kupata huduma za matibabu ya ukoma katika Hospitali ya Makete, iliyoanzishwa na wakoloni ambayo ilikuwa maalum kwa ajili ya kutibu wenye matatizo hayo.

Alisema hospitali hiyo ilikusanya wagonjwa kutoka maeneo mbalimbali ikiwamo na nchi jirani ya Malawi kutibiwa ukoma na miaka ya 1990 Daktari bingwa wa ugonjwa huo alihamishwa hali iliyosababishwa huduma hiyo kudorora na hatimaye hospitali kufungwa.

Aliongeza kuwa baada ya hospitali kufungwa huduma za matibabu zilihamishiwa kwenye Kituo cha Afya cha Kisa, lakini kutokana na changamoto za wataalamu huduma zilisuasua.

Alidai tangu mwaka 2002 wagonjwa ambao walihamishia makazi yao kwenye Kijiji cha Ndubi, hawajawahi kupata huduma yoyote ya kutibu ugonjwa huo zaidi ya kuoshwa vidonda na dawa nyingine za kutuliza maumivu.

"Hakuna huduma yoyote ya matibabu tunayoipata katika kituo hiki cha afya zaidi ya kupewa dawa za kutuliza maumivu na kuoshwa vidonda, wakati mwingine tunalazimika kutumia gharama kufuata huduma hiyo katika Hospitali ya Wilaya ya Makandana changamoto ni kwamba hatuna fedha za kugharamia huduma za matibabu, lakini pia maisha yetu kwa sababu tuna ulemavu," alisema Juliana.

Richard Buja, alisema ugonjwa wa ukoma aliupata miaka ya 1986, lakini kutokana na ukata wa fedha hadi sasa unesababisha upofu wa macho yote mawili na mikono yote hivyo kushindwa kufanya kazi yoyote ya kuzalisha.

Alisema ugonjwa huo umekuwa pigo kwake kwa sababu amekuwa tegemezi wa kila kitu, hivyo anahitaji msaada wa vyakula na fedha ili kuendesha maisha yake aliongeza kuwa hata mkewe aliyekuwa anamuuguza naye amepata ugonjwa wa kupooza hivyo hana msaada wa karibu zaidi ya watoto ambao hufika kwa msimu.

Akizungumzia hali ya huduma za afya katika Kituo cha Afya cha Kisa, Mganga wa kituo hicho, Ireneus Mlelwa, alikiri kukosekana kwa huduma za matibabu kwa wagonjwa wa ukoma.

Alisema serikali haileti dawa zozote za kutibu ugonjwa huo badala yake huwatibu wagonjwa hao kwa kuwapa dawa za kutuliza maumivu.

"Tunaomba serikali ifanye utafiti upya wa ugonjwa wa ukoma katika kijiji hiki cha Ndula pamoja na maeneo mengine, itasaidia kujua idadi na namna ya kuwasaidia kuliko ilivyo sasa haitoi msaada wowote wa dawa kwa wagonjwa," alisema Mlelwa.

Alisema kituo hicho cha Kisa ni cha mtu binafsi kinahudumia wagonjwa takribani 30 katika kipindi cha miezi sita na kwamba wagonjwa wengine hushindwa kufika kwa sababu hawapati huduma stahiki.

## Mwekezaji Mbeya Textile apewa miezi 2 kuzalisha

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI ya Mkoa wa Mbeya imetoa muda wa miezi miwili kwa mwekezaji wa kilichokuwa Kiwanda cha Mbeya Textile, kuanza mara moja uzalishaji wa bidhaa nyingine kulingana na makubaliano ya mkataba vinginevyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa. Maagizo hayo yalitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipofanya ziara ya kukagua hatua iliyofikia ya ufungaji mitambo ya kiwanda kipya cha East Africa Starch Limited, ambacho kinatarajiwa kuanza kuzalisha bidhaa ya mafuta yanayotokana na mahindi, glukosi, chakula cha mifugo na unga.

Alisema kasi bado hairidhishi na kuutaka uongozi kuhakikisha ukamilishaji wa mitambo mipya unakamilika haraka ili bidhaa zianze kutengenezwa.


Aliongeza kuwa serikali iliitegemea kiwanda hicho mpaka sasa kiwe tayari kimeanza uzalishaji, lakini bado wanaendelea na ufungaji wa mitambo, aliwahimiza kuongeza kasi ili kuendana na makubaliano.

"Mpaka sasa bado wanaendelea kufunga mitambo ya kiwanda kipya cha East Africa Starch Limited ambacho kitazalisha bidhaa mbalimbali zitokanazo na mahindi kama vile ya mafuta yanayotokana na mahindi, glukosi, chakula cha mifugo na unga," alisema Chalamila.

Katika maelezo yake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema kiwanda hicho ambacho zamani kilikuwa kinazalisha nguo, lakini baadaye wakati wa ubinafsishaji alipewa mtu kwa ajili ya kuendeleza kiwanda kwa malengo ya kuzalisha nguo.

Alisema ulifika wakati zao la pamba ambalo lilikuwa linalimwa katika mikoa ya Mbeya na mikoa mingine liliingiwa na mdudu mwekundu hali iliyosababisha kukosekana kwa bidhaa hiyo, wakaomba kuhamisha mitambo Kanda ya Ziwa na mwaka 2011 waliomba kufunga mitambo ya kuzalisha bidhaa nyingine na taratibu zote zilifanyika.

Alisema kiwanda hicho kipya kinatarajiwa kuajiri watu zaidi ya 200 na kununua tani 40,000 hadi 45,000 za mahindi kila mwaka kwa lengo la kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na nafaka hiyo.





## TCCIA yaiombea gesi asilia Dodoma

Na Renatha Msungu, DODOMA

CHEMBA ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) imeiomba serikali kufikisha gesi asilia jijini Dodoma ili kusaidia viwanda vitakavyojengwa viweze kupata nishati ya uhakika na kwa bei nafuu. Akizungumza mwishoni mwa wiki katika Kongamano la Fursa za Uwekezaji mkoani Dodoma, Rais wa TCCIA, Octavian Mshiu, alisema gesi hiyo inapaswa kufikishwa Dodoma ili kusaidia viwanda ambavyo vinatarajiwa kujengwa, viweze kupata nishati ya uhakika wa kuendeshea shughuli zao.

"Serikali iangalie uwezekano wa kufikisha gesi asilia kwa haraka ili viwanda vinapokamilika viikute gesi asilia ipo tayari," alisema. Alibainisha kuwa Dodoma imekuwa Jiji na watu wanaongezeka, kwa hiyo gesi hiyo ikifika itakuwa rahisi kwa viwanda na shughuli nyingine zinazohitaji umeme. Pamoja na hayo, aliomba ujenzi wa bandari kavu jijini hapa uharakishwe ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo wakati ikisubiri kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa reli.

"Kadri siku zinavyozidi kusogea Dodoma itakuwa mji bora katika uwekezaji kama ilivyo miji mingine ya nje ya nchi na kuongeza kutokana na hilo Watanzania wanakila sababu ya kuchangamkia fursa zinatolewa na serikali kwa ajili ya kuleta maendeleo," alisema. Kadhalika, aliahidi kuwa chemba hiyo itaendelea kuimarisha ushirikiano na serikali ya awamu ya tano katika mipango yote ya maendeleo ili kuinua uchumi wa Taifa.

"Kama Rais John Magufuli alivyosema anapenda kuona uwezeshaji unaanzia ngazi ya chini, na sisi tunafanya hivyo ili kuinua sekta ya biashara ambayo ni muhimu kwa mmoja," alisema Mshiu.

Alisema pamoja na kuimarisha ushirikiano na serikali, katika kongamano lingine wanatarajia kuwaalika wafanyabiashara wengi kutoka nje kuja kuona fursa za uwekezaji kupitia makongamano mbalimbali yatakayoandaliwa.

# Chaula ataka wafanyakazi wa afya wawe wazalendo

Na Augusta Njoji, DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainab Chaula, amewataka watumishi wa afya nchini kufanya kazi kwa uzalendo na kuondokana na migogoro mahala pa kazi.

Dk. Chaula alitoa kauli hiyo juzi katika uzinduzi wa Baraza la kwanza la Taasisi ya Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini hapa.

Alisema kila mfanyakazi anawajibika katika majukumu aliyopewa kwa uadilifu na uaminifu.

"Tufanye kazi yetu kwa upendo licha ya kuwa ni ngumu, lakini tukiifanya kwa upendo, umoja na mshikamano itakuwa rahisi sana na tutakusanya baraka nyingi kutoka kwa tunaowahudumia, na tafsiri ya kazi yetu kuwa ya wito itathibitika," alisema.

Alibainisha kuwa kazi ya utabibu na udaktari inahitaji uvumilivu, huruma na maneno ya faraja kwa wagonjwa hivyo kila mmoja anatakiwa kuguswa pindi anapotoa huduma kwa mgonjwa.

"Kila mmoja akijituma atatimiza wajibu wake, mfano mzuri mimi mwenyewe sisubiri kutumwa napenda hekaheka hivyo napata shida ninapokutana na mtu anayesubiri kutumwa, maana ataona tu unamfuatilia," alisema.

Aliwataka kutekeleza majukumu yao na kutowakwaza wagonjwa.

Akizungumzia migogoro na majungu kazini, alisema kamwe huwa haileti tija katika utendaji bali inasababisha makwazo na kuifanya kazi kuwa ngumu zaidi.

Alisema ni lazima kila aliyepewa dhamana hasa viongozi kuhakikisha wanatenda haki na kuwajali watumishi waliochini yao pamoja na kuwatia moyo ili waweze kufanya kazi vyema.

Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) Mkoa wa Dodoma, John Mchenya, aliahidi kuwa wataendelea kuyafanyia kazi maelekezo yote muhimu yaliyotolewa.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi na Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema taasisi hiyo ina takriban miaka mitatu tangu ianzishwe na walikuwa hawajaunda Baraza la Wafanyakazi kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na idadi ndogo ya wafanyakazi.

Alisema kutokana na idadi hiyo kujitosheleza wameona kuwa na umuhimu wa kuwa na baraza hilo ili kushughulikia masuala ya wafanyakazi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akizungumza na mmoja wa watu 300 wenye ulemavu waliopokea vifaa saidizi vilivyotolewa na Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC Plc), huku baadhi ya viongozi waliohudhuria wakishuhudia. Kushoto ni Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa TCC Plc, Godson Killiza.

# TABOA yataka mjadala ukataji tiketi kwa kielektroniki

Na Ibrahim Joseph, DODOMA

SIKU chache baada ya serikali kutamka kuanza majaribio ya mfumo wa ukataji tiketi za mabasi ya mikoani kwa njia ya kielektroniki, Chama cha Wamiliki wa Mabasi ya abiria nchini (TABOA) kimeomba kufanyika majadiliano kati yao na serikali.

Hayo yalielezwa jana na Katibu wa Mkuu wa Chama hicho, Enea Mrutu, katika kikao cha wamiliki hao kilichofanyika jijini hapa.

Mrutu alisema wamiliki hao wanaona ni vyema kuwapo na kikao cha majadiliano kati ya Serikali na Taboa kwanza ili kuainisha changamoto zao.

"Tumejadili kwa kina kwenye kikao chetu jinsi mfumo huo na namna ya uendeshaji wake na kubaini yapo mapungufu ambayo yanahitaji majadiliano kati yetu na serikali," alisema. Alisema Taboa hawapingi kuwapo kwa majaribio hayo ya tiketi kwa njia ya kielektroniki ila kuwapo na majadiliano ambayo kila upande utanufaika.


Aidha, Mrutu alisema kabla ya kuanza kwa zoezi hilo pana hitajika elimu kwanza ili kuepuka wananchi kutapeliwa fedha zao na watu wasio waaminifu.

Naye, Mmiliki wa Mabasi ya Kampuni ya Jambo, Omari Chaka, alisema maeneo mengi hapa nchini hakuna uhakika wa mtandao jambo ambalo linaweza kusababisha wananchi kushindwa kupata huduma hiyo.

Chaka aliongeza kuwa lazima pawepo na majadiliano kuhusu matumizi ya mashine za kielektroniki zitakazotumika katika kukata tiketi. "Sambamba na utoaji elimu panahitajika mazungumzo ili ikitokea mtu amekosea katika kukata tiketi aweze kujua namna ya kurudishiwa fedha zake," alisema. Aliongeza "Tunapozungumza mitandao kuna wajanja wanaweza kuingilia wakawatapeli wananchi na matokeo yake tunajua lawama zitapelekwa kwa mmiliki wa chombo cha usafiri jambo ambalo si kweli." Hata hivyo alisema ukataji tiketi kwa njia ya kawaida ulikuwa unatoa ajira kwa watu wengi hivyo hilo nalo litazamwe kwa sababu litakosesha wengi ajira.

Hivi karibuni, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isaac Kamwelwe, alitangaza kuanza kutumia mfumo huo ambao pamoja na mambo mengine utakusanya taarifa zote muhimu kwenye sekta hiyo na kuondoa vitendo vya ulanguzi wa nauli kwa abiria.

Kamwelwe alisema mfumo huo ukikamilika utaondoa rasmi shughuli za wapigadebe na mawakala wa mabasi maeneo mbalimbali nchini.





Padri Eric Isdore Temba wa Parokia ya Mtakatifu Joseph mjini Zanzibar, akimpaka mafuta mtoto Dailan Temba wakati wa ubatizo wa mtoto kwenye sherehe ya wanajumuiya ya Mtakatifu Paulo ya Kidongo Chekundu Zanzibar jana. Kushoto ni msimamizi wa mtoto huyo. **PICHA: DONALD MARTIN KABEMBA**

# Diaspora wapania kujenga daraja Dar hadi Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) uko tayari kusimamia ujenzi wa daraja refu la kisasa lenye uwezo wa kuunganisha miji miwili ya Dar es Salaam hadi Zanzibar katika harakati za kuimarisha uchumi na mawasiliano.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo akiwa pia mjumbe wa kamati ya biashara Tanzania, Jonas Njao, akiiongoza timu ya wanajumuiya hiyo alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ofisini kwake Vuga Mjini Zanzibar.

Jonas alisema Diaspora imeanza harakati za maandalizi ya kufanya utaratibu wa kuziomba serikali zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Mapinduzi ya Zanzibar kuuridhia mradi huo mkubwa wa kimataifa utakaoweza kupunguza kundi kubwa la ajira nchini Tanzania.

Alisema wataalamu pamoja na wafadhili wa ujenzi wa mradi huo wa kiuchumi tayari wameshajitokeza na kinachosubiriwa kwao kwa sasa ni kukubalika kwa maombi ya mradi ambao bado umekuwa adimu ndani ya Bara la Afrika. Alieleza kuwa fursa wanazozipata za kuwasiliana na taasisi na kampuni wanazozunguka katika mataifa tofauti duniani zimelenga kutafuta nafasi za ajira zitakazosaidia kuimarisha ustawi wa wananchi kutokana na vijana wao kujikomboa katika masuala ya ajira.

Ofisa Mwandamizi wa kampuni ya Maxtruder ya nchini Ujerumani, Felix Von Lumburg, alisema uongozi wa taasisi yake uko tayari kuwekeza miradi ya ujenzi wa nyumba zenye bei nafuu kufuatia ushawishi mkubwa walioupata kutoka jumuiya ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi.

Kwa upande wake Balozi Iddi, alisema serikali zote mbili nchini Tanzania zimetoa fursa kwa wananchi wake kutafuta maisha mahali popote ilimradi wanazingatia sheria na taratibu za mataifa wanayoamua kuishi.

Balozi Iddi alisema ni vyema kwa Watanzania hao walioko ughaibuni wakachuma katika njia ya halali, wakala, lakini wasisahau kuweka akiba kwa ajili ya kusaidia familia zao pamoja na wao wenyewe.

Aliwaomba kuitumia fursa ya uwekezaji iliyopo nchini hivi sasa kwa kuanzisha miradi ya uzalishaji vikiwamo viwanda vidogo na vikubwa ili vije kuwasaidia pale watakapoamua kurudi kumaliza maisha yao nyumbani.

Vile vile, aliwahakikishia Watanzania wanaoishi ughaibuni kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa vile tayari imesharidhia uwepo wa jumuiya hiyo, iko tayari kuwasaidia wana-Diaspora hao kwa wale watakaoamua kuwekeza miradi yao ikiwamo nyumba na mashamba.

# Ahimiza wanawake kuipa ushindi wa kishindo CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Mjini Unguja, Asha Abdalla Juma, amewataka wanawake kuiamini, kulinda na kuipigania CCM na kuhakikisha inashinda kwa kishindo mwaka 2020 kuliko chaguzi zote zilizopita toka kuanzishwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992.

Alisema serikali ya awamu ya saba ya Zanzibar pamoja na serikali ya awamu ya tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini wa marais wake ambao ni Dk. Ali Mohamed Shein na Dk. John Magufuli, wamesimamia utekelezaji wa mambo mengi ya kimaendeleo yanayokidhi mahitaji ya wanawake na jamii nzima kwa ujumla.

Hayo aliyasema wakati akifungua kikao cha Baraza la Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Wilaya ya Amani kilichofanyika katika ofisi za wilaya hiyo Sebleni Amani Unguja.

Asha alieleza kwamba kupitia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015/2020, serikali imeimarisha huduma za afya, miundombinu ya barabara, umeme, elimu, mikopo kwa wanawake yenye masharti nafuu pamoja na kutoa fursa za uongozi kwa wanawake katika chama na serikali zote mbili.

Alisema kutokana na mambo mengi ya kimaendeleo yaliyotekelezwa nchini, wanawake wanatakiwa kuunganisha nguvu zao bila ya kujali tofauti za vyeo, rangi na kabila wahakikishe CCM inashinda kwa ngazi zote katika uchaguzi mkuu ujao kwa kuwa hiyo ndio njia pekee ya kuthamini kwa vitendo juhudi zinazofanywa na serikali.

Kupitia mkutano huo aliwasihi wajumbe wa mkutano huo kuendeleza umoja na mshikamano katika kutekeleza majukumu yao ya kisiasa ndani na nje ya UWT, kwa lengo la kuandaa mazingira rafiki ya kisiasa yatakayoimarisha CCM.

Aliwakumbusha wanawake hao kwamba pamoja na majukumu yao wanatakiwa kusimamia malezi ya watoto katika maadili mema na kuhakikisha wanalindwa dhidi ya vitendo vya udhalilishaji.

Akizungumzia suala la uimarishaji wa chama na jumuiya hiyo, alisisitiza umuhimu wa kuongeza wanachama wapya wenye sifa kisheria za kuipigia kura CCM kwa kila uchaguzi wa dola.

"Kila mwanachama kwa nafasi yake aanze kuwatafuta wapigakura wapya wa makundi yote wenye sifa za kupiga kura, waelezeni mazuri mengi yanayopatikana ndani ya CCM japokuwa mengi wanayaona na kuyatambua, lakini bado tuna jukumu la kuwakaribisha kwa ukarimu kwa kuwa CCM ni chama cha wote, nyumbani kumenoga," alisema.

Naye Katibu wa UWT wilaya hiyo, Asha Mzee Omar, akisoma taarifa ya utendaji wa kazi za UWT, alisema viongozi, watendaji na wanachama wanashirikiana vizuri huku wakijipanga kukabiliana na dalili zozote za upinzani ili CCM ishinde katika uchaguzi ujao.

# Serikali yatenga bil. 4/- kukopesha vijana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Iddi, amesema wakati serikali inatarajia kufanya marekebisho ya mishahara kwa wafanyakazi wake wenye uzoefu na makundi mengine ambayo hayakunufaika na nyongeza za mishahara iliyopita, Sh. bilioni nne zimetengwa kwa lengo la kuwapatia mikopo vijana ili waweze kujiajiri.

Alisema pia Serikali ya Abudhabi, kupitia Mfuko wa Khalifa (Khalifa Fund) itatoa Sh. bilioni 23 kwa Zanzibar kwa ajili ya kusaidia tatizo la ajira kwa vijana wa Zanzibar.

Akifunga mkutano wa 14 wa Baraza la tisa la Wawakilishi lililojadili Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020, alisema kupatikana kwa fedha hizo kunatokana na ziara aliyoifanya Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, katika nchi za Falme za Kiarabu mwishoni mwa mwaka jana.

Alieleza katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pia baadaye itaongeza kiasi kama hicho kitakachotolewa na Mfuko wa Khalifa wa Abudhabi ili kusaidia miradi ya vijana nchini. Alisema serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha vijana wake wanapata ajira, ikielewa ukubwa wa tatizo hilo ambalo ni changamoto ya dunia ikiwamo Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Balozi Iddi alitoa wito kwa vijana hasa wanaomaliza vyuo vikuu na elimu ya sekondari kujikusanya pamoja katika kubuni au kutafuta mradi wa kufanya ili kuitumia vyema fursa iliyopo.

Akizungumzia suala la ardhi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Iddi aliwaomba watendaji wote waliopewa dhamana ya usimamizi wa Sheria za Ardhi wawe wazalendo kwa kutumia taaluma zao ili kutatua migogoro ya ardhi iliyopo kuanzia shehia, wilaya, mikoa hadi taifa kwa ujumla.

Alisema Zanzibar kwa sasa ina sheria tisa zinazohusiana na matumizi bora na endelevu ya ardhi, lakini bado kumejitokeza baadhi ya viongozi, watendaji wa serikali na wananchi kuendelea kutoziheshimu sheria hizo.

Balozi Iddi alisema wahusika hao wamekuwa na tabia ya kuwa madalali wa kuuza au kuchukua ardhi bila ya kufuata sheria na taratibu zilizopo hali inayosababisha dhuluma na migogoro mingi katika jamii.

Aliwaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wote wa Zanzibar kutambua kwamba ardhi ni rasilimali muhimu katika maendeleo ya taifa kwa wananchi wake kiuchumi na kijamii.

Alieleza kwamba Serikali Kuu inatambua kuwa wapo baadhi ya wanaojiita wawekezaji wa kizalendo wanaoomba na kupewa ardhi na badala yake huitumia kwa kuinadi sokoni na kuiuza kwa fedha nyingi za kigeni jambo halikubaliki na dola haitasita kuwanyang'anya ardhi wale watakaobainika kuendeleza vitendo hivyo viovu vinavyohujumu uchumi.

Alisema hatua mbalimbali zitaendelea kuchukuliwa na serikali katika kupunguza au kuondoa kabisa migogoro ya ardhi ikiwamo kuimarisha Mahakama ya Ardhi nchini pamoja na kuendeleza hatua ya maandalizi ya upimaji wa miji mipya Unguja na Pemba.

## Tigo mdhamini tena mawasiliano Sabasaba

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo kwa mara ya nne mfululizo imekuwa mdhamini rasmi wa mawasiliano kwenye maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam maarufu kama Sabasaba ambayo huandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade).

Maonyesho ya Sabasaba yalianza Juni 28 hadi Julai 8, mwaka huu, yakiwa na kauli mbiu 'Usindikaji wa Mazao ya Kilimo kwa Maendeleo Endelevu'.

Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, alisema, Tigo imekuwa ikidhamini maonyesho hayo kwa miaka minne mfululizo kwenye eneo la mawasiliano na kuongeza kuwa udhamini huo pia unalenga kuunga mkono jitihada za serikali za kukuza biashara na kukuza viwanda vya ndani kwa ajili ya ukuwaji wa uchumi. Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano kwa Umma na Mawasiliano wa Tan-Trade, Theresia Chilambo, aliishukuru kampuni ya Tigo kwa kudhamini maonyesho hayo kwa mara ya nne.

Theresia alisema, Tan-Trade inayo furaha kuwa na mshirika wa kuaminika kwenye sekta ya mawasiliano na kuongeza kuwa mamlaka hiyo inasubiria kwa hamu ushiriki wa Tigo katika maonyesho hayo ya kimataifa.

Pamoja na udhamini huo, Tigo pia imeungana na kampuni sita za kutengeneza simu kutoa ofa za kipekee kwa data pamoja na simu janja kwa maelfu ya wateja wao wataokuwa wanashiriki maonyesho hayo jijini Dar es Salaam. "Wakati tunaingia msimu mwingine wa kusisimua wa Sabasaba, tumeandaa ofa nzuri za data pamoja na simu janja kwa ajili ya wateja wetu. Tunashirikiana na Infinix, Itel, Nokia, Samsung, TECNO Mobile na KaiOS kuwapa wateja wetu siyo tu chaguo pana la huduma mbalimbali bali pia aina mbalimbali za simu janja na data ambavyo vinakidhi mahitaji yao," alisema Woinde.

Aliongeza: "Wateja wetu wataweza kupata ofa za kuvutia ikiwa ni pamoja na simu janja za gharama nafuu ambazo zitapatikana kwa kuanzia Sh. 74,900 zikiwa na GB 96 za intaneti zinazoweza kutumika kwa kipindi cha mwaka mmoja. Tigo pia itakuwa na promosheni maalum kwa ajili ya wateja wa Tigo Pesa pamoja na wateja watakaosajili laini zao kwa utaratibu mpya wa alama za vidole."

Akifafanua zaidi Woinde alisema, wateja wapya wa Tigo Pesa kipindi cha Sabasaba wataweza kutuma pesa (Tigo kwenda Tigo) pasipo makato kwa kipindi cha miezi 3 na kuongeza kuwa mteja atakayejisajili kwa kutumia utaratibu mpya wa alama za vidole atazawadiwa dakika 100 za bure kutoka Tigo. Kwa mujibu wa Woinde, Tigo imejiandaa kikamilifu kutoa ofa mbalimbali ikiwamo data, simu janja, huduma za kifedha pamoja na huduma kwa ajili ya biashara ndogo, kubwa na za kati ikiwa ni jitihada za kuhamasisha maisha ya kidijitali ambayo yataongeza matumizi ya simu janja na matumizi ya data pamoja na mtandao wenye kasi wa 4G.

# Makamu Rais wa Shell asifu mazungumzo na mawaziri

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAKAMU wa Rais wa Kampuni ya Mafuta ya Shell, Clare Harris, amesema kuwa amefurahishwa na matokeo ya mikutano yake na mawaziri watatu juu ya mradi mkubwa wa gesi asilia (Tanzania LNG Project) unaoandaliwa hapa nchini.

Kiongozi huyo alifanya mazungumzo na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, Waziri wa Sheria na Katiba, Dk. Augustine Mahiga na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dk. Hamis Mwinyimvua. Harris amesema: "Nimefurahi kutembelea tena Tanzania na kukutana na viongozi wa juu wa Serikali ya Tanzania. Mradi huu ni muhimu kwa Shell na kwa Tanzania na utachangia vikubwa azma ya serikali ya kulifanya

taifa hili kuwa na uchumi wa kati na wa viwanda na pia kuchangia juhudi ya kuleta mageuzi ya kiuchumi. Hakutoa maelezo zaidi juu ya mazungumzo yao." Lakini kiongozi mmoja wa Shell amefafanua kuwa Harris anaongoza idara muhimu ya (Integrated Gas Ventures) katika kampuni ya Shell ambayo ndiyo husimamia miradi ya LNG duniani kote.

Ameeleza kuwa Harris amekuja wakati muhimu kwani Shell na wabia wake Ophir Energy na Pavillion Energy wamekuwa na mazungumzo ya kimkakati na serikali ya Tanzania yanayoitwa "Host Government Agreement [HGA] Term Sheet" toka Aprili mwaka huu.

"Kukamilika kwa mazungumzo haya na kutia saini mkataba huu itakuwa ni hatua muhimu kuelekea ujenzi na ukamilishaji wa mradi huu wa LNG.

Mradi huu unatarajiwa kuwa ndiyo mradi mkubwa kiuwekezaji katika historia ya Tanzania ambao utatekelezwa kwa dola za Marekani bilioni 30."

Alisema Shell inaichukulia Tanzania kuwa ni soko muhimu katika Afrika.




Mmoja wa washindi wa shindano lililoandaliwa na Mantrac Tanzania lijulikanalo kama 'The Operator Challenge' ikiwa ni sehemu ya mafunzo ya siku tatu kwa waendeshaji wa makatapila, Samwel Leonard (kushoto), akipokea zawadi yake kutoka kwa mkufunzi kutoka Kampuni ya Mantrac, Ehab Abdelfatah Mohamed. **MPIGAPICHA WETU**

# Wahamasishwa vyakula vyenye lishe

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WAKAZI wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wameshauriwa kuwa na utamaduni wa kula mboga za majani na matunda kwa wingi kuongeza vitamini, ili kuepukana na magonjwa.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Victoria Ngatunga, alipokuwa akisona taarifa ya hali ya lishe katika robo ya tatu kwenye kikao cha kamati ya lishe.

Alisema bado baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Masasi hawajawa na mwamko wa kupenda kula vyakula vya asili hasa mboga za majani pamoja na matunda, hivyo kutokana na hilo kumekuwa na matatizo mengi ya kiafya ikiwamo lishe duni kwa jamii.

Alisema mlo kamili unaundwa na makundi manne ya vyakula ambayo ni wanga, protini, vitamin na mafuta, na kwamba vyakula vya wanga vinavyotokana na nafaka ni kama ugali, wali, ndizi zilizopikwa na viazi, vyakula vyenye protini ni nyama, mayai, samaki, maharage na maziwa.

Alisema Wilaya ya Masasi ni miongoni mwa wilaya ambazo zimejaliwa kuwa na mboga za majani kwa wingi na bei zake ni nafuu.

"Tunakula chakula kwa kuzingatia virutubisho vinavyohitajika mwilini... virutubisho hivyo vinakuwa na uwiano sahihi wa virutubisho vyote muhimu katika chakula ambavyo vinaitwa mlo kamili navyo ni protini, mafuta na wanga hivyo tupende kula mboga za majani," alisema Ngatunga.

Naye mjumbe mmoja wa kikao hicho ambaye pia ni Katibu wa Bakwata Wilaya ya Masasi, Shekh Hamisi Baina, alisema mboga za majani zinauzwa kwa bei ya chini, lakini wananchi wamekuwa na uwelewa mdogo juu ya umuhimu wa kula mboga hizo pamoja matunda, hivyo kusababisha baadhi yao kuwa na lishe duni.

"Sisi kama viongozi wa dini na wadau wengine tushirikiane kwa pamoja kuhamasisha wananchi wetu kula vyakula vinavyozingatia mlo kamili ikiwamo hizi mboga za majani na matunda ili kujenga afya bora hatimaye kuweza kuondokana na kukabiliwa na magonjwa yanayotokana na lishe duni," alisema Shekh Baina.

## Trump, Kim uso kwa uso

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amekutana na kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un katika eneo lisilo la kijeshi la mpakani, kwamba viongozi hao wawili walipeana mikono kuonyesha ishara ya matumaini ya amani.

Rais Trump na Kim Jong Un wamekubaliana kuanzisha tena mazungumzo ya nyuklia yaliyokwama.

Mojawapo ya makubaliano ni nchi zote kuanzisha vikosi kazi, kwa upande wa Marekani utaongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo.

Rais Trump hakutoa maelezo zaidi kuhusu masuala yatakayojadiliwa, lakini ameeleza wazi kwamba vikwazo dhidi ya Korea Kaskazini vitaendelea kubaki kwa muda.

Marekani imeitaka Korea Kaskazini isimamishe mpango wake wa kutengeneza nyuklia. Korea Kusini na Marekani pia wanahimiza upatikane mkataba rasmi wa amani kati ya Korea Kusini na Kaskazini.

Kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis amepongeza hatua ya viongozi hao kukutana kwa kueleza kuwa hatua hiyo itawezesha kupatikana kwa amani.

Ni mara ya tatu kwa viongozi hao wawili kukutana katika kipindi cha mwaka mmoja. Kukutana kwa viongozi hao kumeongeza matumaini ya kuyarejesha mezani mazungumzo ya nyuklia yaliokwama.

Rais Trump aliandamana na Kim kuvuka eneo hilo la mpaka lisilo la kijeshi na ambalo kwa miaka kadhaa limekuwa katika fukuto la vita baridi.

Rais Trump ndiye Rais wa kwanza wa Marekani kufika eneo hilo la upande wa ardhi ya Korea Kaskazini.

Baada ya mazungumzo ya takribani dakika 50, Rais Trump na Kim walirejea upande wa Korea Kusini na kuungana na Rais Moon Jae-in kwa mazungumzo mafupi. Baadaye Rais Trump na Kim walifanya mazungumzo ya faragha.

Rais Trump alikutana na wanajeshi wa Marekani katika kambi ya wanahewa ya Osan iliyoko kusini mwa Mji Mkuu wa Korea Kusini, Seoul.

Hatua hiyo ndio ilikamilisha safari yake ya barani Asia na kisha kurudi Washington.

Rais Trump aliwasili Korea Kusini juzi jioni kwa ajili ya mazungumzo na Moon baada ya kuhudhuria mkutano wa kilele wa mataifa 20 unaoendelea jijini Osaka, Japan, ambapo alifanya ziara ya kushtukiza na kutoa wito wa kutaka kuonana na kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un.

**DW**



Rais wa Marekani, Donald Trump (kushoto), akiwa na Mwanamfalme wa Saudi Arabia, Mohammed bin Salman. **PICHA: REUTERS.**

# Trump ammwagia sifa mwana mfalme kwa kuleta mageuzi

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amempongeza mwana mfalme wa Saudi Arabia, Mohammed bin Salman walipokutana katika kikao cha mkutano wa Kundi la Mataifa 20 nchini Japan, akieleza kuwa ni rafiki yake ambaye amefanya mambo makubwa.

Rais Trump alisema juzi kuwa anaridhika na kitendo cha Saudi Arabia kununua vifaa vya kivita vinavyotengenezwa na Marekani na kusema kuwa mwana mfalme amejitahidi kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii katika nchi yake.

Kwenye mkutano huo Rais Trump alisita kujibu swali kutoka kwa waandishi wa habari, alipoulizwa iwapo ataibua sakata la mauaji ya mwandishi wa Saudi Arabia, Jamal Khashoggi yaliyotokea mwaka 2018.

Mwana mfalme huyo wa Saudi Arabia ameendelea kukabiliwa na uchunguzi wa kimataifa tangu kuuawa kwa Khashoggi katika ubalozi mdogo wa Ufalme wa Saudi Arabia mjini Instanbul mwaka 2018.

Kufuatia mazungumzo ya pamoja kati ya viongozi hao wawili Jumamosi, Ikulu ya Marekani imesema mkutano wa viongozi hao ulikuwa na tija, pia walizungumzia tishio linaloongezeka la Iran, ulazima wa kuhakikisha utulivu katika soko la mafuta la kimataifa na umuhimu wa masuala ya haki za binadamu.

Rais Trump pia anatarajia kukutana na Rais wa China, Xi Jinping ili kujaribu kuanzisha mazungumzo ya kibiashara tena kati ya nchi hizo yaliyovunjika mwezi uliopita.

Rais Trump alipoulizwa na Shirika la Habari la VOA wakati alipofanya mkutano na Rais wa Brazil, Jair Bolsonaro iwapo anatarajia Xi kuja na pendekezo la makubaliano ya kibiashara watakapokutana, alijibu: "Tutaona nini kitatokea kesho. Itakuwa ni siku yenye hamasa, na hakika, kwa watu wengi na dunia nzima... nimatumaini yangu matokeo ya mkutano yatakuwa na manufaa kwa nchi zote mbili na yataweza kutekelezeka."

**VOA**

# Watu 200 wakamatwa Ethiopia kwa kupanga mapinduzi

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

VYOMBO vya usalama nchini Ethiopia vimewakamata watu zaidi ya 200 wakiwamo raia, wanausalama na wanasiasa wanaotuhumiwa kuhusika katika jaribio la mapinduzi kwenye Jimbo la Amhara, ambako rais wa eneo hilo na mnadhimu wa jeshi waliuawa.

Mashambulizi yaliyotokea mwishoni mwa juma lililopita nchini Ethiopia yamezidisha shinikizo zaidi kwa utawala wa Waziri Mkuu, Abiy Ahmed ambaye ameendelea kukabiliana na changamoto za machafuko ya kikabila na mabadiliko ya uchumi wa taifa hilo.

Machafuko hayo ambayo serikali inasema yalikuwa sehemu ya njama iliyofanywa na Jenerali mmoja muasi na wanajeshi wake kuchukua udhibiti wa Amhara, yalidhihirisha namna mivutano ya kikabila inavyotishia ajenda ya mageuzi ya Waziri Mkuu Ahmed.

Waziri Mkuu Ahmed (42), amepata sifa kutoka mataifa mbalimbali duniani kwa hatua ya kuboresha maridhiano nchini Ethiopia, lakini wachambuzi wanasema mabadiliko ya kasi aliyoyafanya yamezusha hali ya sintofahamu na ukosefu wa usalama.

Hadi sasa tayari watu sita wamefikishwa mahakamani kwenye Mji Mkuu wa Ethiopia, Addis Ababa na kushtakiwa kwa makosa ya ugaidi kuhusiana na jaribio la mapinduzi ya serikali ya Jimbo la Amhara.

Katika vurugu zilizotokea mwishoni mwa juma lililopita, kinara anayetuhumiwa kuandaa jaribio hilo, Brigedia Jenerali Asaminew Tsige nae aliuawa na vyombo vya usalama.

Mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yameikumba Amhara na miji mingine miaka ya hivi karibuni.

Tangu uchaguzi wa mwaka jana, Waziri Mkuu Abiy amekua akipambana kumaliza mvutano wa kisiasa kwa kuwaachia huru wafungwa wa kisiasa, kuondoa makatazo dhidi ya vyama vya kisiasa na kuwashtaki maofisa wanaoshutumiwa kukiuka haki za binadamu.

**RFI**

# Hofu yatawala Tunis baada ya milipuko kutokea

**TUNIS, Tunisia**

WAZIRI Mkuu wa Tunisia, Youssef Chahed, amekashifu mashambulizi mawili ya bomu yaliyotokea mjini Tunis, akiyataja mashambulizi hayo kama ya kutengeneza hofu kwa wananchi.

Kauli hiyo imekuja wakati Kundi la Islamic State likijinasibu kuhusika na mashambulizi mawili tofauti yaliyosababisha kifo cha askari na kuwajeruhi raia kadhaa.

Habib ni mfanyakazi wa benki ambaye alinusurika katika mashambulio alisema yanatokea ikiwa imesalia miezi michache kabla ya uchaguzi mkuu wa rais na wabunge.

Hayo yanajiri wakati Rais wa nchi hiyo, Beji Caid Essebsi, akiwa amelazwa hospitalini baada ya kuugua.

Waziri Mkuu Youssef Chahed alieleza kuwa serikali inafanya kila inachowezesha kumpa huduma nzuri rais huyo.

Hata hivyo, bado haijafahamika ni ugonjwa gani unamsumbua rais huyo, lakini serikali imelazimika kutoa taarifa hiyo baada ya uvumi kuwa rais huyo alikuwa amefariki dunia.

**RFI**

# Mtoto anusurika kuuawa Dar akidhaniwa ni mchawi

**Beatrice Moses**

MTOTO wa kiume anayetajwa kuwa na matatizo ya akili mwenye umri wa miaka 8 amenusurika kuuawa na wananchi wenye hasira akidhaniwa kuwa ni mchawi.

Mtoto huyo jina linahifadhiwa, alikutwa akiwa mlangoni mwa nyumba ya mkazi wa Makondeko Temboni Kata ya Saranga, wilayani Ubungo jijini Dar es Salaam, huku akiwa uchi usiku wa manane.

Taharuki ilizuka juzi saa 9 usiku baada ya Agness Miyeji kueleza kuwa alishtuka baada ya kusikia sauti ya paka akilia katika hali iliyomshangaza, hivyo akamwamsha mumewe wakaanza kusali.

"Ajabu ikatokea wakati tunasali ile sauti ikawa inazidi kusikika kama inafuata kwenye mlango, ndipo mume wangu akalazimika kwenye kufungua mlango ndipo tukamkuta mtoto wa kiume akiwa uchi kasimama mlangoni," alisema mama huyo.

Alieleza kuwa kitendo hicho kiliwapa hofu wakaamsha baadhi ya majirani, kisha wakashauriana kwenda kwa mjumbe wa eneo lao liitwalo Makondodeko, ambapo pia waliona kaptula wakamvalisha mtoto huyo.

"Mjumbe aliwasiliana na polisi jamii wa Saranga ambapo walifika hata hivyo, mtoto hakuweza kujieleza chochote kila alipohojiwa alikuwa kama vile anaweweseka tu, wakawasiliana na viongozi wa msikiti jirani ili watangaze kama mtu kapotelewa na mtoto ambaye alichukuliwa na kwenda kuhifadhiwa kwenye ofisi ya ulinzi shirikishi Saranga," alisema.

Hata hivyo mama wa mtoto huyo (Ester Hurra) alifika kwenye ofisi hiyo akiwa ameongozana na baadhi ya jirani zake ambapo baada ya kuhojiwa na polisi jamii alieleza kuwa mwanaye ana matatizo ya akili anatibiwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

"Nilikwenda kwenye mkesha kwenye kanisa la Sabato liilopo jirani na nyumbani kwangu nilimwacha mwanangu amelala na kaka zake, lakini niliporejea saa 11 alfajili sikumkuta, kaka zake walikuwa wamelala fofofo," alisema mama wa mtoto huyo.

Alibainisha kuwa hali hiyo ilimtisha akawaamsha na kuwahoji hakuna aliyejua mtoto amekwenda wapi, ndipo akawashirikisha wenzake aliokuwa ameongozana nao kutoka kwenye mkesha wakaanza kumtafuta kwa kuuliza kwa majirani, lakini hakuna aliyekuwa amemuona.

Kutokana na taarifa za kukutwa akiwa mtupu polisi jamii walishauriwa mtoto huyo kuchunguzwa na mzazi ili kujiridhisha kama hajafanyiwa vitendo vya kikatili ikiwamo kulawitiwa, ilithibitika kuwa yu salama.



Ofisa Bima wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Robert Ndaweka (kushoto), akitoa elimu ya bima kwa wakazi wa Dar es Salaam waliotembelea banda la shirika hilo mwishoni mwa wiki kwenye maonyesho ya 43 ya Sabasaba yanayoendelea jijini Dar es Salaam Viwanja vya Mwalimu Nyerere Barabara ya Kilwa. Wa pili kushoto ni Ofisa Bima, Athuman Imary.

## 'Serikali haijazuia utafiti mbegu za GMO'

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

SERIKALI imesema utafiti kuhusu mbegu za Teknolojia ya Uhandisi Jeni (GMO), haujawahi kuzuiwa wala kuchoma moto majaribio yake yanayofanyika hapa nchini bali unaendelea kufanyika kwa baraka zote za serikali na utakapokamilika maamuzi yatatolewa.

Majaribio ya utafiti wa mbegu za GMO yanafanyika katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo cha Makutupora kilichopo mkoani Dodoma, kuhusu mbegu za mahindi na Taasisi ya Utafiti Mikocheni iliyopo jijini Dar es Salaam, kuhusu mbegu za mihogo.

Kauli ya serikali ya kuendelea na utafiti wa mbegu za GMO imekuja ikiwa takribani miezi minne iliyopita kufuatia Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Mhandisi Mathew Mtigimwa, kueleza uamuzi wa serikali kusitisha utafiti huo unaofanyika katika taasisi hizo mbili za utafiti.

Akizungumza katika mjadala wa wazi wa siasa za uchumi wa GMO kwa Tanzania uliofanyika katika ukumbi wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mratibu wa Utafiti wa Bioteknolojia za kilimo Tanzania kutoka Taasisi ya Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Fred Tairo, alisema kwa sasa utafiti huo unaendelea na upo katika hatua mbalimbali katika vituo hivyo.

Alisema TARI haijaacha kufanya utafiti wa GMO tangu ilivyoanza na unaendelea na umeonyesha matokeo chanya kwa mbegu zote mbili.

Dk. Tairo, alisema watu pamoja na vyombo vya habari nchini walielewa vibaya kuhusu taarifa zilizotolewa na kwamba serikali ilitaka watafiti wafuate utaratibu wa kutoa matokeo waliyokuwa wanayapata kwenye majaribio hayo ili kuondoa mkanganyiko.

Mtafiti huyo alisema msimamo wa serikali ni kuendelea na utafiti wa GMO ili uweze kukamilika katika hatua zake muhimu na kisha utakapokamilika utapeleka katika mamlaka husika kwa ajili ya kutoa maamuzi.

Akizungumzia kuhusu utafiti huo katika Taasisi ya Utafiti ya Makutupora, alisema umelenga kutafuta ufumbuzi wa changamoto ya ukame na bunguaji wa mahindi na matokeo ya awali yameonyesha kufanikiwa kupambana na viwavi jeshi vamizi.

# Umaskini bado tishio vijijini, Rukwa kinara

INATOKA UK. 3

(7.7), Singida (9.3), Tabora (11.1), Rukwa (19.8), Kigoma (14.2), Shinyanga (8.2), Kagera (12), Mwanza (9.4), Mara (2.2), Manyara (8), Njombe (3.3), Katavi (9.2), Simiyu (7.5), Geita (14.5) na Songwe (5.6).

**Mgawanyo wa Watu Maskini**

Kadhalika, mgawanyo wa watu maskini Tanzania Bara kwa kuzingatia umaskini wa mahitaji ya msingi kwa mwaka 2017/18, unaonyesha kuwa asilimia 81 ya watu maskini wanaishi maeneo ya vijijini ikilinganishwa na asilimia 84.1 mwaka 2011/12.

Maeneo mengine ya mijini, mgawanyo wa watu maskini ni asilimia 16.1 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 14.4 mwaka 2011/12.

Aidha, asilimia 3.0 ya watu maskini wanaishi katika Jiji la Dar es Salaam ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2011/12.

Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam kiwango cha watu maskini kimeongezeka mara mbili.

**Kina cha Umaskini**

Matokeo ya Utafiti yanaonyesha kuwa wastani wa kina cha umaskini wa mahitaji ya msingi katika ngazi ya Taifa ni asilimia 6.2 na wastani wa kina cha umaskini wa mahitaji ya chakula ni asilimia 1.4.

Kina cha umaskini kimeonekana kuwa kikubwa katika maeneo ya vijijini kwa asilimia 7.4 ikilinganishwa na maeneo ya mijini kwa asilimia 3.5.

Aidha, kina cha umaskini kwa kuzingatia tofauti ya kipato kati ya watu maskini kimeonekana kuwa na asilimia 2.1 kitaifa ambapo maeneo ya vijijini kimekuwa kikubwa kwa asilimia 2.6 kuliko maeneo ya mijini asilimia 1.2.

Umaskini wa Watoto

Vile vile, umaskini wa mahitaji ya msingi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 - 17 ni asilimia 30.1 huku wa chakula ni asilimia 9.4 .

Hata hivyo, umaskini wa mahitaji kwa watoto umeonekana kuwa mkubwa katika maeneo ya vijijini kwa asilimia 34.5 ikilinganishwa na maeneo ya mijini kwa asilimia 11.0.

Kwa upande wa chakula kwa watoto wanaoishi maeneo ya vijijini umeonekana kuwa asilimia 11 ikilinganishwa na asilimia 5.4 maeneo ya mijini.

Mkoa wa Rukwa umeonekana kuwa na kiwango kikubwa cha watoto wenye umaskini wa mahitaji ya msingi kwa asilimia 47.6 wakati mkoa wa Dar es Salaam una kiwango kidogo cha asilimia 9.6.

Pia, Mkoa wa Rukwa una kiwango kikubwa cha watoto wenye umaskini wa chakula kwa asilimia 21.2 ikilinganishwa na Mkoa wa Mara umeonekana kuwa na kiwango kidogo cha asilimia 1.9.

**Alichokisema Waziri Mkuu**

Akizindua matokeo ya utafiti huo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema kiwango cha umaskini wa kipato cha Watanzania hakitofautiani sana na nchi nyingine ndani ya Bara la Afrika.

"Tukiangalia hali ya umaskini katika nchi nyingine za Bara la Afrika kwa miaka ya hivi karibuni, nikianza na Kenya kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi ni asilimia 36.8 (mwaka 2015), Afrika ya Kusini asilimia 55.5 (mwaka 2015), Rwanda asilimia 38.2 (mwaka 2016), Zambia asilimia 54.4 (mwaka 2015), Ethiopia asilimia 23.5 (mwaka 2015) na Zimbabwe asilimia 72.3," alisema.

Alisema kupunguza umaskini kwa nchi yoyote ile kunapaswa kuhusishwa na uwekezaji kwenye sekta nyingine za kiuchumi ambazo hugusa na kuwanufaisha wananchi walio wengi.

Hata hivyo, Majaliwa alisema kaya zinazoishi kwenye makazi bora zimeongezeka kwa asilimia 16 katika kipindi cha miaka sita ikilinganishwa na hali ilivyokuwa mwaka 2011/2012.

"Kaya zinazoishi kwenye nyumba zenye paa la kisasa zilizoezekwa kwa bati zimeongezeka kutoka asilimia 68 mwaka 2011/2012 hadi kufikia asilimia 84 mwaka 2017/2018 wakati kuta za kudumu zimeongezeka kutoka asilimia 46 mwaka 2011/2012 hadi kufikia asilimia 79 mwaka 2017/2018," alisema.

**Kauli ya Mtakwimu Mkuu**

Akitoa taarifa juu ya utafiti huo, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi duniani ambazo kiwango cha umaskini kimeendelea kushuka na kufikia tarakimu moja.

Alisema utafiti huo uliofanywa na ofisi yake kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, baadhi ya balozi na mashirika ya Umoja wa Mataifa ulilenga kupata makadirio ya viwango vya umaskini ili kufuatilia, kupima na kutathmini mipango mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

## NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI,** Wanahitajika IT – Diploma, Sales Lady, Messenger – awe mvulana. Elimu kidato cha nne/ cha sita. Wawe wazoefu wa kutosha. Mawasiliano: 0715 885533. Email: jmtofficetraders96@gmail.com au jmtofficetraders@gmail.com.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA CHETI



**TEREZA ERASTO TITO** amepotelewa na Cheti cha elimu ya kidato cha nne alichosomea ktk shule ya Secondari ELLY'S, Alichomaliza mwaka 2010 na chenye **index namba S2455-0129.** Kwa yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Taarifa ya polisi; **MOR/PS/B.I/35/VOL..LXXIX/239.**

115301802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGRO.**

**MAOMBI NA.15 YA MWAKA 2019.**

**IDDI ATHUMAN NDAKI..............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**ANTAR SAID KKLEB.............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**ANTAR SAID KLEB............MJIBU MAOMBI**

Popote Ulipo Unaarifiwa Ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 12/08/2019 mwenyewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 24 Mwezi June, 2019.

115301702

## NYUMBA INAUZWA

**ROYAL RUNNER'S & COURT BROKER GEN SUPPLIES T. LTD**

**WANAUZA NYUMBA YENYE NO. CN/UH – 16/15**

IPO CHINYOYA – DODOMA, MALI YA HARUNA YAHAYA KIFIMBO, ANADAIWA NA TWALIB SHABAN ISSA MNADA UTAFANYIKA TAREHE 18/07/2019 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI.

**DIRECTOR 0713 913150**
**M.D 0715 170553.**

215301902


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Pochettino ataja kituo kinacho-fuata



**LONDON,** Engand

KOCHA Mauricio Pochettino ametaja kazi tatu atakazofikiria kuzifanya mara baada ya kuachana na Klabu ya Tottenham Hotspurs.

Alipoulizwa na redio moja nchini Hispania mapema wiki hii, kocha huyo raia wa Argentina amesema kwamba itakuwa vizuri mno kama atainoa Real Madrid, timu ya Taifa ya Argentina au klabu yake ya zamani ya Espanyol.

Real Madrid ndiko alikokuwa akihusishwa mno Pochettino mwaka jana baada ya kumtimua kocha wake, lakini wakamrudia tena Zinedine Zidane.

Akizungumza na Redio Catalunya, alisema hizo ndio sehemu ambazo siku moja anafikiria kufanya nazo kazi mara atakapoondoka pale Spurs.

Alisema: "Nilitoa neno langu wakati nasaini mkataba mpya na Tottenham. Bila shaka ndoto yangu kubwa ni kuzinoa klabu kama Real Madrid, timu ya Taifa ya Argentina au kurudi kwenye klabu yangu ya zamani ya Espanyol.

"Sikufikiria chochote dhidi ya Tottenham kwa wakati ule, lakini sasa nikiondoka hizi ndio sehemu ninazoziwaza."

Kocha huyo ameiongoza kwa mara ya kwanza Tottenham kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mwaka jana alisaini mkataba mpya wa miaka mitano ya kuendelea kukaa na Spurs, ambao utamweka hapo hadi Mei 2023.

Hiyo ilikuwa kabla ya Zidane kuondoka, lakini alipoondoka yeye ndiye aliyekuwa akitajwa zaidi kuchukua nafasi hiyo ya kuwa kocha pale Real Madrid.

# AS Roma yathibitisha Spinazzola kutua Juve



**ROME,** Italia

KLABU ya AS Roma imethibitisha kwamba, nyota wa Juventus, Leonardo Spinazzola amefanyiwa vipimo vya afya na atajiunga na timu hiyo katika dili ambalo litawahusisha mabeki wa pembeni, Luca Pellegrini na Maurizio Sarri.

Katika makubaliano waliyofikia mapema wiki hii, Juve na Roma walikubaliana kuuziana wachezaji hao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, atasaini mkataba wa muda mrefu na Roma na anatarajia kuwa mrithi wa beki wa kushoto, Aleksandar Kolarov.


Pia kwa upande wa mabingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus, Pellegrini jana alifanyiwa vipimo vya afya kwa ajili ya kujiunga na klabu hiyo kuelekea msimu mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, anachukuliwa kama nyota mpya wa timu ya Taifa ya Italia kwa siku za usoni na amesaini mkataba wa miaka mitano utakaomweka hapo Turin.

Juventus ukiacha mchezaji huyo hadi sasa wamefanya usajili wa mchezaji mmoja tu ambaye ni kiungo wa Arsenal, Aaron Ramsey.

Kwa sasa Juventus ipo chini ya kocha mpya, Maurizio Sarri ambaye alikuwa akiinoa Chelsea msimu uliopita.

# TARGETT WA SOUTHAMPTON AMWAGA WINO ASTON VILLA



**LONDON,** England

KLABU ya Aston Villa imeshinda mbio za kuipata saini ya Matt Targett wa Southampton kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 15.

Targett alilazimika kucheza kama chaguo la pili mbele ya Ryan Bertrand msimu wa 2018/19 na alicheza mechi 16 tu za Ligi Kuu chini ya kocha Mark Hughes na Ralph Hasenhuttl baada ya kuamua kurudi kutoka kwa mkopo kule Fulham.

Gazeti la The Telegraph limeripoti kwamba, Villa imeishawishi Southampton kumuachia Targett na usajili wake utatangazwa siku chache zijazo baada ya klabu hizo mbili kufikia makubaliano.

Beki huyo wa kushoto ada yake imeripotiwa kwamba itakuwa ni pauni milioni 15 ili kwenda kuitumikia Aston Villa msimu ujao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, pia alikuwa akiwaniwa na Klabu za Liverpool, Newcastle na Fulham.

HABARI MICHEZO



# Eriksen akaribia kutua Madrid

**LONDON,** England

KIUNGO wa Tottenham Hotspur, Christian Eriksen, ameripotiwa kuwa katika hatua za mwisho kabisa za kukamilisha uhamisho wake wa kwenda kujiunga na Real Madrid.

Gazeti la The Times limeripoti kwamba familia ya kiungo huyo wa kimataifa wa Denmark ilionekana huko katika mitaa ya Jiji la Madrid wakitafuta makazi ili kurahisisha mambo wakati watakapohamia kwenye jiji hilo.

Kiungo huyo wa Spurs anatazamwa na Real Madrid kama mbadala endapo watakwama kwenye mpango wao wa kumnyakua kiungo wa Manchester United, Paul Pogba.

Real Madrid sasa wanaonekana kwamba huenda wakaamua tu kupeleka ofa ya pauni milioni 100 huko Spurs kumnasa kiungo huyo baada ya kuona Man United kuamua kukomaa na kiungo wao, Pogba wakidai wanamuuza kwa pauni milioni 150.

Kabla ya msimu uliopita kumalizika, Eriksen alisema: "Nina heshimu kwa kila kitu nilichokipata hapa Tottenham. Lakini, pia ningependa kujaribu kitu kipya. Nadhani mambo yatakuwa wazi kwenye kipindi cha usajili. Huo ndio mpango.

"Itategemea na Daniel Levy. Kama kutakuwa na klabu itanitaka au kama nitakaa mezani kujadili mkataba mpya. Real Madrid? Hiyo itakuwa hatua ya mbele zaidi. Lakini, kwanza Real Madrid ni lazima wawapigie simu Tottenham na kuwaambia kwamba wanataka kumsainisha Eriksen. Na bado hawajafanya hivyo hadi kufikia sasa ninavyoelewa."

# Solskjaer akunwa usajili Wan-Bissaka



**MANCHESTER,** England

BAADA ya Klabu ya Manchester United kukamilisha usajili wa Aaron Wan-Bissaka, kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer amesema mchezaji huyo ni mmoja wa walinzi bora wakuu wanaoibuka katika Ligi Kuu ya England.

Man United ilitangaza juzi Jumamosi kukamilisha usajili wa beki huyo wa Crystal Palace kwa ada ya pauni milioni 50.

Akizungumzia usajili huo, Solskjaer ambaye amekuwa akipigania kukiimarisha kikosi chake, amesema anaheshimu kipaji cha Wan-Bissaka na hivyo ana matumaini naye makubwa.

"Ana heshimu kazi yake, ana kipaji kikubwa kitakachomwezesha kuchezea Manchester United na ana vigezo vyote vya mchezaji tunayemtaka ajiunge na kikosi chetu na bila shaka atatusaidia kufikia malengo," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

Aaron Wan-Bissaka ambaye alichezea Crystal Palace katika mechi 35 za Ligi Kuu ya England msimu wa mwaka 2018-19, alisema amefurahia mno kujiunga na timu hiyo.

"Siamini nimejiunga na Manchester Utd, kwa kweli najivunia sana usajili huu," alisema Wan-Bissaka akiwaambia waandishi wa habari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amekubali kutia saini mkataba wa miaka mitano utakaomwezesha kulipwa pauni 80,000 kwa wiki.

United ipo kwenye harakati za kuimarisha kikosi chake akiwa ni mchezaji wa tano mkubwa kusainiwa na klabu hiyo baada ya Paul Pogba, Romelu Lukaku, Angel di Maria na Fred.

Mlinzi huyo ni wa pili kusajiliwa na klabu hiyo, baada ya usajili wa kiungo wa kimataifa wa Wales, Daniel James mwenye umri wa miaka, 21, ambaye alijiunga na United kutoka Swansea kwa pauni milioni 15.

United wana nafasi ya kurefusha mkataba wa miaka mitano wa Wan-Bissaka hadi miaka sita.

Wan-Bissaka, ambaye alikuwa akitekeleza wajibu wake wa kimataifa mwezi huu katika michuano ya Ulaya ya wachezaji wa chini ya miaka 21, alijiunga na chuo cha mafunzo ya mpira Palace akiwa na miaka 11.

Nyota huyo alikuwa akilipwa pauni 10,000 kwa wiki katika Uwanja wa Selhurst Park, kiwango ambacho ni cha chini kulipwa mchezaji wa kikosi cha kwanza.

Uhamisho wake ulicheleweshwa na mashauriano ya mwisho kati ya klabu hizo, hatua ambayo iliiwezesha Eagles kupata asilimia 10 ya mauzo ya Wan-Bissaka kwa kujiunga na United kwa zaidi ya pauni pauni milioni 50.

# Wenger atajwa Newcastle

**LONDON,** Ennglanď

ARSENE Wenger amekiri kuwa na mpango wa kurudi kufanya kazi Ligi Kuu England, lakini amejiweka mbali na mpango wa kwenda kuinoa Newcastle United.

Wenger amekuwa hana kazi tangu alipoachana na Arsenal mwishoni mwa msimu wa 2017/18 baada ya kudumu kwenye timu hiyo kwa miaka 22, akibeba mataji matatu ya Ligi Kuu England na saba ya Kombe la FA.

Kocha Rafael Benitez ataondoka Newcastle mwishoni mwa mwezi huu kutokana na mkataba wake kufika mwisho na hajafikia makubaliano kwa ajili ya mkataba mpya wa kuendelea kubaki hapo.

Jambo hilo limemfanya Wenger kuwa miongoni mwa makocha wanaotajwa kwamba huenda wakaenda kupewa kazi huko St James' Park, lakini Wenger alisema kwa sasa anapumzika kwanza kabla ya kuamua kurudi rasmi mzigoni.

Wenger alihusishwa na mpango wa kujiunga na Real Madrid mapema msimu uliopita, lakini pia alitajwa huku Fulham akihusishwa na kibarua cha kuinoa timu hiyo kabla hajachukuliwa Claudio Ranieri, Novemba mwaka jana.

Wakati ikiaminika atarudi kwenye soka kama mkurugenzi, Wenger ameonekana kubadili mawazo yake na kutaka kuja kuendelea kwenye kazi yake ya ukocha.

Alisema: "Sawa, nilikuwa nafikiria kwenda kufanya kazi nchi nyingine, huo ndio ulikuwa mpango wangu baada ya kukaa kwa muda mrefu England, lakini kwa sasa huko ndiko kunakostahili kuwapo."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# JESUS KUTUMIA DARASA LA AGUERO KUIA ARGENTINA

**Ni wakati Brazil ikiivaa kesho kwenye robo fainali Copa America, asema amejifunza mengi...**

**Belo Horizonte,** Brazil

Ubinafsi wa Sergio Aguero ulisaidia kumhamasisha Gabriel Jesus kurejea katika kiwango chake, lakini straika huyo wa Brazil ataendelea "kumfurahia" mchezaji mwenza huyo wa Manchester City kama 'Selecao' wataitoa Argentina kwenye Copa America.

Jesus na wenyeji timu yake ya Taifa ya Brazil, watawavaa mahasimu wao wakubwa, Argentina katika mechi ya robo fainali itakayopigwa Belo Horizonte kesho.

Kikosi hicho cha Tite, kilihitaji matuta kuweza kuitoa Paraguay katika hatua ya 16-bora, na Jesus, ambaye alianza mechi yake ya pili, alifunga penalti ya ushindi.

**Kilikuwa kipindi cha ahueni baada ya msimu mgumu klabuni ambao nilifunga mabao saba tu kwenye Ligi Kuu, lakini matatu katika mechi mbili kwa Brazil kwa Juni hii kunaonyesha kuimarika na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alimsifu Aguero kwa mfano wa kuwa sehemu ya mafanikio yake.**

"Nilikuwa na wakati mgumu pale City mwanzoni mwa msimu uliopita, sikuwa vizuri na sikucheza sana, lakini familia na watu walionizunguka walinisaidia sana," Jesus alisema.

"Nilimtafuta mkufunzi wa utimamu kimwili kunisaidia na yeye yu pamoja nami leo.

"Na nilijaribu kipiga mashuti zaidi golini. Wastani wangu wa mashuti ulikuwa mdogo sana - kulikuwa na mechi ambazo sikuwa na shuti hata moja golini. Hivyo ni vitu vilivyonichanganya kidogo.

"Leo nataka kupiga mashuti zaidi. Hilo limebadilika sana, nikiwa pale City na hapa na timu ya taifa. Ni moja ya vitu muhimu nilivyobadilika.

"Ninaona washambuliaji wengine kama Aguero, anapiga mashuti sana langoni na hili linafanya mambo kuwa rahisi.

"Nimejifunza mengi kutoka kwake. Lakini sasa ni mmoja aliyeko katika kikosi chake na mimi kingine."

Na wakati akijiandaa kukutana na mchezaji mwenza mwingine wa City, Nicolas Otamendi, katika kile kitakachokuwa vita ya ana kwa ana, Jesus anajua kuna mengi ya hatari.

"Hizi ni timu mbili kubwa, nchi mbili zenye historia kubwa katika soka," mchezaji huyo wa zamani wa Palmeiras alisema.

"Brazil, tangu tunacheza nyumbani na ni katika wakati mzuri, kuna shinikizo kubwa la kushinda kuliko Argentina, lakini ya viwango."

## KWA UFUPI

### ZAHA KUVUNJIWA BENKI ARSENAL
Arsenal itapaswa kuilipa Crystal Palace pauni milioni 100m ili kuipata saini ya mshambuliaji wa kimataifa wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, 26, majira haya ya joto. **(Mail on Sunday)**

### LARSEN AVUTIA VIGOGO EPL
MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund, Jacob Bruun Larsen amezivutia Liverpool, Manchester United na Arsenal. Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ameichezea Dortmund mechi 30, akianza michezo 17 na kutupia mabao matatu akichomoza kwa mara ya kwanza msimu wa 2018-19. **(Mail)**

### SPURS YAIITIA MADRID ERIKSEN
MWENYEKITI wa Tottenham, Daniel Levy ameipigia simu Real Madrid akihitaji ofa ya kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 27, ambaye amekataa kuongeza mkataba na Spurs zaidi ya huu wa sasa unaomalizika majira ya joto 2020. **(Marca)**

### POGBA KULAZIMISHA KUONDOKA
KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba atafanya mazungumzo na kocha Ole Gunnar Solskjaer wiki ijayo, lengo likiwa ni kulazimisha kuondoka Old Trafford. **(Sun)**

### MBAPPE ATOA MSIMAMO PSG
MSHAMBULIAJI Mfaransa Kylian Mbappe, 20, amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake na Paris St-Germain na hana lengo la kuongeza. **(Marca)**

### MORATA ANUKIA KURUDISHWA CHELSEA
Chelsea imeitahadharisha Atletico Madrid kwamba itafuta mkataba wa mkopo wa straika Mhispania Alvaro Morata, 26, kama timu hiyo ya La Liga haitashughulikia suala la kumpa mkataba wa jumla wa pauni milioni 50 majira haya ya joto. **(Sunday Telegraph)**

### LUKAKU KUUZA WAWILI INTER
Inter Milan itatengeneza pauni milioni 75 zinazohitajika ili kuipata saini ya Mbelgiji Romelu Lukaku, 26, kutoka Manchester United kwa kumuuza Mreno Joao Mario, 26, na beki wa kushoto Mbrazil Dalbert, 25. **(Sun on Sunday)**

### WOODWARD AAHIDI MAJEMBE UTD
MAKAMU Mwenyekiti wa Manchester United, Ed Woodward amewaambia viongozi wa klabu hiyo kuwa wanampango wa kuongeza zaidi wachezaji "wakusisimua" majira haya ya joto ikiwa ni baada ya kukamilisha uhamisho wa beki Aaron Wan-Bissaka kutoka Crystal Palace. **(Sunday Telegraph)**

### LIVERPOOL YATAKIWA KUSAJILI ZAIDI
NGULI wa zamani wa Liverpool, Ray Clemence amesema mabingwa hao wa Ulaya wanapaswa kumwaga fedha zaidi sokoni kama wanataka kutoa upinzani dhidi ya Manchester City kwenye Ligi Kuu England. **(Mirror)**

### SOUTHAMPTON YAMNASA ADAMS
MSHAMBULIAJI wa Birmingham City, Muingereza Che Adams, 22, amewaaga wachezaji wenzake kabla ya uhamisho wake wa pauni milioni 16 wa kujiunga na Southampton. **(Mail on Sunday)**

### LIVER YAIACHIA UNITED FERNANDES
WANAFAINALI wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Liverpool na Tottenham wamejiweka kando katika mbio za kuisaka saini ya Bruno Fernandes, 24, hivyo kutoa nafasi kwa Manchester United kumnasa kiungo huyo wa Sporting Lisbon. **(Sunday Express)**

### POCHETTINO HANA UAMUZI USAJILI
KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino amesema hana kauli ya mwisho kuhusu suala la usajili katika klabu hiyo ya Kaskazini mwa London. **(Independent on Sunday)**

# MORIS KUPASULIWA GOTI CAIRO

**Na Somoe Ng'itu,** CAIRO

KATIKA kuhakikisha matibabu ya beki wa kati wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Aggrey Moris, yanakwenda vizuri, uongozi wa klabu yake ya Azam FC umemleta daktari wake, Mwanandi Mwankemwa ili kusimamia upasuaji wa beki huyo.

Moris aliumia goti katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Misri (Mafarao) na hivyo kutakiwa kufanyiwa upasuaji.

Kutokana na maumivu aliyopata, beki huyo akaondolewa kwenye kikosi cha wachezaji 23 wanaopeperusha bendera ya Tanzania katika fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019 na nafasi yake kuzibwa na David Mwantika, naye kutoka Azam.

Daktari Mwankemwa ametua jijini hapa juzi, na kuanza mazungumzo na daktari wa Taifa Stars, Richard Yomba, ili kufahamu kinachotakiwa kutekelezwa kwa beki huyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari Msaidizi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Mohammed Mkangara, alisema wanaamini Moris atapata matibabu mazuri jijini hapa na kurejea katika hali yake ya kawaida kabla ya msimu mpya haujaanza.

Mkangara alisema madaktari wa Taifa Stars wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na wenzao wa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara ili kuhakikisha wachezaji wanaoumia, wanapata matibabu sahihi.

"Mchezaji anapoumia anahitaji kutibiwa, na matibabu sahihi ndio yatamrejesha mchezaji katika kazi yake mapema, hiki ndio kinachofanyika kwa sasa," alisema kiongozi huyo.




Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (wa tatu kulia), akizungumza na walimu wa michezo wa Shule ya Fountain Gate Academy, wakati alipoitembelea katika uwanja wa shule hiyo, Miyuji Dodoma mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Mwakyembe apongeza vipaji Fountain Gate

**Na Mwandishi Wetu,** Dodoma

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, ameipongeza Shule ya Fountain Gate kwa kuibua vipaji mbalimbali na amewataka wachezaji soka nchini kutoridhika na mafanikio ya kuchezea Simba na Yanga.

Pongezi hizo alizitoa jana wakati alipokaribishwa kutembelea Kituo cha Michezo cha Fountain Gate Academy cha jijini Dodoma pamoja na kukagua viwanja vya michezo ndani ya shule hiyo.

Dk. Mwakyembe alisema wachezaji wengi wamekuwa wakiua vipaji vyao baada ya kuridhia kuishia kucheza soka katika klabu kubwa mbili nchini, Yanga na Simba.

Hata hivyo, baada ya kutembelea miundombinu ya viwanja na maeneo wanapoishi na kusoma vijana hao alisema ameridhishwa na kuupongeza uongozi wa kituo hicho kuibua vipaji kutoka umri wa chini.

Alisema michezo ni ajira na uchumi hivyo wachezaji wanatakiwa kuwa na kiu ya mafanikio kwa kufanya vizuri ili kuleta mafanikio katika eneo hilo.

Aidha, aliwataka makocha nchini kuwekeza kwenye kutafuta vipaji vya soko mikoani na kuacha kugharamikia wachezaji kutoka nje ya nchi.

Naye Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, alishauri timu za michezo na wachezaji kuacha kuweka imani yao kwenye ushirikina katika michezo.

"Kamati za ufundi hazima maana ya ufundi wa ushirikina au uchawi ila ni kundi la watu wenye uwezo na utaalamu katika michezo," alisema.

# Amunike atetewa vipigo Taifa Stars

**Na Shufaa Lyimo**

MWENYEKITI wa Kamati ya Waamuzi Tanzania, Salum Omande, amewataka Watanzania kuacha kumtupia lawama Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa, 'Taifa Stars', Mnigeria Emanuel Amunike, kwa timu hiyo kupata matokeo mabaya katika fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 nchini Misri.

Akizungumza na Nipashe jana, Omande alisema kocha hapaswi kulaumiwa kwani yeye tayari amefanya kazi yake ya kuwafundisha wachezaji wake na kilichokuwa kinatakiwa ni wachezaji kutekeleza walichofundishwa.

"Sioni sababu ya Watanzania kumtupia lawama yeye kazi yake ni kufundisha kazi kubwa ipo kwa wachezaji wenyewe," alisema.

"Mchezo wa kesho (leo) utakuwa mgumu kwa sababu Algeria ni timu nzuri yenye wachezaji wengi wakulipwa nje ya Afrika tofauti na sisi kwetu wapo wachache," alisema Mwenyekiti huyo.

Aidha, alisema juzi alikuwa nchini Misri na alipata nafasi ya kukaa na kuzungumza na wachezaji na kumwahidi kufanya vizuri katika mchezo wa leo.

"Nilipokuwa Misri nilipata bahati ya kuzungumza na wachezaji wa Taifa Stars kila mmoja aliniahidi ushindi na waliomba Watanzania wazidi kuwaombea ili wasiishinde," alisema.

Stars imepoteza mechi zake mbili za Kundi C baada ya kuchapwa na Senegal 2-0 na kisha Kenya (Harambee Stars) kuinyuka 3-2.

# ZFF yataka vyeti makocha wa makipa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesema halitasita kuichukulia hatua za kisheria klabu yoyote itakayomweka katika benchi la ufundi kocha wa makipa ambaye hana angalau vyeti vinavyomruhusu kufanya kazi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Ofisa Habari wa Shirikisho hilo, Adam Natepe alisema msimu huu ZFF watakuwa wakali kwa klabu zote zinazokiuka sheria kwa makocha kukaa katika mabenchi ya ufundi ambao hawana vyeti vinavyopa sifa ya kuifanya kazi hiyo kisheria.

Alisema ZFF haitasita kuichukulia hatua za kisheria klabu itakayofanya hivyo ikiwamo kuipiga faini ya Sh. 500,000 ili iwe fundisho kwa klabu zinazofanya hivyo kwa makusudi hususan katika msimu huu unaotarajiwa kuanza Agosti, mwaka huu.

"ZFF tutakuwa wakali katika suala hili tena sana, maana hili lipo kisheria, Caf na Fifa imeeleza hili, lakini baadhi ya klabu zetu za Zanzibar zimekuwa zikikaidi mno, hivyo msimu huu haitaachwa klabu ambayo itakiuka sheria hiyo," alisema.

Aidha, alisema ZFF inatarajia kufanya mafunzo ya siku saba kwa makocha wa makipa ambao hawana vyeti hivyo ni muda mwafaka kwa klabu kuwashawishi makocha wao ili kuhudhuria mafunzo hayo na kupata vyeti vitakavyowapa sifa ya kuzitumikia klabu zao.

Alisema mafunzo hayo ambayo yataanza leo Julai Mosi, lengo litakuwa kutoa fursa kwa makocha ambao hawana vyeti kupata vyeti hivyo ili msimu wa ligi ukianza waweze kutumikia klabu zao kama sheria inavyotaka.

"Tumeamua kufanya mafunzo haya kabla ya kuanza kwa msimu wa ligi kwa makusudi kabisa ili makocha ambao hawana vyeti wapate fursa ya kushiriki mafunzo na kupata vyeti vitakavyowafanya wakae katika benchi la ufundi na kuitumikia klabu yake," alisema.

Alisema ni muhimu makocha hao kuwa na vyeti ili iwe rahisi hata kupata kazi katika klabu nyingine zilizopo nje ya Zanzibar ambavyo vitawafanya kujitangaza zaidi kupitia taaluma yao.

Aidha, Rais wa Shirikisho hilo, Seif Kombo ametengua uteuzi wa Salum Ali Haji aliyekuwa mwenyekiti wa kamati ya ufundi na maendeleo ya mpira badala yake atakuwa mkurugenzi wa ufundi wa shirikisho hilo.

Michezo
Jumatatu Julai 1, 2019
Nipashe

Jesus kutumia darasa la Aguero kuia Argentina



HABARI UK. 30

## Okwi aandaliwa makubwa Simba

**Na Somoe Ng'itu,** CAIRO

WAKATI jana ikiwa ni siku ya mwisho kwa dirisha la usajili wa kimataifa kufungwa, uongozi wa Simba ya jijini Dar es Salaam umesema uko tayari kuhakikisha wanambakisha klabuni hapo mshambuliaji wake, Mganda Emmanuel Okwi, hata kwa kulipa faini, imefahamika.

Mwisho wa dirisha la usajili la Shirikisho la Soka Afrika (Caf) ilikuwa jana Julai 30 na baada ya hapo klabu zitalazimika kulipa faini ya Dola za Marekani 250 kwa kuchelewa kwa wiki moja au Dola za Marekani 500 baada ya muda huo kupita.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), pia jana lilitangaza mwisho wa usajili wa wachezaji wa Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Daraja la Pili ni Julai 31, mwaka huu, na hakutakuwa na muda wa nyongeza katika kukamilisha mchakato huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, kiongozi mmoja wa juu wa Simba jijini hapa, alisema kuwa bado Okwi ni chaguo lao na kinachofanya achelewe kusaini mkataba mpya, ni anaamini ataweza kupata timu nyingine kubwa zaidi ya mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kiongozi huyo alisema kuwa klabu yao imejipanga kutompoteza mshambuliaji huyo, kwa sababu inataka kuendeleza makali waliyoyaonyesha katika msimu uliopita kwenye ligi ya ndani na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kwa upande wa dau analotaka hatuna tatizo naye, ndio maana anasema Simba ndio ataipa kipaumbele, kinachofanyika sasa anasubiri kuona kama anaweza kubahatika kupata klabu kubwa zaidi, lakini sisi tumejipanga kutompoteza, tuko tayari kulipa na faini ya Caf," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kuwa licha ya kukamilisha mazungumzo na Mkenya Francis Kahata, bado kiungo huyo hajasaini mkataba rasmi wa kuwa mchezaji wa Simba.

"Kahata bado, ila mchakato wake uko vizuri, ni suala la muda tu haujafika, tukikamilisha, tutawatangazia katika utaratibu wetu ule ule," aliongeza kiongozi huyo.

Aliongeza kuwa Simba inaendelea kuweka mipango yake sawa sawa kwa kuhakikisha inasajili kikosi imara kwa lengo la kufanya vema zaidi katika msimu ujao.

Mbali na kuwapa mikataba mipya wachezaji wake wa zamani, mabingwa hao wameshatangaza kuwasajili nyota sita ambao ni pamoja na Beno Kakolanya, Kennedy Wilson wa hapa nchini, Gerson Vieira, Tairone da Silva, Wilker da Silva kutoka Brazil na Sharaf Ali wa Sudan.

HUPENYEZI...



Kiungo wa Chile, Arturo Vidal (kulia), akizuia shuti la mshambuliaji wa Colombia, Roger Martinez lisilete madhara langoni kwao wakati wa mechi ya robo fainali ya michuano ya Copa America iliyomalizika kwa Chile kushinda kwa mikwaju ya penalti 5-4 juzi kufuatia sare tasa. **PICHA: MTANDAO**

# ETO'O AICHAMBUA STARS, AMUNIKE ATAKA HISTORIA

Asema itakuwa tishio fainali zijazo huku akieleza namna ambavyo soka la Afrika Mashariki...

**Na Somoe Ng'itu,** CAIRO

WAKATI Kocha wa Taifa Stars, Emmanuel Amunike, akipania kufungua ukurasa wa historia mpya ya soka la Tanzania kikosi chake kitakapoivaa Algeria katika mechi ya mwisho ya Kundi C ya fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019, mshambuliaji wa zamani wa timu ya Taifa ya Cameroon, Samuel Eto'o, ameichambua na kutoa neno la faraja.

Taifa Stars, leo itashuka katika Uwanja wa Al Salaam jijini hapa, kuivaa Algeria ikiwa ni baada ya kikosi hicho cha Amunike kupoteza mechi zake mbili za mwanzo dhidi ya Senegal kwa kufungwa 2-0 na kisha kuchapwa 3-2 na Kenya, 'Harambee Stars'.

Lakini Eto'o baada ya kuitazama katika mechi hizo mbili, amesema Stars imekua na kushauri kikosi hicho kiendelee kuwa pamoja ili kuwajenga zaidi wachezaji.

Eto'o aliliambia Nipashe jijini hapa jana kuwa, Taifa Stars ambayo ameiona katika mechi mbili za hatua ya makundi ni bora, na mapungufu yaliyopo yakifanyiwa kazi, itakuwa ni timu yenye ushindani katika fainali zijazo.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid, Barcelona na Chelsea, alisema pia amebaini kuwa tayari wachezaji wa Afrika Mashariki wameanza kujitambua na kuonyesha vipaji vyao na hapo ndipo watasaidia mataifa yao kukua kisoka.

"Nimeona kuna mabadiliko sana, kuna maendeleo yameanza kuonekana, wanapambana na wanaonyesha wana vitu, katika mpira kila siku unajifunza, naona watakuwa na timu nzuri hapo baadaye ndani ya kipindi kifupi," alisema mshambuliaji huyo ambaye ni balozi wa fainali hizi za mwaka huu.

Kwa mara ya kwanza Afrika Mashariki imekuwa na timu nne katika fainali hizi, na licha ya Taifa Stars na Burundi kupoteza mechi zake mbili za kwanza, vikosi vyake vimetajwa kuimarika na kutoa upinzani kwa timu walizocheza nazo.

Taifa Stars ilianza kwa kuchapwa mabao 2-0 na Senegal wakati Burundi iliyoko katika mji wa Alexandria na inayoshiriki kwa mara ya kwanza fainali hizi yenyewe ilipoteza mchezo wake kwa kufungwa bao 1-0 na Nigeria (Super Eagles).

Wawakilishi wengine wa Afrika Mashariki ni Uganda (The Cranes) ambayo ilianza kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na mchezo wa pili ikatoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Zimbabwe wakati jana usiku ilitarajia kuwavaa wenyeji Misri (Mafarao).

Harambee Stars wao walianza kwa kufungwa mabao 2-0 na Algeria na kuwafunga Taifa Stars 3-2 na leo inatarajia kumaliza mechi zake za hatua ya makundi kwa kucheza dhidi ya Senegal.

Hata hivyo, akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Amunike, alisema kuwa kikosi chake kiko vizuri na anaamini kitaweka historia mpya baada ya kuwaambia wachezaji wake wasahau matokeo ya nyuma ambayo walipata dhidi ya Waarabu hao.

Amunike alisema amewaandaa wachezaji wake kuungalia mchezo wa leo na kuacha kufikiria matokeo ya mechi zilizopita dhidi ya Senegal na Kenya, kwa sababu katika mpira, muhimu ni kuangalia mechi iliyoko mbele na si iliyopita.

"Nakumbuka walitufunga mabao 2-0, Dar es Salaam, halafu tukatoka nao sare ya 2-2, na pia walitufunga 7-0, hiyo ni historia, sasa tunahitaji kufungua ukurasa mpya, Jumatatu (leo) tutaianza safari mpya dhidi ya Algeria, kikubwa ni kurekebisha makosa yetu," alisema Amunike ambaye jijini hapa anakumbukwa kutokana na kuwahi kuichezea Klabu ya Zamalek.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >